

**USAWAZISHAJI WA LEKSIMU KATIKA KISWAHILI:**  
**UTAFITI KIFANI WA VIHIGA**

**NA**

**ANUSU JOSHUA**

**C50/82903/2015**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2017**

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na kwa maoni yangu haijawahi kuwasilishwa na mtu yeoyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote

Sahihi..... Tarehe.....

Anusu Joshua

C50/82903/2015

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi ..... Tarehe.....

Prof. Mohamed H. Abdulaziz

Sahihi..... Tarehe.....

Bw. Basilio G. Mungania

## **TABARUKU**

### **Tasnifu hii naitabarukia wafuatao:**

Mable Vigehi Misinga (Marehemu Mamangu)

Rachael Salano (Marehemu Shangazi yangu)

### **Kisha naitabarukia wafuatao:**

Sarah Vugutsa (Nyanyangu mpendwa)

Babangu Evans Misinga Jemedai

Ndugu yangu Thomas Idiong'o Misinga

Shemeji yangu Lucy Amagove Inzilia

Mazanza Alfred (Kitinda mimba)

## **SHUKRANI**

Shukrani zangu za dhati namtolea Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, nguvu na uwezo wa kuikamilisha kazi hii.

Ninakishukuru sana chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipa udhamini wa karo ya masomo yangu ya Uzamili.

Aidha, ninawashukuru sana sana wazazi wangu wapendwa, mamangu Mable Vigehi na Babangu Evans Misinga ambao walinilea na kunielimisha. Ni kwa juhudzi zao na mapenzi yao nilipata msingi mzuri wa masomo ambao umeniwezesha kufika hapa nilipofika. Siwezi kuwasahau ndugu zangu wapendwa, Mazanza Alfred, una kila sababu ya kuendelea na masomo yako. Bw. Thomas Idiong'o na Bi. Lucy Inzilia pamoja na familia yenu, mmekuwa wakarimu na wavumilivu sana kwangu wakati nimekuwa nikizisomea shahada zangu. Elizabeth Musimbi, Geofrey Idiong'o, Serenge Julius na Otuche Maurice, siwezi kusahau undugu wenu kwangu.

Sitasahau kumshukuru Mtumishi wa Mungu Harun Menywa na familia yake. Menywa, umekuwa babangu huku Nairobi wakati nimekuwa nikizisomea shahada zangu. Mama Gladys Menywa, siwezi kusahau ukarimu wako wakati ambapo nimekuwa nikizisomea shahada zangu. David Omido, Esther Kanaiza, Shaban Felix, Emma Kanaiza na Annet Sidika, mmekuwa ndugu na marafiki wa karibu sana wakati nilikuwa nikibukua. Nilifurahia uchangamfu wenu ambauliniondolea machovu ya kusoma. Nanyi mna kila sababu ya kuendeleza masomo yenu.

Kisha ninawashukuru wasimamizi wangu, Prof. Mohammed H. Abdulaziz na Bw. Basilio G. Mungania kwa kuchukua muda wao licha ya shughuli nyingi walizokuwa nazo, walipitia kazi yangu na kunielekeza vilivyo. Nilinufaika zaidi katika vikao vyatia kiusomi tulivyofanya pamoja wakati nilipokuwa nikiandika tasnifu hii. Mawaihda na maelekezo yenu ya kitaalam yalinipa msingi bora wa kuendeleza kazi hii hadi mwisho.

Ninawashukuru sana wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Luga katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambao walinfundisha. Wahadhiri hao ni pamoja na, Prof. Abdulaziz, Prof. Habwe, Prof. Rayya Timmamy, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Mukhwana, Dkt. Olali, Dkt. Buregeya, Dkt. Mbuthia, Bw. Mungania, Dkt. Mwaliwa na Dkt. Zaja.

Aidha, ninawashukuru Wahazili Peris Kemei na Pauline Kuria wa Idara ya Kiswahili. Mlikuwa wakarimu na wenyе moyo wa kusaidia kila nilipohitaji usaidizi kutoka idarani.

Sitasahau kuwashukuru walimu wangu wote wapendwa wa shule za Msingi na Sekondari kwa kuniwekea msingi dhabiti katika elimu yangu ambao umefanya nifike mahali hapa nilipofika. Sitakosa kumtaja Bw. Hadson Otego Agumba, ulinifanya nianze kuona mwangaza masomoni wakati ambapo nilikuwa nimechelea gizani. Msingi uliouweka katika masomo yangu bado naukumbuka.

Wenzangu tulioanza nao safari hii pamoja, sitawasahau kwa mengi tuliyoyafanya pamoja ambayo yametuwezesha kufikia ufanisi huu. Marafiki wa karibu ambao ni pamoja na, Purity Kolongei, Lilian Chacha, Zipporah Kitiku, Bw. Mwaviro Ngulamu, Bw. Otwera Albert, Ngunyi Samwel na Muna Edwin. Pia ninawashukuru wenzangu wa mwaka wa kwanza katika Idara ya Kiswahili, Daniel Nyamboga, Janet na Lusige Willy.

Ninawashukuru jamaa wengine wote ambao walichangia pakubwa katika kufanikisha kazi yangu. Arnold Mmatsi na Olivia Kageha, mlikuwa wavumilivu sana wakati mkinisaidia kukusanya data yangu. Marafiki zangu, Atian, Eric Mbore, Lusige Francis, Ezekiel Atetwe, Suleiman Mwahari, Edward na Phanice Amisi, Mutunga Simon, Makabe, Michael Wafula, Owwina, Maroro, Cornelias, Elna, Nabugwere, Opiyo, Mama Mburu, Nehemiah Lubang'a, Kahi, Maggy, Chide na Keverenge. Ninawashukuru sana na wengine wote ambao walinisaidia kwa njia moja au nyininge, na ambao sijawenza kuwataja. Ninasema asante sana.

## **ORODHA YA MICHORO**

Mchoro 1: Kaunti ya Vihiga.....	3
Mchoro 2: Usimbaji wa dhana.....	14
Mchoro 3: Ubanaji wa kileksika .....	14
Mchoro 4: Upanuzi wa kileksika .....	15
Mchoro 5: Upanuzi wa Kisitiari .....	15
Mchoro 6: Chuku .....	16
Mchoro 7: Kisio la Maana .....	16
Mchoro 8: Upanuzi wa Kategoria.....	17

## **ORODHA YA VIFUPISHO**

NASA                    National Super Alliance

UKIMWI                Ukosefu wa Kinga Mwilini

ARV                    AntiRetroVirals

MCA                    Member of County Assembly

ODM                    Orange Democratic Movement

## **IKISIRI**

Utafiti huu unahuusu usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili kwa kujikita katika eneo la Vihiga lililoko Magharibi mwa Kenya. Utafiti huu unahuusu aina za mabadiliko ya maana zinazohusika katika kuelezea maana za maneno katika Kiswahili. Nadharia ya Pragmatiki Leksika ndiyo iliyotuongoza kwa kiasi kikubwa katika utafiti huu. Nadharia hii imetusaidia katika kuchunguza dhana iliyosimbwa na neno kwenye tamko na michakato ya kiakili inayompitikia msikilizaji katika kufasiri dhana iliyosimbwa na neno ili kufikia uhusiano. Katika utafiti huu, tumetoa tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na nadharia tete. Vilevile tumetoa muhtasari kuhusu kaunti ya Vihiga na soko la Mbale ambalo ni eneo la utafiti. Aidha, tumelezea umuhimu wa kufanya utafiti huu, upeo na mipaka, udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu mabadiliko ya kisemantiki na yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti. Msingi wa nadharia ya utafiti umeelezwa kwa kina pamoja na mihimili muhimu ya nadharia hii. Tulitumia mbinu za kushiriki shughuli, mahojiano, majadiliano na kurekodi miitikio ya washiriki katika kukusanya data yetu katika eneo la Vihiga. Katika utafiti huu, tumeainisha na kuchanganua aina za mabadiliko ya maana zinazotokea katika Kiswahili kwa mujibu wa Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kuna aina mbili kuu za mabadiliko ya maana zinazotokea katika Kiswahili –ubanaji wa kileksika na upanuzi wa kileksika. Sababu za usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili zimeelezwa. Ilidhihirika kwamba, sababu za mabadiliko ya maana zinazoibuka katika utafiti huu ni za kiisimu. Aidha, athari za usawazishaji wa maana zimetathminiwa. Maneno ya Kiswahili yanapata athari mbili kuu za mabadiliko ya maana ambazo ni, badiliko katika mawanda na badiliko katika tathmini. Badiliko katika mawanda linajumuisha kupanuka na kubanika kwa maana. Badiliko katika tathmini linajumuisha msawajikomaana na uemeshajimaana. Yapo maneno ambayo yanapata athari zaidi ya moja kama vile kupanuka maana na kubanika maana mtawalia au msawajikomaana na uemeshajimaana mtawalia. Mwisho, matokeo ya utafiti huu yametathminiwa na nadharia tete zote kushikiliwa. Aina mbalimbali za mabadiliko ya maana zinazotokea katika Kiswahili zilibainika na ziliweza kuelezwu kwa misingi ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Sababu za mabadiliko ya maana katika leksimu za Kiswahili zilikuwa za kiisimu na ziliibuka kutokana na miktadha ya matumizi ya maneno hayo. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba, kuna kudhoofika au kupotea kwa mawasiliano katika Kiswahili kwa sababu ya mabadiliko ya maana za maneno yanayoathiri miktadha iliyozoleka.

## MAELEZO YA ISTILAHINI

**Istilahi Muhimu:** Istilahi *usawazishaji wa leksimu, mabadiliko ya maana na usawazishaji wa maana* katika utafiti huu zimetafsiriwa kihafifu kutoka *Lexical adjustment* na *Meaning adjustment*. Dhana hizi zinakaribiana kimaana na tumezitumia kwa kubadilishabadi.

**Usawazishaji wa Leksimu** (Lexical Adjustment) Huu ni ubadilishaji wa maana ya kileksika ya leksimu kutegemea muktadha ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano ya msemaji.

**Pragmatiki** (Pragmatics) Taaluma ya Isimu inayochunguza maana ya neno kimatumizi, kimuktadha, kimazingira, kiwakati na kiutamaduni.

**Pragmatiki Leksika** (Lexical Pragmatics) Nadharia ambayo inashughulikia maana za leksimu katika matumizi yake kimuktadha.

**Semantiki Kileksika** (Lexical Semantics) Semantiki inayoshughulikia maana za kileksika za maneno.

**Implikecha za Mazungumzo** (Conversational Implicatures) Hizi ni maana ambazo msemaji hukusudia kutoa lakini hazitoi waziwazi.

**Uvutaji Fahamu** (Drawing Inference) Mchakato wa kukumbuka mambo yanayohusiana na kitu fulani kwenye kauli.

**Maarifa ya Ufahamu** (Encyclopaedic Knowledge) Ujuzi unaotumiwa kufikiria maana inayofaa kwenye kauli.

**Dhana ya Dharura** (ad hoc concept) Ni dhana ambayo inaundwa papo kwa papo pindi msikilizaji anaposikia tamko fulani.

**Michakato ya Kileksika** (Lexical Processes) Hii ni mikondo ambayo leksimu hupitia ili kuibua fahiwa au dhana mpya (dhana inayowasilishwa kwenye tamko).

**Dhana Iliyosimbwa** (Encoded Concept) Hii ni maana ya kileksika iliyoko kwenye neno.

**Dhana Inayowasilishwa** (Communicated Concept) Hii ni maana ambayo msemaji anakusudia kupitisha katika tamko.

## **TAFSIRI YA ISTILAHINI NA DHANA**

Utata wa kileksika	(Lexical ambiguity)
Vitengo vya maana	(Units of meaning)
Kiashiria mahususi cha kiisimu	(Linguistically specified denotation)
Faridi za kileksika	(Lexical items)
Vitomeo vya maarifa ya ufahamu	(Encyclopaedic entries)
Rajamu	(Brand)
Elimuawali	(Prior knowledge)
Jumuia lugha/Jamii lugha	(Speech community)
Ujumbe, muktadha na athari za kimawazo	(Content, context and cognitive effects)
Dhana ya Kimantiki	(Logical concept)
Maana za pembeni/Maana za ukingoni	(Marginal meanings)
Maana kuu	(Central meaning)
Neno jumuishi	(Superordinate word)
Uvulivuli	(Vagueness)
Maarifa ya kiusuli	(Background knowledge)
Msawajikomaana	(Pejoration)
Upanuaji maana chapwa	(Over extension)
Umeshajimaana	(Amelioration/Melioration)

## YALIYOMO

UNGAMO.....	i
TABARUKU .....	ii
SHUKRANI.....	iii
ORODHA YA MICHORO.....	v
ORODHA YA VIFUPISHO.....	vi
IKISIRI .....	vii
MAELEZO YA ISTILAHİ.....	ix
TAFSIRI YA ISTILAHİ NA DHANA.....	ixiii
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>MSINGI WA UTAFITI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi .....	1
1.1.1 Usuli wa Utafiti-Vihiga, Mbale.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	4
1.3 Maswali ya Utafiti.....	4
1.4 Malengo ya Utafiti .....	4
1.5 Nadharia Tete .....	5
1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu.....	5
1.7 Upeo na Mipaka .....	7
1.8 Udurusu wa Yaliyoandikwa .....	7
1.9 Msingi wa Nadharia .....	10
1.9.1 Uwakilishi wa Dhana.....	10
1.9.2 Semantiki Kileksika.....	11
1.9.3 Implikecha za Mazungumzo.....	11
1.9.4 Dhana za Dharura .....	13

1.9.5 Michakato ya Pragmatiki Leksika .....	14
1.9.5.1 Ubanaji wa Kileksika .....	14
1.9.5.2 Upanuzi wa Kileksika.....	15
1.9.5.2.1 Upanuzi wa Kisitiari.....	15
1.9.5.2.2 Chuku .....	16
1.9.5.2.3 Kisio la maana.....	16
1.9.5.2.4 Upanuzi wa kategoria .....	17
1.9.5.2.5 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu .....	17
1.10 Mbinu za Utafiti.....	17
1.10.1 Kushiriki Shughuli .....	18
1.10.2 Mahojiano na Mijadala.....	18
1.10.3 Uchanganuzi wa Data .....	18
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>19</b>
<b>AINA ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU .....</b>	<b>19</b>
2.1 Utangulizi .....	19
2.2 Dhana ya Muktadha .....	19
2.3 Semantiki na Pragmatiki .....	20
2.4 AINA ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU .....	23
2.4.1 Ubanaji wa Kileksika.....	23
2.4.2 Upanuzi wa kileksika.....	26
2.4.3 Upanuzi wa kisitiari.....	30
2.4.4 Chuku .....	32
2.4.5 Kisio la Maana.....	34
2.4.6 Upanuzi wa Kategoria .....	37
2.4.7 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu .....	38

2.5 Hitimisho .....	42
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>43</b>
<b>SABABU ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU .....</b>	<b>43</b>
3.1 Utangulizi .....	43
3.2 Kutokea Kisadfa.....	44
3.3 Mahitaji ya Maana Mpya .....	46
3.4 Maneno ya Kisayansi .....	48
3.5 Mwiko .....	50
3.6 Lugha Kupokezanwa Kutoka Kizazi Kimoja Hadi Kingine .....	54
3.7 Uvulivuli wa maana/Uwazi katika maana.....	56
3.8 Kupotea kwa motisha.....	59
3.9 Upolisemia .....	60
3.10 Mabadiliko kutokea katika miktadha tata .....	62
3.11 Muundo wa Msamiati.....	65
3.12 Hitimisho.....	66
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>68</b>
<b>ATHARI ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU .....</b>	<b>68</b>
4.1 Utangulizi .....	68
4.2 Kupanuka kwa Maana.....	68
4.3 Kubanika kwa Maana.....	69
4.4 Msawajikomaana.....	70
4.5 Uemeshajimaana .....	72
4.6 Kupanuka Maana na Kubanika Maana Mtawalia .....	74
4.7 Msawajikomaana na Uemeshajimaana Mtawalia .....	77
4.8 Hitimisho.....	78

<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>79</b>
<b>HITIMISHO.....</b>	<b>79</b>
5.1 Utangulizi .....	79
5.2 Matokeo ya Utafiti Huu.....	79
5.3 Mapendekezo .....	80
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>83</b>
<b>KIAMBATISHO .....</b>	
<b>SAMPULI YA MASWALI .....</b>	

## **SURA YA KWANZA**

### **MSINGI WA UTAFITI**

#### **1.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tumeelezea tatizo la utafiti. Tatizo letu la utafiti limejengeka kwa misingi kwamba, mawasiliano ni dhima ya kimsingi ya kila lugha na haja yetu ni kutaka kuthibitisha kuwa, usawazishaji wa leksimu unasababisha kupotea kwa mawasiliano katika Kiswahili. Fauka ya hayo, tumedokeza malengo yetu ya utafiti, haipothesia zimetokana na malengo yetu.

Sura hii vilevile inajumuisha usuli wa utafiti ambapo tumeelezea eneo letu la utafiti kwa kifupi na sababu ya kuchagua eneo hili la utafiti. Umuhimu wa utafiti umeelezwa kwa kutoa hoja baada ya hoja. Aidha, tumewekea utafiti huu mipaka. Udurusu wa yaliyoandikwa umekuwa wa vitengo viwili; yaliyoandikwa kuhusu mabadiliko ya kisemantiki na yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti.

Msingi wa nadharia ya utafiti umeelezwa kwa kina katika sura hii. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika ambayo iliasisiwa na Blutner (1990) kisha kuendelezwa na Wilson (2003). Nadharia hii inaelezea maana za maneno kulingana na muktadha. Mihimili muhimu ya nadharia hii imeelezwa. Mwisho, tumeelezea mbinu zetu za utafiti ambapo data yetu ilikusanya kutoka maeneo ya Vihiga, Kenya. Mbinu tulizozitumia katika utafiti huu ni pamoja na kushiriki shughuli za kila siku na wasemaji. Tulifanya mahojiano na majadiliano ya moja kwa moja katika kukusanya data zaidi. Mwisho, tulirekodi miitikio ya watafitiwa kwa kuwahoji.

#### **1.1.1 Usuli wa Utafiti-Vihiga, Mbale**

Kiswahili ni lingua franca ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, utafiti huu ulifanyika katika kaunti ya Vihiga, Mji wa Mbale ulioko katika tarafa ya Wamuluma. Tutatoa maeleo mafupi kuhusiana na sehemu hii na sababu ya kuchagua eneo hili la utafiti;

Kaunti hii inapatikana sehemu za magharibi mwa Kenya. Vihiga inapakana na kaunti za Kisumu kusini mwake, kaunti ya Kakamega kaskazini mwake, kaunti ya Nandi mashariki mwake na Kaunti ya Siaya magharibi mwake. Kaunti ya Vihiga ina maeneobunge matano ambayo ni Vihiga, Emuhaya, Sabatia, Luanda na Hamisi. Kaunti hii ina jumuia ya watu takribani 554, 622. Wakaazi wengi wa Vihiga wanatumia Kiswahili kama lugha yao ya pili kwa wingi. Hivyo basi, wanao

umilisi wa kiwango fulani wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, wasemaji wengi wanatumia Lulogooli, Kitiriki na Kinyore kama lugha yao ya kwanza au lugha yao ya mama. Yapo makundi mengine machache ambayo yanatumia Lwidakho, Kikikuyu na Kisomali. Lulogooli, Kitiriki, Kinyore na Lwidakho ni mionganini mwa lahaja za Kiluhya. Kwa ujumla, Mji wa Mbale una wasemaji wengi wa lahaja ya Lulogooli.

Sababu ya kuchagua eneo hili la utafiti ni kutokana na ugunduzi wetu kuitopia uchunzaji kuwa, wakaazi wengi katika eneo hili na maeneo mengine ya magharibi mwa Kenya wana mazoea ya kufanya ubunaji wa maana na ule wa kileksimu kwa kiwango cha juu zaidi katika Kiswahili. Sababu mojawapo ikiwa ni kutokana na athari za lugha zao za kwanza. Hivyo basi, Vihiga ilikuwa ya muhimu katika sehemu ya magharibi kutokana na idadi nzuri ya lahaja za Kiluhya zinazopatikana eneo hili. Wingi wa lahaja hizi umeathiri ubunaji wa maana katika Kiswahili kwa kiwango fulani. Aidha, kutokana na ubunaji wa maana pamoja na aina nyingine za mabadiliko ya maana, sehemu hii ilitufaa sana katika kupata data ya kiasi cha haja katika utafiti wetu.

Kwa ujumla, Kiswahili na Lulogooli ama zilitumiwa kwa kuchanganya msimbo au zikiwa kwa upekee wake kulingana na sababu za kimawasiliano za msemaji. Hali hii ilijitokeza hivyo hivyo katika matumizi ya Kiswahili na lahaja nyingine tulizozitaja.

Katika utafiti huu, tulikusanya data yetu katika soko la Mbale na maduka yanayolizunguka soko hilo. Mbale ni mji ulioko kati ya mji wa Kisumu na Kakamega katika barabara kuu ya Kisumu-Kakamega. Mbale ndiyo makao makuu ya kaunti ya Vihiga na ndicho kitovu cha wasemaji wa Lulogooli. Tulikusanya matamko yetu kutoka muktadha wa sokoni pamoja na mazungumzo ya kawaida. Mazungumzo ya kawaida huweza kutokea katika miktadha mbalimbali kama vile nyumbani, viwandani (Habwe n.w. 2010). Habwe n.w. (keshatajwa) wanaongezea sifa moja mionganini mwa nyingine kwamba, mazungumzo ya kawaida yana sifa ya kuweza kubadilisha mada. Kwa sababu ya mahitaji yetu ya data ya kiasi cha haja, mazungumzo ya kawaida yalikuwa ya muhimu kwani yalitokea katika miktadha tofautitofauti na hayakujifunga kwenye mada moja. Hata hivyo, Kiswahili kinatumia katika shughuli na miktadha tofautitofauti kama vile sokoni, maabadini, katika magari ya uchukuzi, shulenii, mitaani, nyumbani na katika shughuli za benki katika eneo hili.

## Mchoro 1: KAUNTI YA VIHIGA

## Wamuluma

Eneo la Utafiti

West  
bunyor

C.  
bunyore

N.E  
Bunyore

Sabatia west

Chavakali

Lyzava

Busali

Muhudu

Shiru

Wemlab

## Wamuluma

Gisambai

Banja

Luanda Township

Mwibona

Emabungo

Mungoma

## South maragoli

Tambua

Kilomita

N-18

# Eneo la Vihiga Nchini Kenya



## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Mawasiliano ni dhima kuu katika ulimwengu wa lugha yoyote ile. Mawasiliano ni njia ya kupidisha ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine au wengine, lengo likiwa ni kuelewana. Ujumbe unapopitishwa kutoka kwa mtu hadi mwingine, kunaweza kutokea ama utata wa kimawasiliano, au kupotea kwa mawasiliano.

Utata wa kimawasiliano na kupotea kwa mawasiliano mara nyingi hutokea mionganoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili katika eneo la Vihiga. Wasemaji wa lugha huwa na ari, haja, matamanio na mahitaji ya kutaka kupidisha ujumbe fulani kwa njia fulani bila ya kukosesha mawasiliano. Aidha, wao huwa na hamu ya kuwasilisha ujumbe fulani na mara nyingine wakapata kuwa ni vigumu kwao kupidisha ujumbe huo. Usawazishaji wa leksimu ni ugeuzaji wa maana ya kileksika ya neno kulingana na muktadha kwa malengo ya kupidisha ujumbe fulani. Hivyo basi wasemaji wanapopata ugumu huo, wao hulazimika kusawazisha maana za maneno ili waweza kupidisha ujumbe wao kwa njia rahisi. Hali hii husababisha neno hilo kupata maana mpya ambayo huweza kutofautiana kwa kiasi fulani na maana yake asilia. Maana mpya zinazozuka huweza kusababisha kudhoofika kwa mawasiliano au kutokea utata wa kimawasiliano zinapotumiwa katika miktadha tofauti na ile iliyozoleka na wasemaji. Kwa kifupi, hizi maana mpya huweza kuathiri miktadha iliyopo tayari ya matumizi ya maneno. Maswali yafuatayo yalituongoza katika kutatua tatizo letu,

## **1.3 Maswali ya Utafiti**

- i. Je ni aina zipi za usawazishaji wa leksimu zinazotokea katika Kiswahili?
- ii. Je ni sababu zipi zinazopelekea usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili?
- iii. Je, ni athari zipi zinazoletwa na usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili?

## **1.4 Malengo ya Utafiti**

Malengo yafuatayo yalituongoza katika kuyajibu maswali yetu;

- i. Kutambua na kuelezea aina za usawazishaji wa leksimu zinazotokea katika Kiswahili.
- ii. Kuchunguza sababu zinazopelekea usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili.
- iii. Kueleza athari za usawazishaji wa leksimu zinazotokea katika Kiswahili.

## **1.5 Nadharia Tete**

Nadharia tete zifuatazo zilituongoza katika utafiti huu;

- i. Aina za usawazishaji wa leksimu kama vile ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kileksika, upanuzi wa kisitiari, chuku, kisio la maana, upanuzi wa kategoria na ubunaji wa maana mpya zinatokea katika Kiswahili.
- ii. Sababu zinazopelekea mabadiliko ya maana za leksimu katika Kiswahili ni za kiisimu na zinatokana na mawasiliano katika miktadha.
- iii. Mabadiliko ya maana ya leksimu yanababisha kuvunjika kwa mawasiliano mionganoni mwa wazungumzaji.

## **1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu**

Utafiti huu utakuwa wa muhimu kwa sababu zifuatazo;

Kwanza, utafiti huu utaweza kusaidia katika kutatua matatizo ya mawasiliano mionganoni mwa wawasilianaji mbalimbali wa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu leksimu fulani zilizobadilika maana na kuzua fahiwa mpya huweza kutumiwa na watu wa kundi fulani au umri fulani bila kujali iwapo wenzao wanaelewa maana hizo. Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa kuwa umethibitisha maana mpya na miktadha mipy ya maneno ambayo inazuka mionganoni mwa wasemaji wa Kiswahili, jambo ambalo litasaidia katika kutatua mawasiliano.

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wanaleksikografia katika kuunda makamusi ya Kiswahili. Mfano; vikoa vya maana vitapanuliwa na maana mpya za maneno zitaongezwa kwenye leksimu ambazo tayari zipo kwenye makamusi. Jambo hili litasaidia katika kuendeleza msamiati wa lugha ya Kiswahili. Kwa sasa yapo maneno ambayo yameweza kupanuliwa maana yazo katika makamusi na ambayo hayakuwa na maana hizo. Maana nyingi mpya zimetokana na matumizi ya Kiswahili katika miktadha mipy. Aidha, wataweza kubainisha maneno ambayo maana zake zinaffia kimatumizi au maana zake zimekwisha kufa katika matumizi ya Kiswahili. Utafiti huu utawasaidia katika kufufua maana hizo. Zaidi ni kwamba, utafiti huu utawasaidia wanaleksikografia katika kuchunguza etimolojia ya maneno mapya yanayobuniwa pamoja na maana mpya za maneno yaliyoko tayari katika lugha ya Kiswahili. Jambo hili litakuwa la muhimu sana hasa katika kuunda makamusi ya etimolojia ya Kiswahili. Kwa ujumla, marekebisho haya yatarahisisha na kusawazisha mawasiliano katika ulimwengu wa Kiswahili.

Utafiti huu utawasaidia wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya kigeni au lugha ngeni. McMahon (1994) anadokeza kwamba ...neno huelekea kupata maana mpya kutokana na matumizi yake na kikundi fulani cha kijamii au neno likitumika katika fahiwa mahususi na kikundi fulani huja kuwa katika desturi ya kawaida na maana iliyoongezeka. Wanaojifunza Kiswahili wataweza kubainisha leksimu ambazo zimeongezewa maana mpya mbali na maana zake asilia. Maana hizi zilizoongezeka kwenye neno na kuzooleka katika matumizi ya lugha zikieleweka na wanaojifunza Kiswahili au kurasimishwa katika Kiswahili, basi hapatakuwa na utata wa mawasiliano kwa wanaojifunza lugha hii.

Aidha, matokeo ya utafiti huu ni ya muhimu kwa watoto wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Ullmann (1972) akimnukuu Meillet (1948) anaeleza kuwa, lugha hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kukoma. Kwa sababu hii, kila mtoto anapaswa kujifunza lugha upya. Baadaye watoto wataelewa maana za maneno vinginevyo. Hata hivyo wao hurekebishiwa lakini kwa namna nyingine wakikosa kurekebishiwa kunaweza kutokea mabadiliko ya kisemantiki katika kizazi kipyga. Watoto wanaojifunza Kiswahili watafaidika na utafiti huu zaidi na hii itazuia mkorogano wa maana na fahiwa za leksimu katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Tena, mwanya wa kimawasiliano kati ya vizazi utakuwa umezibwa.

Fauka ya hayo, utafiti huu utawafaa zaidi wapangaji lugha katika kuangazia mabadiliko yanayotokea katika lugha ya Kiswahili kisha kuipanga kimuundo. Kwa mfano; utafiti huu utakuwa wa faida katika kuirekebisha lugha ya Kiswahili, katika uasiriaji na katika usanifishaji wa maneno yanayopitia mabadiliko ya maana. Utafiti huu utawawezesha wapangaji lugha kuchunguza miundo mipyga ya maneno na kuifanya marekebisho ili kukidhi mahitaji ya mazungumzo na maandishi katika Kiswahili.

Mwisho ni kwamba, Nadharia ya Pragmatiki Leksika tulioitumia katika utafiti huu itakuwa ya manufaa katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano; nadharia hii itawafaa watafiti wengine ambao watakuwa na haja ya kuitumia katika kuchanganua na kuchunguza masuala ya Kiisumu pamoja na ya Kifasihi katika Kiswahili. Zaidi ni kwamba, utafiti huu utakuwa ni kielelezo cha kuonesha kwamba, Nadharia ya Pragmatiki Leksika inafaa zaidi katika kuchunguza mabadiliko ya maana kimuktadha katika Kiswahili, ikumbukwe kwamba, nadharia hii inakua kwa haraka sana kimaendeleo.

## **1.7 Upeo na Mipaka**

Usawazishaji wa lesksimu ulioshughulikiwa katika utafiti huu ulihusu dhana iliyosimbwa kwenye neno katika tamko hadi dhana inayowasilishwa na msemaji. Pale ambapo tulilazimika kutumia makamusi katika kukisia au kupata maana iliyosimbwa na leksimu au maana inayowasilishwa na msemaji, tulifanya hivyo. Makamusi ya hivi maajuzi yalitumiwa. Kiswahili ni lugha iliyo na lahaja takribani ishirini. Tulizingatia mabadiliko ya maana yanayotokea katika leksimu za Kiswahili sanifu pekee. Tunachukulia kwamba, usawazishaji wa leksimu unatokea katika Kiswahili sanifu kwa wingi kuliko katika lahaja zake. Hii ni kwa sababu ni wazi kwamba, Kiswahili sanifu kinatumika katika miktadha minge kuliko lahaja zake.

Pili, utafiti huu ulihusu usawazishaji wa maana katika matumizi ya kila siku ya Kiswahili. Hatukushughulikia mabadiliko ya kihistoria ya maana za maneno hayo. Hii ni kwa sababu, lengo hasa la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kuvunjika au kudhoofika kwa mawasiliano mionganoni mwa wawasilianaji wa lugha ya Kiswahili. Tulitumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika katika kuainisha aina za mabadiliko ya maana. Katika kuainisha sababu za mabadiliko ya maana, tulitumia uainishaji wa Palmer (1981) na Ullmann (1972, 1970). Mwisho, athari za mabadiliko ya maana ziliainishwa kwa mujibu wa Ullmann (keshatajwa). Tulifanya hivi, kwa sababu wataalamu tofauti wanaainisha aina, sababu na athari tofautitofauti za mabadiliko ya maana na wakati mwingine kunatokea mwingiliano.

Mwisho na muhimu ni kwamba, dhana ambazo tulichagua kuwa ndizo dhana zinazowasilishwa na msemaji katika matamko zilikuwa za uchukulio. Hii ni kwa sababu utafiti huu haukuwa wa kisaikolojia na hatukuwa na vyombo vya kutuwezesha kufikia dhana faafu za msikilizaji wakati anapofanya mchakato wa kufikia dhana inayowasilishwa kwenye tamko.

## **1.8 Udurusu wa Yaliyoandikwa**

Udurusu wetu wa yaliyoandikwa ulikuwa wa vitengo viwili; udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu mabadiliko ya kisemantiki au ya maana na yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti:

Bloomfield (1933) anaelezea aina za mabadiliko ya maana katika lugha. Anaainisha mabadiliko mawili makuu ambayo ni kutanuka kwa maana na kubanwa kwa maana. Mabadiliko haya mawili yanaweza kusababishwa na mabadiliko mengine madogo kama vile chuku na sitiari. Kazi hii

ilitusaidia katika kuelezea aina za mabadiliko ya maana zinazotokea katika Kiswahili. Aidha, kazi hii ilitufaa katika kuelewa jinsi aina za mabadiliko ya maana zinavyoolezwa.

Habwe (1999) alichanganua diskosi ya hotuba za kisasa za Kiswahili kwa kutumia Nadharia ya Ushirikiano mionganoni mwa nadharia nyingine. Alichunguza namna implikecha zinavyoundwa katika kufasiri ujumbe ulioko kwenye matamko ya wanasiasa. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa implikecha za mazungumzo zinavyoundwa katika Kiswahili. Pia, kazi hii ilitufaa sana katika kuelewa namna masuala ya kipragmatiki yanavyoolezwa hasa katika diskosi za Kiswahili. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa tulishughulikia maana za maneno katika matamko kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika.

Carston (2002) ameeleza kwa undani baadhi ya mihimili muhimu ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kwa mfano, ameeleza jinsi msikilizaji anavyouna dhana za dharura, pia ameeleza michakato ya Pragmatiki Leksika ambayo ni muhimu katika kufasiri ujumbe. Aidha, ametoa maelezo ya kiulinganuzi ya baadhi ya michakato hii kama vile upanuzi wa kileksika na ubanaji wa kileksika. Pia ameeleza kwa undani upanuzi wa kisitiari kwa kubainisha jinsi dhana zilizosimbwa na sitiari zinaweza kusimbiliwa na msikilizaji. Kazi hii ilikuwa ya muhimu katika kuelewa michakato ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika na kuitumia katika Kiswahili.

Muyuku (2009) alichunguza uchanganyaji wa lugha katika matangazo ya benki ya *Commercial banks* na *Mobile telecommunicatons* kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kwa mfano, alichunguza dhana zinavyosimbwa ili kuwashawishi wateja. Alielezea namna dhana hizi zinavyosimbwa na kusimbiliwa na umuhimu wake katika kuwashawishi wateja. Aidha, aliweza pia kuchuguza lugha zinavyotumiwa kwa kuzichanganya. Ilionekana kwamba, Kiswahili kilikuwa ni mojawapo ya lugha iliyotumiwa kwa wingi. Maneno yake yakitumiwa kwa pamoja na yale ya lugha nyingine. Utafiti huu ilitufaa kwani uliweza kutupa mwelekeo wa namna leksimu za Kiswahili zinavyosimbwa na kusimbiliwa. Tofauti na utafiti wetu ni kwamba, tulishughulikia usawazishaji maana katika Kiswahili sanifu pekee.

Wambugu (2010) alichanganua mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya Kikikuyu chini ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Alichunguza sababu zinazopelekea mabadiliko ya kisemantiki katika Gikuyu. Katika utafiti wake, aliweza hasa kujikita katika sababu zinazoelezwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Aidha, aliweza pia kuchunguza jinsi Nadharia ya Pragmatiki Leksika

inavyoweza kutumiwa katika kufanya utatuzi mawasiliano mionganini mwa wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu. Utafiti huu ulitusaidia kuchunguzia mabadiliko mengine ya maana ambayo yametokea katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu Kikikuyu na Kiswahili ni lugha za kibantu na Kikikuyu ni mojawapo ya lugha jirani ya Kiswahili katika matumizi yake.

Njimu (2010) alichanganua matumizi ya leksimu katika magazeti ya michezo chini ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Alikuwa na lengo la kubaini umuhimu wa muktadha katikauzuaji wa dhana za dharura. Alitumia magazeti matatu yanayopatikana nchini Kenya; *The Nation*, *The Standard* na *The star*. Alifanikiwa katika utafiti wake kwa kuangazia matumizi ya dhana za dharura katika michakato ya kileksika ya ubanaji na upanuzi wa maana. Utafiti wake ulikuwa wa muhimu kwani ulitusaidia katika kuelewa namna dhana za dharura zinavyojitokeza katika muktadha.

Ochoki (2010) alikusanya data kutoka kwenye mtandao na kuifanyia majoribio Nadharia ya Pragmatiki Leksika katika kuchunguza maana zilizosimbwa katika nyimbo za *Hip hop* za Kenya. Alichanganua data yake kwa kutumia vipengele kama vile upanuzi na ubanaji wa maana za maneno. Utafiti huu ulitufaa katika kuelewa jinsi dhana zinavyosimbwa na kusimbuliwa katika Kiswahili kwani baadhi ya nyimbo zimetumia maneno ya Kiswahili.

Ochichi (2013) alishughulikia umaanisho na usimbaji maana kimazungumzo katika Kiswahili na Ekegusi. Alitumia Nadharia ya Uhusiano katika kuchunguza kategoria za kileksika na kategoria za kimuktadha. Aidha, aliangalia uwazi na umaanisho wa kauli katika Kiswahili na Ekegusi ambapo ilimbainikia kwamba lugha hizi zilitumia mitindo tofauti kuzua umaanisho. Pia tofauti za kiuteuzi wa maneno zilibainishwa katika lugha hizi. Utafiti huu ulitusaidia katika kuelewa namna usimbaji unavyotokea katika Kiswahili. Vilevile Nadharia ya Uhusiano aliyoitumia ilikuwa ya manufaa kwetu hasa katika tafsiri ya baadhi ya istilahi kwa sababu Nadharia ya Pragmatiki Leksika ni nadharia ndani ya Nadharia ya Uhusiano. Tofauti na utafiti wetu ni kwamba tulitumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika kwa upana wake na tulichunguza usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili pekee.

Simiyu (2016) alishughulikia namna taswira ya wanaume na wanawake inavyojitokeza katika nyimbo teule za tohara za Bukusu. Alitumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika katika kuchanganua faridi za kileksika zilizotumiwa katika nyimbo hizi. Aliweza kuchunguza michakato kama vile

ubanaji, upanuzi, sitiari na kinaya katika leksimu na ilimbainikia kwamba, faridi za kileksika zilitoa ujumbe tofauti kwa wasikilizaji. Utafiti huu ulitusaidia katika kuelewa namna faridi za kileksika zinavyochanganuliwa kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika.

### **1.9 Msingi wa Nadharia**

Tuliongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Nadharia hii ina mihimili mingi ila tulielezea mihimili ambayo tuliona itakuwa ya muhimu katika utafiti huu;

Nadharia ya Pragmatiki Leksika ilianzishwa na Blutner mwaka wa (1990). Baadaye iliendelezwa na Wilson (2003) katika miadhara yake katika chuo kikuu cha Havard. Mtazamo huu unachanganua maana kupitia muktadha, hivyo basi ni mtazamo faafu katika kuwakilisha dhana.

Nadharia hii inajikita katika stadi za mabadiliko ya maana. Mtazamo wa Pragmatiki Leksika unaelezea mwelekeo kwamba, faridi za kileksika za lugha zinachanganuliwa kiutaratibu na kufasiriwa kulingana na muktadha mahususi.

Mchango wa semantiki katika ufasiri wa kijumla wa tamko umebanwa kuliko ilivyodhaniwa mwanzoni. Pragmatiki Leksika inajaribu kuelezea fenomena za kipragmatiki ambazo zimeunganika na semantiki hiyo chini ya umahususi wa faridi za kileksika.

#### **1.9.1 Uwakilishi wa Dhana**

Dhana ni uwakilishi wa kiakili ambao unaweza kutwaliwa na kutoweka. Uwakilishi huu wa kiakili unafanya kazi kama kitomeo kwa fahamu zinazowakilishwa kiakili. Vitajwa ambavyo kawaida huwaziwa tunapolisoma neno vinaonekana kama utambuzi wetu wa maneno hayo. Vitajwa ambavyo kwavyo tunafanya uwaziaji huu ni dhana za maneno ambazo tunazo tayari (Murphy 2003). Murphy (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba, namna tunavyoyatumia maneno ni tofauti kwa kiasi fulani na imani zetu kuhusu namna maneno hayo yanavyotumiwa.

Wilson (2006-07) anaeleza kwamba, katika kile kielelezo rahisi cha semantiki, maneno yanachukuliwa kama yanayosimba dhana na dhana zinachukuliwa kama zinazoashiria kategoria ya vitajwa, nyakati au sifa katika ulimwengu (au katika ulimwengu tofauti mbadala unaopatikana). Wilson (2006-07) anaendelea kueleza kuwa, njia moja ya kuelezea ni kusema kuwa kuna mwanya kati ya dhana iliyosimbwa na neno na dhana ya tamko (au usemi) kwa matumizi ya neno hilo katika wakati mahususi. Mwanya ulioko kati ya dhana iliyosimbwa na dhana inayowasilishwa kwa

matumizi ya neno unapeana data ya msingi ya Pragmatiki Leksika, na lengo kuu la Pragmatiki Leksika ni kuelezea namna wasikilizaji hubana mwanya huo.

Mtazamo wa Pragmatiki Leksika unajumuisha nadharia mbili:

1. Semantiki kileksika
2. Implikecha za mazungumzo

### **1.9.2 Semantiki Kileksika**

Semantiki kileksika inashughulikia maana ya neno. Maneno yanaweza kuchukuliwa kuashiria vitu katika ulimwengu au katika dhana kutegemea mtazamo mahususi wa semantiki kileksika. Vitengo vya maana katika semantiki kileksika ni vitengo vya kileksika ambavyo kwavyo msemaji anaweza kuongezea kwa mfululizo maishani pamoja na ujifunzaji wa maneno mapya na maana za maneno hayo (Mmbwanga 2010) mfano;

Neno *baba* lina maana ya kiisimu ya mzazi wa kiume. Neno hili limeongezewa fahiwa mpya ya *mbabe wa kisiasa wa jinsia ya kiume*. Hii inaonesha kwamba binadamu wana uwezo wa kuongezea vipashio vipya vya maana kwenye maneno.

### **1.9.3 Implikecha za Mazungumzo**

Marmaridou (2000) akimnukuu Grice (1975) anaeleza kuwa implikecha za mazungumzo ni fahamu ambazo huibuka wakati wa mazungumzo kwa misingi ya *kanuni* fulani zilizo chini ya maingiliano ambazo wazungumzaji huonekana kuzingatia au kuvunja, huku *wakiwasiliana kiuhusiano* baina yao. Hivyo basi, implikecha ni fahamu za kipragmatiki.

Grice alianzisha imani kwamba, ‘si kila ukweli kuhusu matumizi ya neno unaleta utambuzi wa moja kwa moja hadi kwenye maana ya neno’. Hata hivyo, utofauti wake dhabiti kati ya kile kinachosemwa (semantiki) na kile kinachomaanishwa (uundaji wa implikecha) hauzingatii michakato ya kipragmatiki katika mawasiliano. Implikecha ya mazungumzo hivyo basi, haihusishwi na usemi wowote ila kama kawaida hupata ufahamu kutokana na matumizi ya tamko fulani kutoka kwenye muktadha (Levinson 1983).

Levinson (1983) anataja kuwa, nadharia ya Implikecha ya Grice ni nadharia kuhusu namna watu wanavyotumia lugha. Anaendelea kueleza kuwa, mapendekezo ya Grice ni kuwa kuna seti ya

machukulio yanayoelekeza matendo katika mazungumzo. Grice anajitokeza na maelekezo manne ya kanuni za mawasiliano ambazo kwa pamoja hudhihirisha kanuni ya ushirikiano;

### **Kanuni ya Ushirikiano**

Katika kanuni hii Grice anaeleza kuwa:

Uufanye mchango wako wa kimazungumzo jinsi inavyohitajika, katika mahali unapotoka, kulingana na mwelekeo au sababu inayokubalika ya mazungumzo ambamo unashiriki. Kwa kuchukulia kuwa kanuni hii hutumika kila mara katika mawasiliano, Grice alitofautisha kategoria nne ya matumizi maalumu ya kanuni hii chini ya kanuni au vikanuni mahususi. Kanuni hizo ni Idadi, Ukweli, Uhusiano na Namna. Tutaelezea kwa kifupi kila mojawapo ya kanuni hizi;

### **Kanuni ya Idadi**

- a) Uufanye mchango wako uwe na ujumbe unaohitajika (kwa ajili ya mawasiliano ya wakati huo)
- b) Usiufanye mchango wako kuwa na maelezo yanayozidi yanayotakikana.

### **Kanuni ya Ukweli**

Jaribu kuufanya mchango wako kuwa wa kweli.

Vikanuni,

- a) Usiseme kile unaamini ni uwongo.
- b) Usiseme kile ambacho huna ushahidi wake.

### **Kanuni ya Uhusiano**

Toa mchango unaohusiana na yanayozungumziwa (muktadha)

Grice anataja kuwa kuvunjwa kwa kanuni hii ni jambo linalotokea kwa nadra labda kwa sababu ni vigumu kutunga majibu ambayo sharti yaeleweke bila kutoka nje ya mada.

### **Kanuni ya Namna**

Toa mchango wako kwa jinsi iliyowazi na inayoelewaka

Vikanuni,

- a) Sema mambo waziwazi
- b) Jiepushe na utata
- c) Usiseme maneno mengi kupindukia

Anavyoeleza Marmaridou (2000) ni kuwa kwa kuzingatia kanuni hizi, wanaozungumza wanazungumza kwa njia fanifu na ya kiushirikiano. Wanazungumza na kuchukulia kuwa wasikilizaji wao wataongea kwa ukweli, kiuhusiano na kinachozungumziwa, na wazi wanapotoa ujumbe wa kutosha. La muhimu ni kuwa hata wakati ambapo mazungumzo hayaendelei kulingana na kanuni hizi, msemewa/msikilizaji huchukulia kuwa kanuni hizi zimezingatiwa katika viwango vya ndani zaidi na anatumia uwezo wake wa kufikiri kuchakata namna ambavyo kanuni ya ushirikiano inavyohusika.

Grice anaeleza kuwa, kanuni hizi zinaweza kuvunjwa au kukiukwa katika mawasiliano ya binadamu. Hata hivyo, anasisitiza sharti kuwepo na ushirikiano. Namna moja ya kuzivunja kanuni hizi ni kuzikiuka au kuzipuuza, ambayo imezua tamathali za usemi nyingi.

#### **1.9.4 Dhana za Dharura**


Wanadamu wanaweza kuunda dhana za dharura katika kielelezo cha dhana zilizoko tayari kwa kutumia chukulizi za kimuktadha ambazo zinatokana na vitomeo vya maarifa ya ufahamu ya dhana zilizoko tayari na zilizo na maana tofauti. Dhana ya dharura ni ile ambayo inaundwa papo kwa papo, ile ambayo kwayo, kuna uwezekano kuwa mtu hawezi kuwa ameiunda tayari (Horn na Ward, 2004).

Kulingana na Carston (2004) istilahi *dhana ya dharura* inaashiria dhana ambazo zinaundwa kipragmatiki na msikilizaji wakati anapojaribu kuelewa tamko. Dhana za dharura hazipatikani kiisimu lakini zinategemea kuundwa kwa miktadha mahususi na kulingana na matarajio mahususi ya uhusiano. Watu wanaweza kujumuisha jumbe tofauti kutoka kwenye kumbukizi za kiusuli za kiakili katika vitomeo vyake vya maarifa ya ufahamu ili kuunda dhana bainifu za kategoria moja.

Nadharia ya Pragmatiki Leksika ina lengo kuu la kuelezea jinsi wasikilizaji wanaziba pengo kati ya dhana iliyosimbwa na dhana inayotokana na matumizi ya neno. Dhana ni mada iliyoko kwenye

kumbukizi za kiakili ambayo ni sehemu ya uwakilishi wa kidhana wa matamko au wa mawazo (Sperber na Wilson, 2007-2008).

*Mchoro 2: Usimbaji wa dhana*



*Mchoro 2: Kutoka Wilson D. 2006-2007*

Mfano; dhana NDEGE ambayo imesimbwa na neno *ndege*<sup>1</sup> inaashiria kategoria ya ndege na inachochea maarifa ya ufahamu ambayo yanaweza kuongezwa kwenye dhana hiyo na kutumiwa katika kuelewa matamko kuhusiana na ndege. Maarifa haya ya ufahamu ndiyo yamebeba dhana ya dharura ambayo kawaida ni ubanaji wa dhana iliyosimbwa NDEGE kuashiria kikundi cha aina fulani ya ndege pekee au upanuzi wa dhana iliyosimbwa NDEGE kuashiria ndege na vitu vingine.


### 1.9.5 Michakato ya Pragmatiki Leksika

Kuna michakato ya aina tofautitofauti ya Pragmatiki Leksika ambayo inaendana na namna dhana inayowasilishwa na neno inaweza kutofautiana na dhana iliyosimbwa. Mifano tulioitoa katika kuelezea michakato hii ni ya Wilson (2003). Michakato hii ni pamoja na;

#### 1.9.5.1 Ubanaji wa Kileksika

Wilson (2003) anaeleza kuwa, hii ni hali ambapo neno linatumwiwa kuonesha fahiwa mahususi zaidi kuliko ile iliyosimbwa, inayosababisha kutokea kwa ufinyu wa maana halisi mahususi ya kiisimu. Matokeo ya ubanaji ni kuonesha kisehemu mahususi cha maana mahususi ya kiisimu.

*Mchoro 3: Ubanaji wa kileksika*



<sup>1</sup> Ndege katika mchoro 2. inaashiria ndege mnyama katika Kiswahili.

(Mchoro kutoka: Wilson D. 2006-07)

Mfano;


1. Madaktari wote *wanywa*.

*Kunywa* inaonekana kuperitisha fahiwa kuwa si *kunywa* tu kitu chochote kiowevu bali inapitisha fahiwa mahususi ya *kunywa* pombe.

### 1.9.5.2 Upanuzi wa Kileksika

Huu ni mchakato ambao kwao neno linatumiwa kuonesha fahiwa ya kijumla zaidi kuliko ile iliyosimbwa, huku tukiwa na mfululizo wa upanuzi wa maana mahususi ya kiisimu (Wilson na Carston 2007).

*Mchoro 4: Upanuzi wa kileksika*




(Mchoro kutoka: Wilson D. 2006-07)

### 1.9.5.2.1 Upanuzi wa Kisitiari

Hili ni aina ya badiliko la kisemantiki ambalo kwalo neno au kirai kinachoashiria kiuwazi wazo moja kinatumika katika nafasi ya neno jingine kuashiria mfanano kati yayo, kwa mfano;

*Mchoro 5: Upanuzi wa Kisitiari*



(Mchoro Kutoka: Wilson D. 2006-07)

Mfano;


2. Mary ni *waridi*...

*Waridi* inaweza kuonekana kwamba inawasilisha vitu dhaifu, vya kupendeza, vinavyodharaauliwa kwa urahisi na ambavyo kwavyo, *waridi* ni kategoria inayotambulika.

### **1.9.5.2.2 Chuku**

Wilson (2006-07) Chuku inaweza kuonekana kama aina ya upanuzi wa kiasi kikubwa kabisa inayoruhusu dhana inayowasilishwa kujitenga mbali zaidi kutoka kwa dhana iliyosimbwa. Hii inahusu matumizi ya kupiga chuku au kutia chumvi lakini haimaanishi kuchukuliwa hivyo wazi.

*Mchoro 6: Chuku*



(Kutoka: Wilson D. 2006-07)

Mfano;


3. Maji haya *yanachemka*.

*Yanachemka* itakuwa ni chuku iwapo maji haya ni zaidi ya kuwa moto kuliko ilivyotarajiwa au yakiwa katika kiwango cha kuwa moto kisichoridhisha.

### **1.9.5.2.3 Kisio la maana**

Wilson (2003) Kisio la maana ni aina ya upanuzi wa maana ambapo neno lililo na fahiwa halisi kiasi linapanuliwa hadi kwa kivuli cha hali (Laserbonn 1999 anaiita ‘mwangaza wa kipragmatiki’) ambazo kwa kusema kweli hali hizi zinapatikana nje ya maana halisi mahususi ya kiisimu. Katika aina hii ya mchakato, dhana inayowasilishwa inajitenga zaidi kutoka kwa ile dhana iliyosimbwa.

*Mchoro 7: Kisio la Maana*



(Kutoka: Wilson D. 2006-2007)

Mfano;


- (4) Koti hili lili nigharimu dola 1,000. [‘karibu 1,000’]

(5) Mawe haya yanaunda *mviringo*, *duara*, *piramidi*. ['umbo linalokaribia mviringo']

#### 1.9.5.2.4 Upanuzi wa kategoria

Wilson (2003) anaeleza kuwa, hii ni aina ya upanuzi wa maana ambayo inajulikana kitabia kwa matumizi ya majina ya rajamu zinazotambulika zaidi kuashiria kategoria pana vikiwemo vitu kutoka kwenye rajamu zisizotambulika zaidi. Kwa mfano;

*Mchoro 8: Upanuzi wa Kategoria*



(6) Federer ni *Sampara mpya*

Sampara inaibusha kategoria ya wachezaji wa mchezo wa tenisi wa (wachezaji) aina fulani na walio na talanta katika mchezo huo.

#### 1.9.5.2.5 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu

Ubunaji wa maana ni mchakato wa kuzua maana mpya na maneno mapya kutoka kwa yale maneno ambayo tayari yapo katika lugha fulani. Ubunaji wa maana mpya hivyo basi unaweza kutokea kupidia mkondo wa uundaji wa kileksimu. Hivi ni kumaanisha kwamba, tunapounda leksimu mpya, leksimu hiyo huweza kupata maana au fahiwa mpya.

Katika Kiswahili tunaweza kutoa mfano huu,

(7) Tom asilet *ubeberu* wake hapa.

Neno *ubeberu* liliwahi kuundwa kutokana na neno *beberu* lenye maana wazi ya mbuzi dume. Maana inayowasilishwa ni kwamba, Tom asiwanyanyase wengine.

### 1.10 Mbinu za Utafiti

Jinsi tulivyotangulia kutaja, utafiti huu ulifanyika katika kaunti ya Vihiga, Magharibi mwa Kenya katika soko la Mbale. Tulikusanya matamko ya Kiswahili yaliyokuwa na maneno yaliyofanyiwa usawazishaji wa maana. Tutaeleza mbinu na hatua za utafiti ambazo tulizitumia;

### **1.10.1 Kushiriki Shughuli**

Tulishiriki katika shughuli za kila siku za wakaazi hawa haswa shughuli za sokoni na zile zinazoendelea kwenye maduka yanayolizunguka soko hilo. Matamko yetu yalitoka kwenye mazungumzo ya kawaida pamoja na yale yeny muktadha wa sokoni. Mazungumzo ya kawaida ni muhimu kwa kuwa huweza kutokea katika miktadha mbalimbali na huwa na sifa ya kubadilisha mada, jambo ambalo lilituwezesha kupata data ya kiasi cha haja. Tuliandika matamko ambayo yalikuwa na matumizi ya maneno yaliyosawazishwa maana. Tulitumia mbinu hii ili kuweza kupata ule muktadha ambamo neno fulani lilitumiwa kwa sababu nadharia yetu inaeleza kwamba muktadha ni muhimu katika kuchanganua maana za maneno.

### **1.10.2 Mahojiano na Mijadala**

Ili kukusanya data hasa kuhusu sababu za mabadiliko ya maana, tulitumia mbinu ya mahojiano kupitia mijadala kisha mahojiano ya moja kwa moja. Tulichagua sampuli kutoka vituo tofauti vy a soko ambayo ilikuwa na jumla ya washiriki thelathini. Washiriki katika utafiti huu walikuwa ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Washiriki waliulizwa wakadirie kiwango chao cha umilisi wa lugha ya Kiswahili. Wale waliokuwa na umilisi wa Kiswahili wa kiasi cha haja ndio waliohusishwa katika utafiti huu. Tuliwapa washiriki mifano ya maneno na matamko tuliyokusanya katika utafiti wa kwanza. Tuliwaaliza watupe maana za maneno hayo na sababu za mabadiliko ya maana kwa kila neno kisha tukarekodi miitikio yao kwa kutumia kinasa sauti.

### **1.10.3 Uchanganuzi wa Data**

Data yetu ilichanganuliwa kimaelezo wala si kitakwimu. Hii ni kwa sababu tulikuwa tunashughulikia maneno na maana zake. Kwanza, tulihamisha yale mahojiano kutoka kwenye kinasa sauti na kuyaundia kanda. Kisha tuliiweka tepu hiyo kwenye kaseti na tukasikiza miitikio ya wahojiwa mmoja baada ya mwingine huku tukiandika chini miitikio ambayo ilikuwa faafu zaidi kwa kazi hii. Katika kuchanganua data yetu, tulichagua maneno kutoka kwenye matamko tuliyokuwa tumekusanya katika utafiti wa kwanza. Kisha tulichunguza aina ya badiliko lililotokea katika neno hilo na athari iliyoweza kutokea katika badiliko hilo la maana. Umilisi wa mtatifi wa lugha ya Kiswahili ulimsaidia mtatifi katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Hii ni kwa sababu mtatifi ni msemaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha yake ya pili.

## **SURA YA PILI**

### **USAWAZISHAJI WA LEKSIMU**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumejadili aina za mabadiliko ya maana katika Kiswahili. Aina za mabadiliko ya maana zinaainishwa na wataalamu mbalimbali kwa namna mbalimbali. Baadhi ya wataalamu waliowahi kuainisha aina za mabadiliko ya maana ni pamoja na, Bloomfield (1933), Ullmann (1970, 1972) ambao wanaainisha aina mbili kuu za mabadiliko ya maana ambazo ni kutanuka kwa maana na kubanika kwa maana. Mtaalamu mwagine anayeainisha aina za mabadiliko ya maana ni Palmer (1981). Wengine ni Blutner (1998), Carston (2002), Wilson (2003), Wilson (2006-07) na Wilson (2007-08) ambao katika kuelezea Nadharia ya Pragmatiki Leksika, wanaelezea aina mbalimbali za usawazishaji wa maana. Katika kazi hii, tumeainisha mabadiliko ya maana kwa mujibu wa Nadharia ya Pragmatiki Leksika.

Katika kuelezea aina za usawazishaji wa maana, tumetoa maelezo yetu kutoka kwa wataalamu tofautitofauti. Tumejadili mabadiliko ya maana za maneno kwa kuzingatia muktadha. Tumeelezea mabadiliko haya kwa kuchunguza maana wazi ya neno na kuilinganisha na maana mpya ambayo neno hilo linapata kulingana na muktadha wa matumizi.

#### **2.2 Dhana ya Muktadha**

Jeffers na Lehiste (1979) wanaeleza kwamba, kutokana na mtazamo wa wanamiundo, maana ya neno inatambuliwa kutokana na seti ya miktadha ambayo kwayo kwa kijumla neno hilo hutokea. Badiliko la kileksika linaweza kutazamwa kama badiliko katika seti ya miktadha ambamo kwamo neno fulani huweza kutokea. Ingawa maelezo haya hayatoi ufanuzi wa dhana ya muktadha, yanatusaidia kuelewa kwamba mabadiliko ya maana za maneno hutegemea muktadha wa matumizi wa maneno hayo. Maelezo haya ni msingi bora katika kuelezea dhana ya muktadha hata ingawa yanaegemea upande wa nadharia.

Schiffrin (1994) anaeleza muktadha kama ulimwengu uliojaa watu wanaotoa matamko, watu ambao wana utambulisho, maarifa, itikadi, malengo na mahitaji ya kijamii, kitamaduni, kisiasa, na ya kibinafsi na ambao hutangamana katika hali tofautitofauti zinazotambulika za kijamii na za

kitamaduni. Ni kutokana na ulimwengu huu unaotajwa katika maelezo haya ndipo tunapata vitu mbalimbali vya kutuwezesha kuunda muktadha ambao unatusaidia katika kuelewa matamko.

Wilson (2007-08) anaelezea muktadha katika kuelewa tamko kuwa ni seti ya chukulizi zinazowakilishwa kiakili ambazo kwa hakika hutumiwa katika ufasiri wa tamko fulani. Chukulizi hizo zinaweza kuchotwa kutoka kwenye ufasiri wa matini inayotangulia, au kutoka kwa kumtazama msemaji na kile kinachoendelea katika mazingira yaliyo karibu, lakini pia chukulizi hizi zinaweza kuchotwa kutoka kwenye maarifa ya kitamaduni, maarifa ya kisayansi, chukulizi zinazotokana na fahiwa za kawaida, na, kwa ujumla zaidi, kutoka kwenye kitengo chochote kinachohusu ujumbe unaojulikana na wote –msemaji na msikilizaji au wa kiupekee ambao kwao msikilizaji anafikiria wakati huo wa tamko. Anatamatisha kwa kusema kwamba, hivyo basi, muktadha unachotwa kutoka kwenye vigezo muhimu vya ulimwengu wa kifisiolojia pamoja na diskosi inayotangulia, lakini pia na mengine zaidi.

Schroder (2012) akiwanukuu Sperber na Wilson (1995) anaeleza kwamba, “muktadha ni muundo wa kisaikolojia, ni sehemu ndogo ya chukulizi za msikilizaji kuhusu ulimwengu.” Muktadha hivyo basi ni aina ya maarifa ya ufahamu kuhusu ulimwengu ambao unabeba itikadi na kaida za jamii, mifumo ya itikadi ya mtu binafsi na kaida za kitamaduni; kwa ufupi, muktadha ni maarifa yote ambayo wawasilianaji watakuwa wamehifadhi katika mawazo yao wakati ule wanapoingia kwenye mazungumzo.

Kwa mujibu wa maoni ya Schiffriin (keshatajwa) inaonekana kwamba, muktadha unahu masuala yaliyoko nje ya lugha. Maoni ya Wilson (2007-08) na yale ya Schroder (keshatajwa) yanaonekana kuwa na uhusiano wa karibu zaidi kwa kuwa yanahuisha muktadha na mambo yaliyoko kwenye lugha pamoja na yale yaliyoko nje ya lugha. Kutokana na maoni ya wataalamu hawa tunaeleza kuwa muktadha unaweza kuwa wa kiisimu au wa kijamii. Kwa sababu hiyo, tunaelezea kwamba, muktadha unaweza kujumuisha mambo mengi kama vile watu walioko kwenye diskosi, mazingira, utamaduni, elimuawali, lugha, wakati na saikolojia. Mambo haya yanaweza kutokea kwenye diskosi moja ama yakiwa yote pamoja au yakiwa machache.

### **2.3 Semantiki na Pragmatiki**

Habwe (1999) anataja kwamba, nadharia tofautitofauti pamoja na wataalamu wamejaribu kuelezea maana ya pragmatiki. Nadharia hizi zimejaribu kuonesha pale ambapo mpaka unapatikana kati ya

semantiki na pragmatiki kwa njia mwafaka. Hata hivyo, hatutajingiza katika mijadala inayohusiana na dhana hizi. Tutajikita kwenye fasiri za baadhi ya wataalamu kuhusu dhana hizi mbili kwa manufaa ya utafiti huu.

Leech (1983) anataja kuwa, semantiki inaashiria kile ambacho x inamaanisha na pragmatiki ni kile ambacho msemaji anamaanisha kwa kutumia x. Mfano;

(8) Kipa wa Mkingi ni *mburukenge* sana. Hawezi shika bao rahisi.

Tukizingatia maelezo ya Leech hapo juu, kianalojia, tutachanganua tamko hili ifuatavyo, ikiwa;

X=Mburukenge,

Mburukenge= aina ya mnyama

Inafuatia kwamba x ni aina ya mnyama (maana ya x)

Matumizi ya x katika tamko la hapo juu, ikiwa;

X=mburukenge

Mburukenge=mnyama mjinga

Inafuatia kwamba; ikiwa Kipa wa Mkingi ni mburukenge na mburukenge ni mnyama mjinga, basi pia Kipa wa Mkingi ni mtu mjinga (maana inayotokana na matumizi ya x)

Kwa kifupi anachomaanisha Leech ni kwamba, semantiki ni maana ya kiisimu huku pragmatiki ikiwa ni maana kimatumizi. Kufuatana na mtazamo huu wa kuelezea pragmatiki basi ni dhahiri kwamba maneno yanapotumiwa au yanavyotumiwa hayatumiwi kwa maana wazi hivyo, jambo ambalo linaweza kusababisha kupotea kwa mawasiliano. Kutokana na maana fiche ya neno *mburukenge* katika tamko hili, inaonekana kwamba neno hili limetumiwa kwa kuhamisha maana. Maana ya msemaji inajitokeza kama kisehemu cha maana pana ya neno *mburukenge* ambacho ni *mtu mjinga*. Kisehemu hiki ndiyo maana inayohamishwa kutoka kwa hali ya kuashiria mnyama hadi kwa hali ya kuashiria binadamu.

Habwe (1999) anakubaliana na maoni ya Searle (1975) anaposema kwamba, hali rahisi za maana ni zile ambazo kwazo msemaji anatamka sentensi na kumaanisha kwa uhakika na kwa uwazi kile

anachokisema...lakini ubaya ni kwamba, si kila hali zote za maana ni wazi hivyo: katika midokezo, kupiga vijembe, kinaya na sitiari –kutaja tu ila kwa mifano michache –maana ya tamko la msemaji inachukua sehemu yake kwa namna tofautitofauti. Habwe (keshatajwa) anaongeza kwamba, sehemu moja muhimu ya hali hii ni ile ambayo kwayo msemaji anatamka sentensi akimaanisha anachokisema, lakini tena anamaanisha jambo zaidi. Tunadai kwamba, hizi hali za maana zisizo wazi ndizo ambazo zinasababisha maana za maneno kukosa kuwa wazi kama vile kinaya na sitiari. Hali hizi zinajitokeza zaidi kwenye leksimu zinazotumiwa katika matamko, hivyo basi matumizi haya ndiyo yanayomfanya msemaji kutomaanisha anachokisema. Kwa kifupi, hali hizi ndizo zinazosababisha msemaji kutumia maneno ama kwa kupanua au kwa kubana maana zake.

Kwa ujumla, tukitathmini maoni ya wataalamu hawa ni kuwa kile ambacho msemaji anamaanisha anachokisema ndiyo semantiki –na ndiyo maana ya x ya Leech (1983) huku lile jambo zaidi analomaanisha msemaji ndiyo pragmatiki –na ndiyo maana ya matumizi ya x ya msemaji. Tunaeleza kwamba, dhana iliyosimbwa na neno katika tamko ndiyo maana ya x na ndiyo semantiki, nayo dhana inayowasilishwa na msemaji kwenye tamko kwa kutumia neno ndiyo matumizi ya x na ndiyo pragmatiki. Kwa usanjari huo, kwa kuchunguza maoni ya Searle (keshatajwa) inafuatia kwamba, maana iliyosimbwa na neno kwenye tamko ndiyo maana ambayo msemaji anamaanisha anachokisema kwa kutumia neno ilhali maana inayowasilishwa na msemaji kwenye tamko kwa kutumia neno ndilo jambo zaidi analomaanisha msemaji na ndiyo implikecha. Fauka ya hayo, tunakubaliana na maoni ya Leech (1983) anaposema kwamba, hapawezi kutokea mpaka wazi kati ya misamiati hii miwili. Ni salama kuiona kama mwelekeo mtupu ukielekezwa upande mmoja badala ya kuelekezwa kwenye mojawapo ya misamiati hiyo.

Mwisho, Schiffriin 1994) anaeleza kwamba, msemaji anaweza kutumia kitaja kwa njia ambayo imefungwa tu katika muktadha fulani na hivyo basi kuhitaji uelewa wa kipragmatiki. Maoni haya yanaendana na maoni ya Wilson (2003) anayeeegemea upande wa leksimu kwa kutumia Nadharia ya Prgamatiki Leksika anaposema kuwa, lengo la semantiki kileksika ni kuchunguza ule uhusiano kati ya maneno na dhana zilizosimbwa katika maneno hayo na lengo la pragmatiki kileksika ni kuelezea ukweli kwamba, dhana inayowasilishwa katika matumizi ya neno aghalabu hutofautiana na dhana iliyosimbwa kwenye neno hilo. Kutokana na maelezo haya tunaeleza kwamba, kwa sababu maana ya maneno hutokea katika muktadha wa matumizi, pana haja na mazoea ya msemaji

kufanya usawazishaji wa leksimu na kwa mkondo huo, kuna kusababisha mabadiliko ya kileksika ambayo yanaweza kuzua kupotea au kutatizika kwa mawasiliano. Ikumbukwe kwamba muktadha hasa ule wa kisaikolojia unaweza kutofautiana mionganoni mwa wasemaji wa jumuia lugha katika kufasiri tamko.

## 2.4 AINA ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU

### 2.4.1 Ubanaji wa Kileksika

Kolaiti na Wilson (2012) wanaeleza ubanaji wa kileksika kama mchakato unaohusu matumizi ya neno au kirai kuonesha dhana mahususi zaidi (iliyo na maana finyu/iliyobanwa) kuliko maana iliyosimbwa ya kiisimu (maana wazi).

Tunakubaliana na maoni haya kwa kuongezea kuwa, ile maana pana ya neno ndiyo maana iliyosimbwa kiisimu na ubanaji unapofanywa huwa tunapata dhana ndogo ambayo ni dhana inayowasilishwa kwenye tamko. Dhana hii inayowasilishwa huwa ni kisehemu cha maana pana iliyosimbwa na neno.

Tuchunguze mfano huu;

(9) a Mtu A: Najua Dady anaongea tu na hajakata kura.

b. Mtu B: (Dady) Bwana wacha zako, kura niko nayo na niko *ndani, ndani*  
kabisa.


c. Mtu A: Sema NASA imekunasa 'paka umeingizwa *ndani*.

Neno *ndani* katika lugha ya Kiswahili limesimba dhana NDANI. Dhana iliyosimbwa kwenye neno ndani ni wazi na ya kijumla kwa kuwa inajumuisha maana nyingine ambapo ndani inaweza kuwa ndani mahali popote. Katika diskosi hii, ili kufikia dhana mahususi ya *ndani*, inamhitaji msikilizaji kufanya ufasiri kutegemea muktadha. Hii ni kwa sababu, msemajji B anaposema kuwa *yuko ndani*, dhana inayojitokeza inakuwa pana kwa kiasi fulani. Horn na Ward (2004) wanaeleza kwamba, ubanaji kwa kiasi kikubwa ni mchakato unaoweza kusawazishwa na unategemea muktadha. Hii ni kwa sababu, maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika viwango tofautitofauti na katika mielekeo tofautitofauti kutegemea wakati mahususi wa matumizi. Ni kutokana na wakati huu mahususi wa kisiasa ndipo msikilizaji anafasiri dhana ya neno *ndani* kuelekea upande fulani wa

wakati wa kisiasa wala si ndani mahali popote. Muktadha wa matumizi ya neno *ndani* unatokana na mwanasiisa fulani nchini Kenya akilitumia neno hili kwa fahiwa ya *kuwa mfuasi sugu wa chama fulani cha kisiasa na ni vigumu mtu mwingine kumwondoa chamani*. Huu ni wakati wa siasa za uchaguzi mkuu 2017 nchini Kenya. Analitumia hili neno kwa kulikaririkariri ili kusisitiza kwamba, kamwe habanduki wala kubanduliwa kutoka chama chake. Hii ndiyo sababu msemaji B kwenye mfano wa (9) analikariri neno hili ili dhana inayowasilishwa ieleteke kwa urahisi na msikilizaji. Tunachukulia kwamba, msikilizaji anayo maarifa ya ufahamu kuhusiana na siasa za uchaguzi mkuu wa mwaka 2017 nchini Kenya.

Matokeo ya ubanaji ni kuonesha kijisehemu mahususi cha maana mahususi ya kiisimu. Dhana ya kileksika ya neno hili ni sehemu ya kitu ambayo haiko upande wa nje Mdee n.w. (2011). Maana hii ni pana kwani inaashiria sehemu yoyote. Dhana hii inabanwa kulingana na muktadha wa diskosi hii. Matokeo ya ubanaji huu ni fahiwa mahususi ambayo ni *kuwa mfuasi sugu wa chama fulani wala hakuna mtu anayeweza kukuondoa chamani kwa urahisi*. Kuwa ndani ya chama ndiyo fahiwa mahususi na ndiyo dhana inayowasilishwa na msemaji huku dhana iliyosimbwa na neno ikiwa ni maana wazi na pana ya neno *ndani*.

#### *Ubanaji wa Kileksika*



Mchoro huu unaonesha kwamba, *dhana iliyosimbwa* kwenye neno ni pana. Inamhitaji msikilizaji kufanya mchakato wa ubanaji wa hii dhana pana kutegemea muktadha ili afikie *dhana inayowasilishwa*. Dhana inayowasilishwa na neno kwenye tamko ni finyu na ni kisehemu cha ile dhana pana iliyosimbwa kwenye neno hilo.

Mfano;

(10) a. Mtu A: Nilisikia ati dawa ya *kirusi* ilipatikana.

---

<sup>2</sup> \*Mchoro huu pamoja na maelezo yake unaweza kutumiwa katika kuelewa mifano ya maneno mengine ambayo yamepitia ubanaji wa kileksika katika kazi hii.

b. Mtu B: Wapi? Jibebebebe ukisema ati kuna dawa... hiyo ni ya watu hawana virusi...

Neno *kirusi* limesimba dhana KIRUSI ambayo inajumuisha aina nyingi za virusi vinavyosababisha magonjwa tofautitofauti. Katika diskosi hii, msikilizaji anaposikia neno *kirusi*, tunachukulia kuwa tayari anayo maarifa mapana kuhusiana na virusi. Hivyo basi, inambidi msikilizaji kufanya kutafuta njia rahisi ya kumwezesha kuelewa dhana inayowasilishwa na neno *kirusi* katika tamko. Kupitia maarifa yake ya ufahamu kuhusiana na neno *kirusi*, anafanya ubanaji ili aweze kufikia maana inayowasilishwa. Kwa mfano msikilizaji anaweza kuwa na maarifa kwamba, upo ugonjwa hatari, ugonjwa huu ni UKIMWI, ugonjwa wenyewe hauna dawa, watu hawataji jina la ugonjwa huu hadharani, awali kulikuwepo na tangazo kuhusu dawa ya UKIMWI na virusi ndivyo hubeba ugonjwa huu. Blutner (1998) anaeleza kuwa ubanaji una maana ya kutumia faridi leksika kupitisha ufasiri uliobanwa zaidi kuliko ule uliosimbwa kisemantiki. Maana ya kisemantiki ya neno *kirusi* ni; kiini kinachosababisha ugonjwa Mdee n.w. (2011). Tunachukulia kwamba, maana hii ndiyo ufasiri uliosimbwa kisemantiki. Maana hii ni pana, inajumuisha aina nyingi za virusi. Kupitia muktadha, basi msikilizaji anabana maana hii ya kisemantiki na kufikia kipashio kidogo cha kileksika ambacho ni *kirusi cha ugonjwa wa UKIMWI* akivitenga au kuvifungia nje aina ya virusi vingine vyote. Msikilizaji anafikia dhana kwamba, kinachorejelewa na neno *kirusi* ni *ugonjwa wa UKIMWI* na *Msemaji ana haja ya kujua ikiwa dawa ya ugonjwa huu imepatikana*.

Mfano;

(11) a. Mtu A: Tena nilisikia Mafunya alikufa na *ugonjwa* \*<sup>3</sup>

b. Mtu B: Eee huyo alikuwa kwa ARVs

Leksimu *ugonjwa* ni haiponimia. Matumizi ya neno ugonjwa katika mfano wa (11) yanamhitaji msikilizaji afanye ubanaji wa maana pana ya neno *ugonjwa* ili afikie dhana inayowasilishwa. Msikilizaji B anaposikia tamko la Mtu A, tunachukulia kwamba, anafanya mchakato wa haraka ili kufikia dhana inayowasilishwa. Msikizaji anaweza kuunda dhana za dharura kuhusu aina mbalimbali za magonjwa anayoyafahamu. Anafanya hivi kwa kuvuta maarifa yake ya ufahamu kuhusu magonjwa haya. Kutokana na muktadha wa matumizi ya neno *ugonjwa* katika diskosi hii,

<sup>3</sup> \*Watu walioko kwenye diskosi nambari 11 ni walewale walioko kwenye diskosi ya nambari ya 10.

msikilizaji anafikia dhana kuwa ugonjwa unaorejelewa ni UKIMWI. Hali ya Mtu B kutaja ARVs ambayo ni dawa ya ugonjwa wa UKIMWI ndiyo inayodhihirisha wazi kwamba Mtu B ameellewa dhana inayowasilishwa na Msemaji A. Hivyo basi wote wanazungumzia kitu kimoja. Msikilizaji anafungia nje aina nyingine zote za magonjwa na kuchagua aina moja ya ugonjwa ambayo ni UKIMWI na ambayo ndiyo dhana inayowasilishwa na msemaji kwa kutumia neno *ugonjwa*.

#### **2.4.2 Upanuzi wa Kileksika**

Fromkin na Rodman (1978) wanaeleza kwamba, wakati maana ya neno inapokuwa pana, neno hilo humaanisha kila kitu kilichokuwa likimaanisha kisha na vitu vingine zaidi. Tunapanua maelezo haya kwa kuongezea kwamba, maana ya neno inapokuwa pana, neno hilo huweza kuwa limeongezewa vitajwa na kujumuisha vitajwa vingine katika maelezo ya maana yake.

Mfano;

- (12) a. Mtu A: Siku hizi sikunywi *chai* ya majani.  
b. Mtu B: Unakunywa gani? ..... Siku hizi uko juu.  
c. Mtu C: (akimwashiria Mtu B) *Chai* ya wanaume unaweka kahawa ama chokoleti. Kwani hujui maana ya kahawa wewe...


Katika diskosi hii, tulitarajia Mtu A aseme tu *hanywi chai* bila kuongezea ...ya *majani*. Ila anasisitiza kuwa *hanywi chai ya majani*. Chai huandaliwa kwa majani ya mchai na huweza kutiwa maziwa au ikose. Kutokana na tamko la Mtu A, ni dhahiri kwamba iwapo hanywi chai ya majani waziwazi hivyo, kianalojia inafuatia kwamba, ipo *aina fulani ya chai* anayoinyuwa au kinywaji cha aina fulani kisichopikwa kwa majani ya mchai. Mbali na neno *chai* kuashiria aina ya kinywaji kinachochemshwa kwa majani ya mchai, pia inaashiria aina nyingine ya vinywaji kama vile kahawa na chokoleti kwa mujibu wa diskosi hii. Jambo hili linadhihirika waziwazi katika mfano wa kauli ya Mtu C katika diskosi hii. Mbali na maana ya chai kuwa na kitajwa kimoja, msemaji huyu anaongezea vitajwa vingine kwenye maana hii na matokeo ni kupanuka kwa maana ya neno *chai*.

Katika muktadha wa Kenya, watu wengi hunywa chai, chokoleti au kahawa kama kiamshakinywa. Katika maeneo yetu ya utafiti, chai ndiyo inayonyewa kwa wingi na watu wengi kama

kiamshakinywa, hasa chai ya maziwa. Viungo vingine vinavyoweza kutumiwa katika kuandaa aina ya kinywaji kama vile kinywaji cha chai havitumiwi sana.

Kutokana na mazoea ya kutumia majani ya mchai kuandaa kiamshakinywa kuliko matumizi ya viungo vingine kama vile kahawa na chokoleti, neno *chai* linatumwa kujumuisha aina nyingine za vinywaji viliviyotajwa. Almradi kinywaji hicho hunywewa alfajiri kama vile chai inavyonywewa, basi kina *kibali* cha kuitwa *chai*. Neno *chai* linapata vitajwa zaidi na maana yake inapanuka. Hivyo basi, matumizi ya neno *chai* katika tamko la Mtu A na Mtu C ni pana kwa kuwa wanajumuisha viashiriwa vingine ndani ya dhana CHAI iliyosimbwa na neno *chai*. Hali hii inaweza kusababisha kudhoofika kwa mawasiliano hasa katika eneo ambalo watu wamezoea kutofautisha chai, kahawa na chokoleti.

#### *Upanuzi wa Kileksika*



Mchoro huu unaonesha kwamba, *dhana iliyosimbwa* kwenye neno ni finyu na dhabiti kwa kiasi fulani. Dhana hii inafanyiwa mageuzi kulingana na muktadha na matokeo yake ni kupata *dhana inayowasilishwa* ambayo ni pana kuliko dhana iliyosimbwa na neno hilo.

Mfano;

(13) a. Mtu A: Siku ile tulienda kwa matanga ya Samweri *walitujenga* vizuri...

b. Mtu B: Hao watu *walitutengeneza*. Nilikula nikajua hivi ndio watu wanaishi.

Leksimu *tengeneza* imesimba dhana TENGENEZA. Maana wazi ya neno *tengeneza* ni kuunda kitu kilichoharibika ili kifae tena. Katika diskosi hii, msemaji B hatoi tamko lake waziwazi hivyo. Inamhitaji msikilizaji aunde dhana za dharura kuhusu vitu vinavyoweza kutengenezwa. Anafanya hivi kwa kusawazisha mkondo wa ujumbe, muktadha na athari za kimawazo. Maana ya kwanza ya neno *tengeneza* inayomfikia msikilizaji huenda ni ile dhana ya kimantiki ya kuunda kitu kilichokuwa kimeharibika. Anafanya mchakato wa haraka na kugundua kwamba, siyo hiyo dhana

<sup>4</sup> \*Mchoro huu pamoja na maelezo yake unaweza kusaidia katika kuelewa baadhi ya aina nyingine za upanuzi wa kileksika katika kazi hii.

wazi inayowasilishwa na msemaji na anaidondosha hii dhana wazi na kuunda dhana za dharura. Dhana hizi za dharura zinaweza kuhusiana na vitu vinavyoweza kutengenezwa kama vile baiskeli na redio kulingana na mazingira ya msikilizaji na maarifa yake ya ufahamu. Aidha, kwa kuwa msikilzaji (Mtu A) ndiye anayetanguliza mazungumzo haya, kuna uwezekano kwamba anayo elimuawali kuhusu mada inayozungumziwa katika diskosi hii. Hali hii itamfikisha msikilizaji kwenye dhana ya dharura TENGENEZA<sup>5</sup> ambayo inajumuisha ujumbe wa *kulishwa au kupewa msaada wa chakula*. Aidha, dhana inayowasilishwa inaweza kuwa ni *kulishwa kwa vinono ambavyo kawaida mtu fulani huenda hajawahi kuvila au amechukua muda mrefu kabla ya kuvila* au dhana kuwa *alilishwa kiasi cha kwamba alishiba zaidi tukilinganisha na jinsi alivyowahi kushiba kabla*. Neno *tengeneza* hivyo basi limepata maana zaidi na miktadha zaidi mbali na maana zake za kawaida.

Hebu tuchunguze matamko tofauti ya matumizi ya leksimu *tengeneza*:

- (14) a Mtu G: Huyo mtu *atatengenezwa* vizuri nakwambia.  
b. Mtu F: Itakuwa kama yule jamaa wa pikipiki... aliundwa! damu ikatoka kwa  
kichwa...

Hapa, neno *tengeneza* lina maana nyingine fiche iliyo tofauti na ile ya kwanza. Hapa, *kutengeneza* kuna maana fiche ya *kumpiga mtu hadi yule anayetekeleza kitendo cha kupiga aridhike kwamba amemuumiza anayepigwa*. Maana hii ni kinyume na maana halisi ya kuunda kitu kilichoharibika ili kifae tena. Mchakato unaotokea katika akili ya msikilizaji unamwezesha kutofautisha fahiwa zote mpya za neno *tengeneza* kutokana na muktadha wa matumizi. Msikilizaji wa tamko hili anavyofanya mchakato wake hadi kufikia maana inayowasilishwa ni tofauti na msikilizaji katika mfano wa (13) kwa kuwa miktadha ya matumizi ya neno *tengeneza* ni tofauti. Maana ya neno huwa pana tunapoongeza miktadha ambamo neno hilo linatokea. Neno *tengeneza* limepata miktadha zaidi ya matumizi na ambayo inalifanya neno hili kupata fahiwa zaidi.

Tutazame mfano wa diskosi hii;

- (15) a. Mtu A: Naambia Dady...

---

<sup>5</sup> \* Hii alama inaashiria dhana ya pili ya dharura ambayo msikilizaji anaunda katika hali ya kufasiri ujumbe ulioko kwenye tamko.

- b. Dady: ...cuzo<sup>6</sup> siku hizi wamekuwa wengi, najua tu huyo ni *mguu*.
- c. Mtu A: .....
- d. Mtu C : Na ni kerenge cha wenya<sup>7</sup> (na ni *mguu* unataka). Ni *mguu* unataka?

Katika diskosi hii, Mtu A anajaribu kujitetea kwamba mwanamke aliyeonekana naye alikuwa ni bintiamu yake. Kabla ya Mtu A kukamilisha kauli yake, anakatizwa usemi na Dady ambaye anamkejeli Mtu A kwa kumwambia kwamba, *siku hizi* amekuwa (Mtu A) na ‘cuzo’ (bintiamu) wengi na kwamba anajua kuwa huyo hakuwa bintiamu bali alikuwa *mguu* (*mwanamke wa kutumiwa kimapenzi*). Mtu C naye anamalizia kwa kutoa kejeli yake kwamba, Mtu A anataka *mguu* kutoka kwa mwanamke anayerejelewa katika diskosi.

*Mguu* imesimba dhana MGUU. Maana wazi ya neno *mguu* ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda TUKI (2013). Dady analitumia neno *mguu* kwa maana ya *mwanamke anayetumiwa kimapenzi kisha kuachwa*. Naye Mtu C analitumia neno *mguu* kwa maana ya *sehemu ya siri ya mwanamke*. Neno *mguu* hivyo basi limepata fahiwa mbili zaidi mbali na maana yake ya kisemantiki. Ullmann (1970) anaeleza kwamba, maneno yanaweza kupewa fahiwa moja bunifu au zaidi bila kupoteza maana yake asilia: maana asilia na maana mpya zitaishi upande kwa upande bora tu kusiwepo na uwezekano wa kukanganya kati yazo. Wasemaji katika diskosi hii wanafikia uhusiano kwa kuwa wanaweza kuitumia maana ya kimsingi ya neno *mguu* na fahiwa mpya za neno hili bila kukanganyikiwa. Hata hivyo, matumizi na uelewa wa maana wazi ya neno *mguu* pamoja na fahiwa zake mpya vinategemea muktadha.

Hock na Joseph (1996) wanataja kwamba, ukopaji mara nyingi huendana na mabadiliko ya kisemantiki. Ukopaji pia umechangia katika mabadiliko ya maana katika Kiswahili kama ilivyo katika mfano ufuatao;

(16) Hii nayo unaiza *senti* ngapi?

Leksimu *senti* katika Kiswahili ni tafsiri ya neno *cent* la Kiingereza. Katika Kiingereza, neno hili lina maana ya kisemantiki ya kiwango cha pesa chini ya shilingi moja. Neno hili lilipokopwa na kuswahilishwa hadi Kiswahili, lilipewa maana zaidi. Neno *senti* katika tamko la hapo juu lina

<sup>6</sup> Cuzo –hili ni neno la sheng linalotokana na ufupishaji wa neno la Kiingereza *cousin*.

<sup>7</sup> Tamko hili ni la lahaja ya Lulogooli ambayo ni mojawapo ya lahaja za Luluhyia. Tumetoa tafsiri yake mabanoni.

maana ya pesa zinazozidi kiwango cha shilingi moja. Muktadha wa kuwa sarafu ya senti haitumiwi tena nchini Kenya na mwaka wa kutolewa<sup>8</sup> tamko hili ni muhimu katika kumsaidia msikilizaji kupata ujumbe unaowasilishwa kuwa, *msemaji ana haja ya kujua bei ya bidhaa fulani*.

#### 2.4.3 Upanuzi wa Kisitiari

Cuddon (1979) na Simiyu (2016) wanashabihiana kimawazo wanapoeleza kwamba upanuzi wa kisitiari ni aina ya upanuzi ambapo maana ya tamko iko mbali na maana wazi. Hivi ni kusema kuwa, maana ya tamko katika matumizi ya neno inatofautiana sana na maana ya kiisimu iliyosimbwa au maana halisi inayopewa neno hilo na sarufi ya lugha. Tunaongezea kwamba, maana ya tamko katika sitiari huwa mbali na maana halisi kwa kuwa kuna kuhamisha maana nzima au sehemu ya maana kutoka kwa kiashiriwa kimoja hadi kingine. Aidha, katika nadharia ya uhusiano, matumizi ya sitiari yanachukuliwa kuwa ni uvunjaji wa kanuni ya ukweli.

Mfano;

(17) Mama Junior ni *sufuria* sana. Nilimkataza aachane na hiyo *loan* hasikii.

Dhana iliyosimbwa na neno *sufuria* ni SUFURIA. Msikilizaji anaposikia tamko hili huweza kuunda dhana za dharura kama vile sufuria ni chombo ambacho hakina uhai, sufuria ni chombo cha jikoni, kinatumiwa kupikia chakula, huwekwa kwenye moto, huwa na mlale katika sehemu yake ya nyuma. Dhana hizi ni wazi hivi kwamba, haziwezi kuwa ndizo zinazowasilishwa kwenye tamko hili. Ila kutokana na muktadha wa matumizi ya neno *sufuria*, msikilizaji anaweza kupata dhana inayowasilishwa. Mfano, sentensi ya pili katika tamko hili itamwongezea msikilizaji kufahamu kuwa anayerejelewa huenda ni mtu mjinga au asiyesikia maoni ya wengine. Dhana ya kuwa mjinga au kutosikia maoni ya wengine ndiyo dhana inayowasilishwa na msemaji huku dhana ya kuwa sufuria ni chombo cha kupikia ndiyo dhana wazi. Dhana inayowasilishwa inajitenga zaidi kutoka kwa dhana wazi ya neno. Bloomfield (1933) anaeleza kwamba, matumizi ya upanuzi wa kisitiari yana dhima ya kuficha ujumbe ule wa mawasiliano. Sitiari inajikita katika mfanano wa kiutambuzi kati ya vitajwa au matendo bainifu. Kwa kuwa sufuria ni chombo kisicho hisivu na huwa inawekwa mekonii kisha kushika mlale bila kulalamika, sifa hii ya sufuria inahawilishwa hadi kwa mrejelewa (Mama Junior). Uhawilishaji huu utamsaidia msikilizaji kuelewa ujumbe

---

<sup>8</sup> 2017, huu ndio mwaka wa kutolewa tamko hili, mojawapo ya kipindi cha wakati ambapo sarafu ya senti haitumiwi nchini Kenya.

uliofichwa kwenye tamko hili kuwa Mama Junior si sufuria wazi hivyo lakini dhana inayowasilishwa kwenye tamko hili ni kwamba *mrejelewa ni mtu asiyesikia maoni ya wengine na kwa sababu hiyo anachukuliwa kuwa mjinga*.

Mfano;

(18) Kipa wa Mkingi ni *mburukenge* sana. Hawezi shika bao rahisi.

Mburukenge ni aina ya mnyama huku kipa anayerejelewa ni binadamu. Aitchison (2003) anaelezea kwamba, utofauti wa vikoa vyta kisemantiki, unamwashiria msikilizaji kwamba ufananishaji wa kiutendaji unafaa kufanyika ili kufasiri sentensi husika. Tofauti ya kisemantiki ya mburukenge kuwa mnyama na kipa kuwa binadamu ndiyo inayomchochea msikilizaji kufanya mchakato wa kufasiri ujumbe ulioko kwenye tamko.

Mburukenge ana sifa zake ambazo msikilizaji huenda anazifahamu kupitia maarifa yake ya ufahamu. Kwa kusikia tamko hili, msikilizaji anajija na maana wazi ya neno *mburukenge* ambayo inaashiria mnyama. Kutokana na muktadha huu, mskilizaji anafanya mchakato wa haraka ambapo anadondosha hii maana wazi na kuanza kuunda dhana za dharura. Neno *mburukenge* limesimba dhana MBURUKENGE. Msikilizaji anaweza kuunda dhana za dharura kama vile, mburukenge ni mnyama, hana akili razini, ni aina ya mamba, anaishi nchi kavu, ni mnene, ni mrefu na anamshinda mjisui. Hata hivyo, maana hizi zinaonekana wazi kwa msikilizaji na huenda si maana ya msemaji. Hivyo basi, msikilizaji atafuata njia iliyio rahisi katika kufikia dhana inayowasilishwa. Anafanya hivi kwa kusawazisha ujumbe, muktadha na athari za kimawazo ili kufikia uhusiano. Kwa mfano, kutokana na tamko la ziada la msemaji kuwa, anayerejelewa *hawezi shika bao rahisi* linakuwa ni ufidiaji muhimu wa kumwezesha msikilizaji kuchagua njia rahisi ya kufikia uhusiano. Aitchison (2003) anaelezea kwamba, katika sitiari ya sampuli ya kiasili, hivyo basi, vitu vinavyofananishwa vina uwezekano wa kutofautiana, hivi kwamba, vinatokana na vikoa tofauti vyta kisemantiki, na kufanana, hivi kwamba vinashiriki sifa chache za kawaida. Maoni haya yanaelekea kushabihiana na yale ya Cruse (2000) anapojadili kwamba, athari nyingine ya maumbile ya kidhana ya sitiari ni kwamba, aina fulani za ruwaza za kuwazia zinaweza kuhawilishwa kutoka kwa wigo chanzi hadi kwenye wigo lengwa. Anaiita hii hali ‘ujumuishaji wa kisitiari’. Maoni ya hawa wawili yanaipa sitiari sifa ya kuhawilisha maana. Msikilizaji anahawilisha sifa moja au zaidi ya mnyama mburukenge (wigo chanzi) hadi kwa kile kiashiriwa (Kipa wa Mkingi) ambaye ni binadamu (wigo

lengwa). Hatimaye, anaunda dhana ya dharura MBURUKEGE\* ambayo inajumuisha sifa ya mtu mjinga ambayo inahusishwa na wanyama kwa kuwa wanyama hawana akili razini. Msikilizaji anafikia ufasiri kuwa kipa wa Mkingi ni mjinga kwa kuwa *mburukenge* huchukuliwa kuwa mnyama mjinga.

Kulingana na washiriki katika utafiti huu ni kwamba, sitiari kwenye mfano wa (18) imetokana na wahusika ambao ni askari katika tamthilia ya Kiswahili ya *Kifo Kisimani*. Mhusika mmoja anamtusi mwingine mburukenge kwa kuashiria kuwa yeye ni mjinga. Kwa sababu tamthilia hii iliwhali kutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya kama kitabu kiteule, sitiari hii ilishika katika matumizi yake kwa kutumiwa na wanafunzi wengi. Aidha, madai mengine ni kwamba, sitiari hii imetokana na viongozi wa kisiasa nchini Kenya wakati ambapo wao hutumia sitiari hii kukejeliana katika mikutano yao ya kisiasa. Chimbuko la sitiari hii ni muhimu kwani linatupatia mazingira sababishi ya kiasili kwa kiasi fulani ambayo yanatusaidia katika kufasiri dhana inayosimbwa na neno *mburukenge* katika tamko.

#### **2.4.4 Chuku**

Hili ni badiliko ambalo linaonekana kushirikisha kiwango kipana zaidi cha upanuzi na hivyo basi kunakuwa na utengano mkubwa kutoka kwa dhana iliyosimbwa (Wilson 2003). Tunaongezea kwamba, aina hii ya badiliko inahusu matumizi ya kupiga chuku au kutia chumvi lakini haimaanishi kuchukuliwa wazi hivyo. Kwa mfano;

- (19) a. Mtu B: *Nilioshwa*. Timu ya Asenali *iliniosha*. Hiyo siku ningekuwa na pesa.
- b. Mtu C: Utaendelea *kuoga* mtu wangu. Wachia sisi haya mambo.
- c. Mtu D: Eeih na wewe (*akimwashiria mtu C*) *umeiva* sana *betting*. Wikendi pia ulishinda...

Dhana iliyosimbwa na neno *iva* ni IVA. Maana wazi ya leksimu iva ni kufikia upeo wa kukomaa na kuwa tayari kuliwa au inaweza kuashiria hali ya kupikika vizuri kwa chakula hadi kufikia kiwango cha kuliwa. Dhana hizi zinaonekana kuwa wazi. Chakula kikiiva huwa tayari kuliwa. Mfano ni kuiva kwa ndizi au kuiva kwa viazi vilivyokuwa vikipikwa. Haiwezi kuwa wazi hivyo kuwa Mtu C amepikika mekonu akaiva bali kuna kutilia chumvi. Msemaji anapomrejelea mtu fulani kuwa *ameiva*, anajaribu kuhawilisha maana ile ya kuiva kwa chakula au ya kukomaa hadi

kwa mrejelewa ila si wazi hivyo. Tukichunguza muktadha wa tamko hili tunaweza kupata ufasiri wake. Tamko hili linatolewa wakati ambapo anayesemekana *kuiva* amekuwa akishinda katika mchezo wa kamari na kwamba yeYe amefikia kiwango cha kutoweza kushindwa katika mchezo huu. Inawezekana kwamba, wasikilizaji katika diskosi hii wameshuhudia chakula chochote kile kinavyopikwa hadi kikafikia kiwango cha kuliwa, jambo ambalo ni muhimu kwao katika kuelewa tamko hili. Inajitokeza kwamba, namna chakula kinavyopikwa kikafikia kiwango cha kuliwa ndivyo mtu aliye na ujuzi wa kufanya jambo fulani anasemekana *kuwa amefikia upeo wa kupigiwa mfano au kuaminika zaidi katika ujuzi wa jambo lile*. Bloomfield (1933) anataja chuku kama aina ya badiliko kutoka kwenye maana yenyе nguvu hadi kwenye maana legevu. Dhana ya kupika chakula kikafikia kiwango cha kuiva ni yenyе nguvu na ya mguso kuliko dhana ya kuwa mtu akiiva huwa *ameimarika katika jambo fulani* ambayo ni dhana ya kidhahania na legevu. Legevu hivi kwamba, iko mbali zaidi na maana halisi ya neno *iva*. Dhana iliyosimbwa kwenye neno *Iva – kitu kupikika* hivyo basi inajitenga sana na dhana inayowasilishwa katika tamko –ya mtu *kuwa na ujuzi wa kiwango cha juu wa kuaminika katika jambo fulani*. Chuku pia inajitokeza katika maneno *oshaa na oga* katika diskosi hii.

Mfano mwengine;

- (20) a. Mtu A: Nitaenda kwa MCA nimpige Kiswahili 'paka atoe sukari.  
b. Mtu B: Huyo anataka lugha. Bila lugha huyo mtu *hatoboki*. Ni mgumu aje!  
ukienda uniambie twende na wewe.  
c. Mtu C: *Mtanijenga* mkitoka huko.

Leksimu *toboka* katika Kiswahili ina maana wazi ya kitu kupata tundu la kuweza kupitisha vitu vigumu au vya majimaji au hewa TUKI (2013). Ni wazi kuwa kitu kinapotoboka huvuja bila ya kujizuia. Msemaji anaposema kuwa MCA *hatoboki* anatilia chumvi kwani si wazi hivyo mtu kupata tundu na kuanza kuvuja. Ingawa kwa kusema kuwa mrejelewa katika diskosi hii *hatoboki* ina maana wazi kuwa *havuji* kama vile ndoo inavyoweza kuvuja maji ikitoboka. Basi ikiwa mrejelewa *havuji* inaonekana kwamba *hajatoboka*. Huenda wasemaji wanaelewa muktadha kwamba, pesa huwekwa mfukoni na mara mfuko unapotoboka hupitisha pesa hizo zikaanguka na wengine wakaziokota kama vile maji yanavyovuja kutoka ndoo iliyotoboka. Hivyo basi, maana

inayowasilishwa ni kwamba, *MCA hasaidii mtu pesa zake kwa urahisi hivyo*. Hali ya kutotoboka kwa kitu inamithilishwa na hali ya kutovuja kwa kitu. Katika muktadha huu, kiuwazi tunachukulia kwamba, hali ya kutotoboka kwa mifuko inamithilishwa na hali ya kutovuja kwa mifuko –*mifuko ya MCA*. Kutotoa pesa kwa urahisi kunamithilishwa na kutotoboka. Msikilizaji anapata ufasiri kwamba *ni vigumu sana MCA kumsaidia mtu mwingine pesa zake*. Ufasiri huu unakuwa masafa ya mbali zaidi na maana ya kitu kuwa na tundu kisha kuvuja.

Mfano;

(21) Siku ile *ulinigonga*, leo unipimie vizuri...

Lesksimu *gonga* ina maana wazi ya kukutanisha kitu kimoja na kingine kwa kuvipiganisha TUKI (2013). Tunachukulia kwamba, msikilizaji anavyo vitomeo vya maarifa ya ufahamu kuhusu hali ya kitu kugongana na kingine. Kwa mfano, huenda msikilizaji anafahamu kwamba, vitu vinapogongana huweza kutokea athari hasi ya kitu kimoja kwa kingine. Aidha huenda msikilizaji anafahamu waziwazi kuwa mtu akigongwa kwa mfano, kwa kutumia nyundo huwa anaumia. Hali hii inahawilishwa kwa hali ya kumgonga mtu ila si kwa maana wazi hivyo. Fahiwa inayoibuliwa na leksimu hii katika tamko hili ni kuwa, *anayerejelewa alimpunja msemaji kisiri na kwa njia ya ujanja fulani bila ya yeye msemaji kugundua*. Mtu anapopunjwa kwa namna hii kwa kiasi fulani huchukuliwa kama kwamba ameumizwa sawa na mtu anavyoweza kuumizwa kwa kugongwa na nyundo.

Aidha, kutokana na hali kwamba msemaji anatoa tamko lake mahali panapouziwa bidhaa anayoirejelea, inakuwa ni kadhia mwafaka ya kumrahisishia msikilizaji njia ya kufikia uhusiano. Hali ya msemaji kutoa kauli kwamba, ‘siku ile ulinigonga...’ inakuwa pia ni ufidiaji muhimu kwa msikilizaji kwani inamfanya msikilizaji kuchokonoa mawazo ya kiusuli kuhusiana na jambo alilomtendea msemaji siku fulani iliyopita. Hali hii inamfanya msikilizaji kutumia elimuawali kuhusu kadhia iliyofanyika siku ile inayorejelewa na msemaji. Muktadha huu unamsaidia msikilizaji kufikia dhana inayowasilishwa kuwa *msemaji analalamika kuwa yeye* (msikilizaji) *alimpunja bidhaa kwa njia ya ujanja*.

#### **2.4.5 Kisio la Maana**

Hii ni hali ambapo neno lililo na fahiwa dhabiti kiasi linapanuliwa ukingoni kujumuisha mawanda ya vitengo ambavyo kwa kweli vinapatikana nje ya maana yake mahususi ya kiisimu. Matumizi

legevu ya takwimu za kukadiria, misamiati ya kijiografia na misamiati inayoelezwa kwa njia ya ukanusho ni mifano mizuri (Wilson 2003).

Kutokana na maelezo haya ni kwamba, dhana hizi zinazopanuliwa ukingoni ndizo dhana zinazowasilishwa na wasemaji katika tamko huku ile dhana dhabiti ya neno ikiwa ndiyo dhana iliyosimbwa kisemantiki na neno lile. Katika aina hii ya badiliko dhana inayowasilishwa na neno inajitenga zaidi kutoka kwa ile dhana iliyosimbwa kama ilivyo katika upanuzi wa kisitiari.

Mifano;


(22) a. Mtu A: Si walisema masomo ni ya *bure*. Tena wanaitisha pesa za nini?

b. Mtu B: Kuna kitu ya *bure* hapa Kenya? Wewe anza kuhesabu vitabu

unanunua, mahindi na maharagwe unapeleka shulen...

Neno *bure* kamusini lina maana ya bila malipo Mdee n.w. (2011). Neno *bure* linasimba dhana BURE. Dhana inayowasilishwa na Mtu B inakuwa mbali mno na maana iliyosimbwa na neno *bure* katika Kiswahili. Kwa mfano, hatuwezi kupima kiwango cha masomo kuwa ya bila malipo. Hii ni kwa sababu pana malipo ambayo wazazi nchini Kenya wanagharamika kama vile kununua sare za shule ambazo wanafunzi hawapewi na serikali na gharama nyingine ambazo zinatajwa na Mtu B. Mtu A anapotoa tamko lake ana nia ya kuwasilisha maana ile wazi ya ‘bila malipo’ ila Mtu B anadokeza ukweli kwamba, masomo yanayorejelewa si ya *bure* wazi hivyo bali yana gharama ya kiasi fulani. Kujikita kwenye maana wazi ya neno *bure* ndiyo sababu inayomfanya Mtu B kulalamika kwani anachukulia kuwa masomo ni ya bila malipo ilhali anagharamika kwa kutoa malipo fulani. Katika kisio la maana, dhana inayowasilishwa hutofautiana mionganoni mwa wasilikizaji hivi kwamba kila msikilizaji huwa na ufasiri wake. Tunachukulia kwamba, Mtu A analitumia neno *bure* kwa fahiwa yake madhubuti ila linatumwa kiulegevu na Mtu B. Dhana inayowasilishwa ni kuwa *walimu wanatutoza pesa kwa njia isiyo halali*.

*Kisio la maana*



Mchoro huu unaonesha kwamba, katika kisio la maana, dhana iliyosimbwa kwenye neno inakuwa finyu na dhabiti. Dhana hii inapanuliwa ukingoni na kila msikilizaji. Matokeo yake ni kwamba kila msikilizaji huwa na ufasiri wake amba ni tofauti na wa mwenzake. Hizi fasiri tofauti za wasikilizaji ndizo zinaunda vivuli nya maana.

Mfano;

(23) Eeeh naona watoto wanaenda kula. *Saa saba* imefika mapema.

Tamko hili linatolewa saa sita unusu hivi wakati wa mchana. *Saa saba* ni muda dhabiti unaotambulikana na kuandikwa kitakwimu kama 7:00 mchana au usiku. Msemaji wa tamko hili anachukulia kihafifu wakati wowote mchana kuwa ni saa saba. Mradi tu chakula cha mchana kimekwisha kuandaliwa, kulingana na msemaji, hiyo huwa ni saa saba. Aidha, kwa kuwa msemaji amezoea kwamba wanafunzi huenda nyumbani kula chakula cha mchana, basi wakati huu wa chakula cha mchana unapofika inakuwa ni saa saba kwake. Hii inatokana na mazoea ya msemaji kuwa chakula chochote kinachokuja katika kipindi cha muda fulani baada ya stafthi, aghalabu huja saa saba. Katika saa za Afrika Mashariki hata hivyo, saa saba ndio muda amba huchukuliwa mwafaka na watu wengi kuwa muda wa kula chakula cha mchana. Mbali na madai ya Wilson (keshatajwa) kuwa misamiati ya kijiografia na takwimu za kukadiria hutumika sana katika kisio la maana, tunaongezea kuwa kisio la maana huweza kutokea kwa wingi katika misamiati ya nyakati. Mifano katika Kiswahili ni msimu wa maembe, mchana, magharibi, usiku, msimu wa gharika na msimu wa kiangazi. Kwa Mfano, tunaposema kuwa huwa kuna kiangazi Kisumu kuanzia Disemba hadi Machi, hatutoi wakati na saa dhabiti ambapo kiangazi hicho hutokea hadi kukamilika bali tunakisia tu. Maana ya msemaji katika (23) ni kuwa *wakati wa wanafunzi kwenda kula umetimia*. Maana hii inajitenga sana na maana wazi ya *saa saba* kwani kikawaida *saa saba* – ni kipindi cha wakati kati ya saa sita na saa nane. Hivi ni kusema kwamba, saa saba ni kirai chenye fahiwa dhabiti ila kinatumiwa kiulegevu.

## 2.4.6 Upanuzi wa Kategoria

Katika aina hii ya badiliko, jina la kitu kinachotambulika zaidi la kategoria fulani ya jamii linapanuliwa kutumikizwa kwenye jamii nzima na pana ambayo kwayo kitu hicho kinapatikana (Wilson 2003). Tunaongezea kwamba, jina hili linapotumiwa kwenye jamii nzima, hufanya maana inayowasilishwa kujitenga zaidi kutoka kwa maana iliyosimbwa na jina hilo.

Haya ni matumizi ya majina ya kitu kinacho julikana kuashiria kategoria pana vikiwemo vitu kutoka kwenye rajamu ambazo hazitambulikani zaidi. Majina ya pekee na nomino za kawaida yote huchangia katika upanuzi wa kategoria (Wilson na Carston 2007). Kwa kumnukuu Glucksberg (2001) wanatoa mifano ya majina ('Chomsky', 'Shakespear').

Mfano katika Kiswahili;

(24) Umekuwa *Shaaban Robert?* Kavore kuhuli<sup>9</sup> (sasa sema tusikie).

*Shaaban Robert* ni jina la pekee. Kwa kuwa Shaaban Robert ni mtaalamu aliyetambulika na anayetambulika hadi sasa katika taaluma ya Kiswahili au ulimwengu wa Kiswahili kwa ujumla, jina lake linatumika kumwashiria yeye (Shaaban) pamoja na wasemaji wengine wanaopenda lugha ya Kiswahili. Shaaban Robert alikuwa anatambulikana zaidi kama baba wa fasihi ya Kiswahili kutokana na machapisho yake mengi katika Kiswahili.

Kulingana msikilizaji katika tamko la (24), dhana iliyosimbwa SHAABAN ROBERT huweza kupeana uwezo wa kufikia maarifa ya aina nydingi ya ufahamu ya akilini na kuunda nadharia tete kumhusu Shaaban Robert. Maarifa mengine yanaundwa kutokana na ujumbe ulioko kwenye tamko hili. Ukiwemo ujumbe kwamba, tamko hili linamrejelea mtafiti wakati ambapo anajaribu kukusanya data yake kuhusu maneno ya Kiswahili. Ingawa nadharia tete huweza kutofautiana kutoka kwa msikilizaji mmoja hadi kwa msikilizaji mwingine, kuna uwezekano wa kiwango cha juu kwamba, msikilizaji katika tamko hili ataongezea ujumbe kwamba, Shaaban Robert alikuwa gwiji wa lugha ya Kiswahili na aliandika vitabu na machapisho mengi ya Kiswahili na kwamba anajulikana kama baba wa fasihi ya Kiswahili. Katika hali hii, msikilizaji anafuata njia rahisi kabisa katika kutafuta implikecha kwa kusawazishaji ujumbe, muktadha na athari za kimawazo.

---

<sup>9</sup> Tamko hili ni la lahaja ya Lulogooli, tafsiri yake iko mabanoni.

Kuna uwezakano mkubwa kwamba, mchakato huu unamwezesha kufikia ufasiri ambao kwao, *Shaaban Robert* linajumuisha dhana ya dharura SHAABAN ROBERT\* ambayo inaashiria Shaaban Robert na wasemaji wengine wa Kiswahili wenyе sifa kama yake au inayokaribiana na yake. Msikilizaji anafikia hitimisho kwamba, anayerejelewa anapatikana katika kategoria hii ya dhana ya dharura na huenda anao ujuzi wa kiwango fulani wa lugha ya Kiswahili sawa na alivyokuwa Shaaban Robert. Dhana inayowasilishwa ikiashiria mrejelewa kwenye diskosi hii inajitenga zaidi na dhana iliyosimbwa inayoashiria Shaaban aliywahi kuishi.

Mfano;

(25) *Al-shabab* ni watu wabaya watu wa kulipua.

Jina *Al-shabab* katika tamko la (25) linatumiwa kwa ujumla zaidi. Jeffers na Lehiste (1979) wanaeleza kwamba, upanuzi wa maana aghalabu hutokana na ujumuishaji wa hali mahususi hadi kwenye jamii ambayo kwayo hali ile mahususi inashiriki. Kwa sababu hiyo, majina ya pekee yatatokea kuashiria jamii ya kijumla ya fenomena ile. Dhana ya jina *Al-shabab* katika Kiarabu ni vijana hasa walio na nguvu. Kutokana na kuwepo na kundi linalojiita *Al-shabab* linalojulikana kutekeleza mashambulizi, ndipo wasemaji wa Kiswahili wana mazoea ya kujumuisha kuwa ye yote anayefanya maangamizi ni Al-shabab. Huenda wasemaji hawa wanayo maarifa ya ufahamu kuhusiana na maangamizi ya kundi la Al-shabab waliyowahi kushuhudia.

#### **2.4.7 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu**

Ubunaji wa maana mpya na uundaji wa maneno mapya unapeana data zaidi kwa nadharia ya kipragmatiki na kupeana uelewa zaidi wa hali ya kimaumbile ya mikakati ya kiakili inayohusika (Wilson 2003).

Ohly (1977) anadai kuwa kwa sasa<sup>10</sup> ruwaza zilizopo za kuanzisha misamiati mipy ya kidhahania katika lugha ya Kiswahili inajumuisha:

- i. Maneno mkopo (kutoka Kiingereza)
- ii. Uundaji wa maana mpya ambapo anaonesha kuwa uundaji huu unaweza kuwa: wa maneno mapya kikamilifu, maneno yaliyokuwako tayari katika lugha kuidhinishiwa maana mpya,

---

<sup>10</sup> Tunachukulia kwamba, kipindi kinachorejelewa ni mwaka wa 1977 wakati ambapo jarida tulimotoa nukuu hii lilipochapishwa.

au kupewa mawanda ya kisemantiki ya kipekee au kwa kutumia makundi ya kisintaksi yaliyo na kijalizo. Tunakubaliana na maoni yake kwani hata wakati huu yapo maneno ambayo yanaundwa ama yanapata maana mpya au yanabadilishwa muundo wake wa kimofolojia au wa kifonolojia na kwa hali hiyo kupata maana mpya. Mifano;

(26) a. Mtu A: Ungeomba Gubara pesa ulipie mtoto...

b. Mtu B: Gubara ama nani? huyo mtu ni *mkonobirika* hujawahi juu? Siku ile uliona hakutoa hata ndururu. Yenya vuzwa yazange kunywa ichai<sup>11</sup> (anataka tu awe akija kunywa chai).

Tuchunguze maana za kikamusi za leksimu hizi; *Mkono* 1. Kiungo katika mwili wa binadamu kinachojitokeza kutoka kwenye bega, hutumiwa kwa shughuli nyingi k.m. kushikia vitu 2. Kitu kinachoshika vitu kama mkono 3. Umbo dogo la kitu linalojitokeza kutoka kwenye kitu chenyewe Mdee n.w. (2011). *Birika* 1. Chombo chenyе mfuniko, kishikio na mdomo mwembamba uliopinda cha kutilia chai au kahawa; buli Mdee n.w. (keshatajwa). Kutokana na maana hizi za kisemantiki tunaweza kukisia dhana inayowasilishwa na msemaji. *Mkonobirika* katika tamko la Mtu B inaashiria mtu wala si birika chombo au mkono kifaa. Tuzingatie maana ya tatu ya *mkono* ambayo ni umbo dogo la kitu linalojitokeza kutoka kwenye kitu chenyewe. Kutokana na maana hii, ni dhahiri kuwa, birika ina mkono ambao ni lile umbo linalojitokeza ambalo kwalo chai au kinywaji hupitia tunapokitia kwenye chombo kingine kama vile kikombeni. Si rahisi kupata kitu kilichomo kwenye birika bila kuiinamisha. Aidha, namna mkono wa birika ulivyopindika, si rahisi kukunjuka na hivyo ndivyo ilivyo vigumu kuukunjua mkono wa mtu ambaye ameshikilia kitu chake ndi! Mtu ambaye ni mgumu wa kupeana kitu chake hasa pesa anamithilishwa na mkono wa birika kwani si rahisi kuukunjua mkono huo ukapata kilichomo. Hii ndiyo maana inayowasilishwa na Mtu B. Anafidia hii maana kwa kuonesha kuwa mrejelewa –Gubara huwa hatoi hata ndururu sembuse ampe ye (Mtu B) pesa zake. Kwamba, anachokifurahia Gubara ni kunywa chai. Neno *mkonobirika* pamoja na maana yake mpya limebuniwa kutokana na namna watu wengi nchini Kenya hutumia chai kama kinywaji cha asubuhi. Hivyo basi, ubunaji huu umetokana na yale mazoea ya kutangamana na vyombo kama vile birika ambayo hutumiwa sana kutilia chai.

---

<sup>11</sup> Hili ni tamko la Lulogooli.

Mfano;

- (27) Wakati tulisikia tu kelele, tulitoka *teketeke*, 'paka tukapata zetu. Ukisikia pesa iko mtu anakimbia...

Fromkin na Rodman (1978) wanaeleza kuwa uambatanishaji ni uunganishaji tena wa maneno ya kale kuunda maneno mapya na maana mpya. Leksimu mpya *teketeke* inatokana na neno *teke* ambalo limefanyiwa urudiaji kwa kuambatanisha neno lilelile. Kama ilivyo na upanuzi wa kategoria, ubunaji wa maana mpya, ambao huzuka katika hali ya ubunifu ya matumizi yake, unaweza kushika katika jamii kama ilivyo katika leksimu hii. Matumizi ya *teketeke* yameshika katika jamii kiasi kwamba inaeleweka na watu wengi.

Maana wazi ya leksimu *teke* ni pigo la mguu. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu ni kwamba, mateke hurushwa hasa na ng'ombe anapokimbia labda anapokosa kutekelezewa hitaji fulani. Katika mazingira ya watafitiwa, ufugaji wa ng'ombe unathaminiwa sana na wasemaji wameshuhudia ng'ombe akirusha mateke ndipo wakabuni neno hili. Hali ya ng'ombe kurusha mateke inamithilishwa na namna mtu hurusha mateke. Anaporusha teke la mguu wa kulia, huwa tunasema amerusha teke moja. Anaporusha teke la mguu wa kushoto, anakuwa amerusha teke la pili. Wakati ambapo anarusha mateke kwa kutumia mguu wa kulia na kushoto mtawalia kwa mfululizo kama anavyofanya ng'ombe, huwa tunasema mtu amerusha mateke mengi na hivyo basi huwa ameondoka akirusha mateke. Kuondoka huku ndiko kunasemekana kuwa ni *kutoka teketeke*. Tunaelewa kuwa teke linaporushwa, aghalabu hurushwa kwa kimo kirefu. Kwa namna hiyo, mtu anayetembea haraka au kuondoka mahali kwa haraka husemekana kuwa *ametoka teketeke*. Hii ni kwa sababu huwa anatembea au kukimbia kwa kimo kirefu sawa na mtu anayerusha mateke. Dhana inayowasilishwa katika (27) ni kuwa msemajji *alitoka kwa haraka za ajabu ili asije akachelewa kupata pesa*.

Mfano;

- (28) Haki Dambare, *utanipatia{-ko}* kile kipande chako kingine nikulie pesa?
- (29) *Nikopeshe{-ko}* kitu nilikuuliza

Vitenzi *-pa* na *-leta* kikawaida vinaonekana kuwa vya kuamrisha mtu. Kwa kuwa wasemaji ama hawajui au hawajazoea kutumia maneno ya tasifida katika Kiswahili kama vile *tafadhalii*, wao

huongezea mofimu tamati kwenye vitenzi kama vile *-pa* na *-leta* ili kuonesha upole. Fromkin na Rodman (1978) wanafafanua kwamba, ukopaji mwingine muhimu hutokea wakati ambapo lugha moja inachukua neno au mofimu kutoka lugha nyingine na kuliongezea/kuiongezea kwenye leksimu yake. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu ni kwamba, mazoea ya kuongezea mofimu tamati kwenye vitenzi vya Kiswahili yanatokana na athari ya lugha zao za kwanza. Wanatupatia mifano ya maneno *mbe{-ku}* na *mbe{-kho}* kutoka lahaja za Lulogooli na Lunyore mtawalia na ambapo kitenzi *mbe* kina maana ya *nipe* ambayo inaonekana kuamrisha ila kikiongezewa viambishi tamati {-ku} au {-kho} na kuwa *mbe{-ku}* au *mbe{-kho}* kinapitisha fahiwa ya kuomba. Hivyo basi *mbe{-ku}* na *mbe{-kho}* vinapitisha fahiwa ya kuamrisha mtu akupe kitu chake ila kwa njia ya upole. Athari hii inahamishwa hadi kwenye vitenzi vya Kiswahili ambapo mofimu {-ku} na {-kho} zinakopwa kutoka baadhi ya lahaja za Luluhyia na kufanyiwa mageuzi ili zijitokeze kama mofimu {-ko} ambayo inachukua nafasi ya {-ku} au {-kho} na matokeo yake ni vitenzi kama vile *nipatie{-ko}*, *-leta{-ko}*. Muktadha kwamba, wazungumzaji katika eneo letu la utafiti wamezoea kuonesha adabu wanapotaka kitu kutoka kwa mtu mwingine ndiyo unaowafanya kuongezea viambishi tamati vya lugha zao za kwanza kwenye vitenzi vya Kiswahili ili kuashiria hali ya kuomba. Hata hivyo, tulitarajia mifano (28) na (29) ichukue miundo ifuatayo ya Kiswahili sanifu kwa kutumia neno *tafadhalii*;

(28) *Tafadhali* Dambare, utanipatia kile kipande chako kingine nikulie pesa?

(29) *Tafadhali* nikopeshe kitu nilikuuliza

Jeffers na Lehiste (1979) wanaeleza kwamba, mazoea ya ujumuishaji wa kiambishi tamati au kiambishi tangulizi ni mkondo unaojulikana zaidi ambao kwao, maneno mapya yanaundwa. Wasemaji wengi katika eneo letu la utafiti wamezoea kuambisha vitenzi kwa kupachika mofimu kama vile {-ko} au {-nga} au zote mbili katika kitenzi kimoja. Kama ilivyo katika mfano huu;

(30) Hata sisi *tunauza {-nga}-{-ko}* mahindi tukipata pesa.

Katika mfano huu, mse maji anapachika kiambishi {-nga} kwenye kitenzi kilichoambishwa tayari kuashiria mazoea ya kufanya jambo fulani na kiambishi {-ko} kuashiria hali ya upole wa namna kitendo fulani kinatekelezwa. Mazoea ya ujumuishaji huu wa viambishi unazua maneno mapya na fahiwa mpya katika vitenzi vya Kiswahili ila vitenzi vipyta vinavyoundwa si vya Kiswahili Sanifu.

## **2.5 Hitimisho**

Lengo la sura hii liliwa ni kuainisha na kujadili aina za mabadiliko ya maana ambazo hutokea katika leksimu za Kiswahili. Imedhihirika kwamba zipo aina tofautitofauti za mabadiliko ya maana katika Kiswahili na aina hizi zinaweza kuainishika kwa kutumia mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Aina za mabadiliko ya maana zilizoshughulikiwa ni pamoja na ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kileksika, upanuzi wa kisitiari, upanuzi wa kategoria, kisio la maana, chuku na ubunaji wa maana na uundaji wa kileksimu. Hizi aina za mabadiliko ya maana zimeweza kuainishika katika makundi mawili makuu –ubanaji na upanuzi wa maana. Kwa ujumla, imeonekana kwamba, mabadiliko ya leksimu yametokana na upanuzi au ubanaji wa maana kulingana na muktadha wa matumizi. Upanuzi na ubanaji ultokea katika aina hizi za mabadiliko ya maana na ulisababisha fahiwa mpya kuzuka katika Kiswahili. Hata hivyo, ingawa leksimu nyingi zimepitia usawazishaji wa maana kulingana na miktadha ya matumizi, leksimu za Kiswahili zimesalia na maana zake asilia. Aidha ubunaji wa kileksimu umeonekana kutokea kwa kiasi cha juu katika leksimu ambazo tayari zipo katika Kiswahili. Jambo ambalo lilisababishwa kwa kiasi kikubwa na athari za lugha za kwanza kwa Kiswahili, vitenzi vikiwa vimeathirika zaidi.

## **SURA YA TATU**

### **SABABU ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tutachanganua sababu zinazosababisha usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili. Sababu za mabadiliko ya maana na mabadiliko ya kisemantiki zimeelezwa na wataalamu tofautitofauti na kwa namna mbalimbali. Hata hivyo, Ullmann (1970, 1972) anaeleza kwamba, sababu za mabadiliko ya maana zilielezwa mwanzoni na Meillet (1948). Anataja kwamba, dhana hii ilianzishwa na Edward Sapir miaka arobaini iliyopita<sup>12</sup>. Ullmann (keshatajwa) anatoa maelezo ya Edward Sapir kwa kusema kwamba, lugha hubadilika katika vipashio vyake vya kisarufi. Katika vipashio hivi vyote vya kiisimu, aliona kuwa maana ndiyo iliyokuwa ikikinza mabadiliko kwa kiwango cha chini zaidi. Hii ilitokana na nguvu fulani ambazo zilitambuliwa awali na Antoine Meillet (keshatajwa) na zingine zimetambuliwa katika miaka ya hivi maajuzi. Anazidi kuelezea kwamba, baadhi ya mambo yanayopelekea kubadilika kwa maana ni masuala ya mwanzoni kabisa. Hizi nguvu zilizotambuliwa mwanzoni ndizo kwazo wataalamu kama vile Ullmann (keshatajwa) wameibua sababu zao za mabadiliko ya maana.

Baadhi ya wataalamu ambao wamejaribu kuelezea au kuainisha sababu za mabadiliko ya maana au mabadiliko ya kisemantiki ni pamoja na, Ullmann (1957, 1970, 1972), Pyles na Algeo (1964), Jeffers na Lehiste (1979), Palmer (1981), Hock na Joseph (1996) na Radford n.w. (1999). Sababu zingine miongoni mwa wataalamu hawa zinaingiliana kwa kiasi kikubwa ila zimepewa majina tofauti. Katika utafiti huu, tutaainisha sababu za mabadiliko ya maana kwa mujibu wa Ullmann (1970, 1972) na Palmer (1981). Baadhi ya sababu zinazoainishwa na Palmer (1981) ni pamoja na;

1. Kutokea kisadfa,
2. Mahitaji ya maana mpya,
3. Maneno ya kisayansi na
4. Mwiko.

Ullmann (1970, 1972) anaainisha sababu za kijamii pamoja na za kiisimu ambazo zinaweza kusababisha mabadiliko ya kisemantiki. Katika utafiti huu, tutatumia sababu za kiisimu wala si za

---

<sup>12</sup> Miaka arobaini iliyopita –tunachukulia kwamba hiki ni kipindi kuanzia mwaka wa 1970 au 1972 kwenda mbele. Miaka ya 1970, 1972 ndiyo wakati ambapo vitabu vinavyorejelewa vilipochapishwa.

kijamii. Hii ni kwa sababu ya matumizi ya nadharia yetu inayoelezea masiala kiisimu. Sababu nyingine ya kutumia uainishaji huu ni kutohana na aina ya data tuliyokusanya nyanjani. Sababu za Ullmann (keshatajwa) ni pamoja na,

1. Lugha kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine
2. Uvulivuli wa maana/Ukosefu wa uwazi katika maana.
3. Kupotea kwa motisha.
4. Upolisemia.
5. Miktadha tata na
6. Muundo wa msamiati.

Katika sehemu hii, tutatanguliza baadhi ya sababu za Palmer (1981) kisha tufuatilize za Ullmann (keshatajwa):

### **3.2 Kutokea Kisadfa**

Maana ya neno hutokea kisadfa au kwa bahati nasibu na kwa kiasi kikubwa hakuna uhusiano wa kimaana unaopatikana kati ya neno jipya na maneno asilia. Mfano;

(31) a. Mtu A: 2007 (Two thousand and seven) ulikuwa unasikia tu *chungwa!*

*chungwa!...ukisikia hivyo mtu unajua tu ni pesa.*

b. Mtu B: Sasa saa hii ni NASA ukisikia *nasa!nasa!* ujue ni... ujue umenaswa  
(kicheko)

Leksimu *nasa* ina maana wazi ya shika kama mtego au kitu kinachonata kishikavyo TUKI (2013). Maana mpya iliyoongezewa kwenye leksimu hii inatokana na muktadha wa kisiasa nchini Kenya 2017 ambapo ukiwa ndani ya chama cha NASA basi unasemekana kuwa *umenaswa*<sup>13</sup>. Pyles na Algeo (1964) wanaeleza kwamba, mfanano au utambulisho wa sauti unaweza pia kuathiri maana. Maneno yale mawili yanamatikika sawa, na kuna uhusiano wa maana katika ncha/sehemu ndogo moja fulani: huu ni uhusiano wa sauti na maana. Inatokea kisadfa kwamba, akronimu inayoundwa

---

<sup>13</sup> Umenaswa –huu ni uambishaji wa kitenzi nasa kauli ya kutendewa.

NASA, ambayo inasimamia chama cha kisiasa nchini Kenya, inafanana kifonolojia na leksimu *nasa* ya Kiswahili sanifu. Kwa sababu hiyo, leksimu *nasa* inapata maana mpya ambayo inatokea kisadfa pia maana hiyo mpya inakaribiana na maana ya kawaida ya neno la Kiswahili *nasa*. Maana mpya inayoibuka ni kwamba, *ukiwa mfuasi wa chama cha NASA unasemekana kuwa umefanyika kushikwa chamani kama vile mtego unavyoshika*. Maana hii mpya inakaribiana na maana wazi ya neno la Kiswahili *nasa* ya *kushika kama mtego*. Hivyo basi kuwa mshiriki wa chama cha NASA ni kama *kunaswa mtegoni*. Ingawa maana mpya ya neno hili inatokea kisadfa, kuna uhusiano wa kimaana kwa kiasi fulani kati ya neno jipya na neno asilia.

Tukichanganua tamko la Mtu A ni kwamba, neno *chungwa* limepata fahiwa mpya. Katika muktadha wa Kenya mwaka wa 2007 ambao unatajwa na msemaji, *chungwa* inatumika na ilitumika kama nembo ya chama cha ODM. ODM ni chama cha kisiasa. Herufi *O* inasimamia *Orange* ambalo ni neno la Kiingereza linaloashiria aina ya tunda. Aina hii ya tunda ndiyo nembo ya chama hiki. Tafsiri ya neno *Orange* hadi Kiswahili ni *chungwa*. Kutokana na mazoea ya kisiasa ya kuhusisha *chungwa* na chama cha ODM, neno *chungwa* katika Kiswahili limekuja kupewa fahiwa mpya hivi kwamba, linaashiria *aina ya chama* katika muktadha wa Kenya. Inatokea kisadfa kwamba, neno *orange* lenye maana ya aina ya tunda ambalo liliashiria nembo ya chama fulani, linapotafsiriwa hadi Kiswahili, tunapata tafsiri ya *chungwa*, hivyo basi neno la Kiswahili *chungwa* pia linapata maana zaidi *ya chama cha kisiasa*. Tunaweza kuielezea sadfa hii ifuatavyo, neno *orange* lililoashiria nembo ya chama linapofasiriwa hadi Kiswahili linafanya neno asilia *chungwa* la Kiswahili kupata maana mpya. Maana hii mpya—*ya aina ya chama* imeongezewa kwenye neno *orange* katika muktdha wa Kiingereza cha Kenya na tunapolitafsiri neno hili hadi Kiswahili fahiwa hii mpya ya neno *orange* katika Kiingereza vilevile inaandamana na tafsiri yenyewe na kuliathiri neno *chungwa* la Kiswahili. Matokeo ni neno *chungwa* la Kiswahili pia kupata maana mpya ya *aina ya chama*. Maana wazi ya neno *chungwa* katika Kiswahili ni aina ya tunda linalotokana na mchungwa. Maana mpya ya *chungwa* *kuwa chama* inajitenga zaidi kutoka kwa maana halisi ya neno *chungwa* ambayo ni aina ya *tunda*. Hakuna uhusiano wa kimaana kati ya chungwa—*tunda* na *chungwa*—*chama*. Matokeo haya ni ya kisadfa tu. Philip (1977) anaeleza kwamba, ...mengi ya maneno na sitiari zinazoingia katika lugha, yanaundwa au zinaundwa na wanasiasa. Anaendelea kusema kwamba, ...wanasiasa wako katika biashara ya kushawishi; na wale wanasiasa wafanisi huelekeea kuwa na hali bunifu ya lugha. Ikumbukwe kwamba, diskosi katika mfano wa (31) inatokea mwaka wa uchaguzi mkuu nchini Kenya 2017 na neno *NASA* linaibuka na wanasiasa.

Nembo ya *chungwa* nayo ilianzishwa na wanasiasa msimu wa kutafuta katiba mpya nchini Kenya katika kipindi cha miaka iliyotangulia mwaka wa kutolewa kwa diskosi hii.

### **3.3 Mahitaji ya Maana Mpya**

Maana ya neno hubadilika wakati neno hilo linapohitaji maana mpya. Ugunduzi/uvumbuzi umesababisha binadamu kuwa mbunifufutu katika kupeana majina kwa vitajwa vipyta. Majina kwa kawaida huchukuliwa kutoka kwa maneno yaliyopo tayari, bila kujali iwapo ni kutoka kwenye lugha iliyoko nje au ndani ya jamii.

Mfano;

- (32) a. Mtu A: ...eeh  
b. Mtu B: Unasema MCA amekuwa *mzeekijana*? Pesa zake zinaishia kwa warembo ...Hataki kuachia vijana.

Neno *mzee* lina maana wazi ya mtu aliye na umri unaozidi miaka hamsini hivi nalo *kijana* lina maana wazi ya mtu ambaye si mtoto na si *mzee*. Neno *mzeekijana* ni neno jipya lenye fahiwa mpya. Jeffers na Lehiste (1979) wanaeleza kwamba, msamiati wa lugha unaendelea kutajirishwa kwa kuvumbua maneno mapya ambayo kwa kawaida uvumbuzi huu unajumuisha malighafi ya kileksika ambayo tayari ipo ndani ya lugha. Neno *mzeekijana* limeundwa kutokana na maneno *mzee* na *kijana* ambayo tayari yapo katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na mahitaji ya kutaka neno la kumwitia yule *mzee* aliye na tabia kama zile za vijana, wasemaji waliweza kubuni leksimu hii kuashiria aina hii ya *mzee*. *Mzeekijana* ni leksimu iliyobuniwa kumwitia *mzee* mwenye umri mpevu hasa mwanamume aliye na tabia za kufanya mapenzi na wanawake anaowashinda kwa umri au *mzee* anayependa kuvalia kama *kijana* au yule ambaye angali na nguvu kama *kijana*. Mtu wa aina hii, anakuwa ni kitajwa kipya katika jamii na wasemaji wanabuni neno *mzeekijana* kutoka kwa maneno *mzee* na *kijana* ambayo tayari yapo kwenye lugha ya Kiswahili ili kuashiria kitajwa hiki. Aidha, kutokana na miitikio ya washiriki katika utafiti huu ni kwamba, hawanagetumia leksimu *kijana* peke yake kumwitia *mzee* mwenye tabia hii kwani ingekuwa ni mwiko kumwita *mzee* mwenye umri mpevu kwa kutumia neno *kijana*. Hii ndiyo sababu inayowalazimu kufanya uambatanishaji wa leksimu hizi mbili na kwa mpangilio huo; *mzee* kisha *kijana*, *Mzee* ikiashiria

umri mpevu wa mrejelewa huku leksimu *kijana* ikiashiria tabia zake zinazolingana na zile za vijana.

Mfano;

(33) *Chomelea* akipita umpatie-{*ko*} hii ‘besheni’ yangu. Nimekosa pa kuoshea nyanya.

Tuchunguze neno *chomelea*. Neno hili linatokana na kitenzi *choma* chenye maana wazi ya kuteketeza kwa moto. Kutokana na uvumbuzi wa binadamu kwamba, vyombo vyaplastiki vinaweza kukarabatiwa kwa kutumia moto wa makaa na kwa kutumia plastiki nyingine kuukuu, basi kukatokea watu wanaofanya ukarabati huu. Jina *chomelea* limekuja kupata maana mpya ya kuashiria mtu anayefanya ukarabati huu. Kwa sababu kumetokea kiashiriwa kipykatika jamii ambacho ni mtu anayefanya ukarabati huu, ilikuwa ni vigumu wasemaji kupata jina la kumwitia, ndipo wakafanya ubunaji na kumwita anayefanya kazi hii *chomelea*. Hollmann (2009) anaeleza kwamba, miundo mipyaya maana za maneno ambayo msemaji mmoja hubuni na mabadiliko ambayo kwamba husambaa kwa baadhi au wasemaji wote wa jamii lugha yote huanza kwa namna sawa: msemaji huunda uhusiano fulani wa kibunifu na wa kijumla au muungano kati ya wazo fulani ambalo ye ye anataka kupitisha na (maana ya) neno au usemi fulani ambao upo tayari. Ubunaji wa neno *chomelea* unatokana na tabia ya mtu anayefanya ukarabati wa vyombo vyaplastiki wakati anapoitisha au kutafuta wateja kwa kuradidiradidi neno *chomelea* kwa sauti huku akitembea njiani. Aidha, neno hili limetokana na tabia yake ya kutembea na makaa yanayowaka moto mkebeni anapofanya ukarabati wa vyombo hivi pamoja na hali kwamba anafanya kitendo cha kuchomelea plastiki. Uhusiano huu wa anayetekeleza kazi hii na maana mpya ya neno *chomelea* huenda ulianzishwa na mtu mmoja katika jamii na matumizi yake yakasambaa katika jamii nzima. *Chomelea* ni kitenzi cha Kiswahili kilichoambishwa katika hali ya kutendea lakini kinavyotumiwa kinatumiwa kama nomino. Kitendaki hili kina maana wazi ya kuteketeza kwa moto. Kwa hivyo, kimefanyiwa unyambuaji kwa sababu ya mahitaji ya maana mpya na kupewa fahiwa mpya ambayo ina mahusiano na maana halisi ya neno *choma* la Kiswahili sanifu.

Mfano;

(34) Na wewe unauzaje *malimali*?

*Mali* ni kitu ambacho mtu anamiliki. Katika mfano huu, kuna uambatanishaji wa neno *mali*. Neno *mali* limerudiwa ili kuunda leksimu mpya ambayo ni *malimali*. Kutohana na biashara ya kubadilishana mali, yaani watu kubadilishana bidhaa yenyе thamani fulani badala ya kutumia pesa, kukatokea hitaji la kuitia aina hii mpya ya biashara. Neno hili linaibuka wakati ambapo tayari watu wanajua pesa zipo na zinaweza kutumiwa katika biashara ila kwa sababu ya kukosa pesa na haja ya kutaka bidhaa fulani, wasemaji walibuni biashara ya kubadilishana bidhaa ikawa sasa biashara hii inaitwa *malimali*. Neno *mali* lina maana wazi ya kitu anachomiliki mtu na mara nyingi kitu hiki huwa cha thamani fulani. Maana hii inaonekana kuwa pana kwani inaashiria vitu vingi au kitu chochote ambacho mtu anaweza kumiliki. Kwa kutokea kwamba, vitu vilivyokuwa vikibadilishwa kwa wingi vilikuwa vyombo vidogovidogo kama vile vya kutumia jikoni, wasemaji wanatumia neno *malimali* katika kuashiria vyombo hivi na vitu vingine vinavyouzwa kwa bei rahisi. Si ajabu kumpata mfanyibiashara anayeaza vyombo hivi ameweka kibandiko chenye maneno *Malimali* kwenye duka au kibanda anachouzia. Aidha, si ajabu kukutana na mchuuzi anayechuuza bidhaa zake akiitisha wateja kwa kulikaririkariri neno *malimali* kwa sauti. Wasemaji wanaposikia mchuuzi huyu akinadi, tayari wao hujua kwamba vinavyorejelewa ni vitu vinavyouzwa kwa bei rahisi au kwa kubadilishana bidhaa.

### **3.4 Maneno ya Kisayansi**

Maana ya neno inabadilika wakati ambapo neno hilo linatumiwa kama neno la kisayansi. Maneno ya kisayansi kwa kweli yanachukuliwa kutoka kwenye matumizi ya kila siku ya misamiati ya lugha lakini yanatumiwa kuelezea kitu ambacho ni tofauti kwa kiasi fulani na wazo la kawaida au lililozoeleka.

Mifano;

(35) Ukifika huko uambie Odari *anirushie* {ka}-kitu bwana.

Katika mfano huu, shina la kitenzi *rusha* limeambishwa ili kupata kitenzi *a-ni-rush-i-e*. Kitensi hiki kilivyoambishwa kinaweza kutumiwa kama kitensi cha kawaida na kwa maana yake ya kawaida ya kutuma kitu upande wa pili hasa kwa kutumia nguvu katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kilivyotumiwa katika muktadha huu (35) kinaleta maana tofauti na ile maana asilia, hivi kwamba, wazo linaloibuka si lile lililozoeleka katika matumizi ya kila siku ya Kiswahili. Wazo linalojitokeza ni kwamba, anayezungumziwa kwenye diskosi hii anaombwa atume pesa kupitia

njia ya simu au apeleke pesa kwa njia ya upesi kupitia huduma ya simu. Yaani kupitia M-Pesa. Kutokana na uvumbuzi wa simu za rununu, kisha uvumbuzi wa kuweza kuhawilisha pesa kupitia njia ya simu kutoka mtu mmoja hadi mtu aliye upande wa pili, ndipo kukatokea haja ya kutaka kutajia hali hii ya kutuma pesa. Namna pesa zinavyoweza kusambazwa masafa marefu kupitia huduma ya simu ya M-Pesa, ndivyo wasemaji wanavyohusisha hali hii na jinsi mtu anavyoweza kurusha kitu kikaenda masafa ya mbali kama vile jiwe. Hali hii ya kawaida ya kurusha kitu inahusishwa na kutuma pesa kwa njia ya simu ndipo msemaji akasema kwamba, anahitaji *arushiwe {ka}-kitu (pesa)* kwa maana ya *mtu fulani amtumie angalau pesa kiasi kwa njia ya simu au kupeleka upesi kiasi fulani cha pesa kupitia huduma ya simu*. Kutokana na uvumbuzi huu wa kiteknolojia, wasemaji wamekosa namna ya kuweza kueleza wazo la kutuma pesa kupitia njia ya simu, hali ambayo inawafanya kubuni maana mpya kutoka kwenye neno *rusha*. Msamati huu ni wa matumizi ya kila siku na wazo jipya linalojitokeza liko mbali kwa kiasi fulani na maana asilia ya neno *rusha*. Mfano mwingine unaohusiana na huu ni;

(36) Jioni nitakuwa nimeuza halafu *nitakuempesa*

Neno *mpesa* ni neno lililoundwa kutokana na maneno *mobile* na *money* ya Kiingereza kwa kuchukua herufi *m* ya *mobile* na kutafsiri neno *money* hadi *pesa* ambayo ni leksimu ya Kiswahili ili kuibuka na neno *M-Pesa*. *M* ikisimamia *mobile* na *pesa* ikisimamia *money*. Neno hili ni nomino ya kutajia ama huduma ya *M-Pesa* au duka lenyewe. Hata hivyo, nomino M-Pesa haiwezi ikatumiwa kuashiria ile hali ya kuhawilisha pesa kupitia njia ya simu katika lugha ya Kiswahili ndipo msemaji anajaribu kufanya unyambuaji na matokeo yake ni kitenzi (*ni-ta-ku-e-mpesa*) kinachoashiria *hali ya kutuma pesa kupitia njia ya simu*. Neno hili jipya na maana mpya limetokana na uvumbuzi wa kiteknolojia wa kutuma pesa kupitia njia ya simu kutoka kwa mhudumu mmoja hadi mwingine sawa na ilivyo katika maelezo ya mfano wa (35).

Mfano;

(37) Sawa nikipata kama unga iko *nitakuvutia waya* mtu wangu

Katika mfano huu, *kuvutiwa waya* kuna maana ya kupigiwa simu. Mwanzoni hapakuwa na simu za rununu. Watu walitumia simu ambazo ziliunganishwa kwa waya zilizosambazwa kwa njia ya mfululizo kutoka mti mmoja hadi mwingine hadi kwa mhudumu aliye upande wa pili. Waya hizi ndizo zilizokuwa zikipitisha mawimbi ya sauti mtu anapoitumia simu upande wa pili. Baadaye,

kukatokea simu za rununu. Kwa sababu ya uvumbuzi huu wa simu za rununu, simu hizi za kutumia waya zilizounganishwa mitini zikadidimia katika matumizi yake. Ikawa sasa kumpigia mtu simu kwa kutumia simu ya rununu ni kama *kumvutia waya* sawa na waya zilivyokuwa zikivurutwa kutoka mti mmoja hadi mwingine kwa mfululizo huo hadi kumfikia mhudumu wa upande wa pili. Fauka ya hayo, kutohana na hali kwamba, waya hizo ndizo zilizokuwa zikipitisha mawimbi ya sauti, ndipo hali hii ikahusishwa na kupiga simu ya rununu kwani mawimbi ya sauti yanamfikia mtu aliye upande wa pili kuitia hewani ila si kwa kutumia waya wakati huu. Kutohana na ukosefu wa msamiati wa kuitia uvumbuzi huu mpya wa kisayansi wa simu za rununu katika matumizi ya kila siku ya Kiswahili, ndipo wasemaji wakahusisha kupiga simu ya rununu na hali iliyokuwepo ya kuunganisha waya kutoka mti mmoja hadi mwingine. Jambo ambalo lilipelekea hali ya kumpigia mtu simu ya rununu kuwa ni *kumvutia waya*.

### 3.5 Mwiko

Maana ya neno inabadilika wakati ambapo neno hilo linatumwa kama neno la mwiko. Maneno mengine ambayo ni ya kimwiko yanaweza kusababisha maneno yanayochukua nafasi yayo, kuongezewa maana.

Fromkin na Rodman (1993) wanasema kwamba, kuwepo kwa maneno ya mwiko au mawazo ya mwiko huchochea ubunaji wa maneno ya tasifida. Neno la tasifida ni neno au kirai ambacho huchukua nafasi ya neno la mwiko au hufanya kazi ya kuepuka mada zinazohofisha au zisizo za kupendeza. Tunapanua haya maelezo kwa kuongezea kwamba, hata kama maneno ya tasifida huchukua nafasi ya maneno ya mwiko, baada ya kipindi fulani cha wakati, maneno haya ya tasifida pia huweza kubadilika kwa utaratibu, yakawa ni mwiko kuyatumia.

Mfano;

- (38) a. Mtu A: Naambia Dady...
- b. Dady: ...cuzo<sup>14</sup> siku hizi wamekuwa wengi, najua tu huyo ni *mguu*.
- c. Mtu A:.....

---

<sup>14</sup> Cuzo ni neno la sheng ambalo ni ufupisho wa neno la Kiingereza *cousin*

d. Mtu C : Na ni 'kerenge cha wenya<sup>15</sup> (na ni mguu unataka). Ni *mguu* unataka?

Maana ya kawaida ya neno *mguu* ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda TUKI (2013). Neno *mguu* limepata fahiwa mbili mpya kutokana na hali kwamba linatumiwa kama neno la tasifida. Fahiwa ya kwanza ni kwamba, neno hili linatumiwa *kumwitia mwanamke ambaye anatumiwa kimapenzi kisha kuachwa* kama inavyojitokeza katika kauli ya Dady. Fahiwa ya pili ni kwamba linatumiwa katika nafasi ya *kuitajia ile sehemu ya siri ya mwanamke*, jinsi inavyojitokeza kwenye kauli ya Mtu C. Maneno yapo katika lugha ya Kiswahili ya kutajia vitajwa hivi, ila kwa sababu ya mwiko, maneno haya hayawezি kutumiwa hadharani na inawalazimu watumiaji lugha kutafuta neno jinginge la tasifida la kuweza kuchukua nafasi ya neno la mwiko. Fromkin na Rodman (1993) wanaeleza kwamba, maneno yanayohusiana na kitendo cha ndoa, sehemu za siri na uamilifu wa kiasili wa kimwili huunda sehemu kubwa ya seti ya maneno ya mwiko ya tamaduni nyingi. Kutokana na maarifa haya tunadai kwamba, kwa sababu ni mwiko kutumia maneno yanayohusisha sehemu za siri na kitendo cha ndoa waziwazi katika jamii nyingi za kiafrika, wasemaji wanalahazimika kutafuta neno la tasifida la kutajia viashiriwa hivi au hali hizi. Neno linalochukua nafasi ya neno la mwiko hivyo basi linapata maana zaidi mbali na maana yake asilia kama ilivyo katika mfano wa neno *mguu*. Tunadai kwamba, maneno yanayotumiwa katika nafasi ya neno la mwiko huwa na uhusiano wa karibu sana na neno au maana ya neno la mwiko kwa sababu wasemaji huwa wanaogopa kupoteza maana asilia ya neno la mwiko. Tukichunguza vizuri tutagundua kwamba, neno *mguu* linavyotumiwa lina uhusiano wa karibu na *sehemu ya siri ya mwanamke*. Ubunaji huu huenda umetokana na tafsiri sisisi ya maneno *ekerenge* au *esilenje* yenyé maana wazi ya *mguu* kutoka lahaja ya Lulogooli na Lunyore mtawalia. Wasemaji wa lahaja hizi hutumia maneno *ekerenge* na *esilenje* kama maneno ya tasifida hasa katika kutajia sehemu ya siri ya *mwanamke*. Mfano;

(39) a. Mtu A: Tura yaha ne zigengere zizio yizio<sup>16</sup> (toka hapa na kengele zako hizo) Nitakufinya hizo *makengele* zako...

b. Mtu D: Eeh kwa sababu we huna...

---

<sup>15</sup> Hii ni lahaja ya Lulogooli

<sup>16</sup> Tamko hili ni la Lahaja ya Lulogooli

Maana wazi ya neno *kengele* ni: kifaa ambacho hutengenezwa kwa chuma na hutoa sauti kinapogongwa. *Kengele* ni neno linalotumiwa kwa fahiwa mpya ya kuelezea sehemu ya siri ya mwanamume hasa ile sehemu inayobeba mbegu za uzazi katika mfano wa (39). Pana mfanano wa kifaa kengele na sehemu hii kwani sehemu hii ya siri inaning'inia namna kengele inavyoning'inia inapogonga. Wasemaji wanabuni neno la tasifida lenye uhusiano wa kimaana na neno la mwiko ili kuepuka kukosa kupoteza maana asilia ya neno la mwiko. Hata hivyo, uundaji wa maneno ya tasifida unaweza kukosesha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika mfano wa (39) Mtu A anamtusi Mtu D kwa kutumia neno *kengele* kwa fahiwa yake mpya. Kwa kuwa katika muktadha wa kiafrika si adabu kutaja hadharani sehemu za siri za binadamu, inamlazimu Mtu A kutumia neno *kengele* kwa fahiwa ya sehemu ya siri ya mwanamume. Hata hivyo analitumia neno hili kama matusi.

Mfano;

- (40) a. Mtu A: Kuwa *shoga* ni kitu cha ujinga sana  
b. Mtu B: *Shoga* ni wewe..... na hiso mapikipiki zako  
c. Mtu C: Na mmeanzaje hii mada ya kuwa *shoga*?...si mtafute mambo  
mengine ya kuongea...

Tukidondo kwa ufasili na kwa muhtasari baadhi ya maelezo ya Philip (1977) anasema kwamba, katika kipindi fulani cha wakati kule Uingereza, ilikuja kuwa vigumu kuelezea marafiki zao wenye furaha na wachangamfu kama ‘*gay*’<sup>17</sup> au hata kusema, ‘*it’s a gay day*’ bila hatari ya kueleweka vinginevyo. Anamalizia kwa kusema kwamba, ni hatia kwamba neno lenye herufi tatu tu kupata maana nzima mpya na kudondosha maana yake ya kale haraka namna hivyo. Hali hii vilevile inaonekana kutokea katika neno *shoga* la Kiswahili ambalo likitafsiriwa kihafifu hadi Kiingereza linaweza kuwa na dhana mpya ya Kiingereza ya neno *gay*.

Maana za kikamusi za neno *shoga* ni: 1. Rafiki wa kike wa mwanamke 2. Msenge, mwanamume anayefirwa; hanithi TUKI (2013). Tukitathmini matumizi ya neno *shoga* kwenye diskosi ya (40), inaonekana kwamba, neno *shoga* linatumwiwa kama matusi kwa sababu wasemaji wengi wa

<sup>17</sup> Gay –Maana ya kiasili ya neno hili katika Kiingereza ilikuwa ni kitu au hali inayomchangamsha mtu.

Kiswahili wanajua maana moja tu ya neno hili –*ya mwanamume anayefirwa* na ambapo kitendo hiki ni mwiko. Kwa sababu ni mwiko katika jamii za kiafrika wanaume kushiriki mapenzi au kuoana, neno hili halitumiwi sana ila huenda halijapata tasifida yake. Fromkin na Rodman (1993) wanaeleza kwamba, wakati ambapo kitendo huwa ni mwiko, uashiriaji wa kitendo hiki huweza pia kuja kuwa mwiko. Hivi ni kusema kwamba, kwanza inakuwa mwiko kutenda kitu; kisha inakuwa mwiko kukizungumzia kitu hicho. Kwa kuwa ni mwiko kutenda kitendo cha ushoga katika jamii za kiafrika, vilevile inakuwa mwiko kuitaja hiki kitendo. Hali hii inadhihirika vizuri kutokana na kauli ya Mt C ambaye analalamika kuwa mada hiyo wanayoizungumzia wenzake haivutii na kwamba watafute jambo jingine la kuzungumzia. Maana asilia ya neno *shoga* ya kuitia *rafiki wa kike wa mwanamke* haitumiwi sana na wazungumzaji wengi wa Kiswahili na wengi hawaijui maana hii asilia sawa na ilivyowahi kutokea katika neno *gay* la Kiingereza ambalo maana yake asilia haikutumiwa sana katika kipindi fulani cha wakati<sup>18</sup>. Na lilipotumiwa neno hili, mtu alielewa vinginevyo. Mt C katika mfano wa (40) anaonekana kuelewa neno *shoga* kwa maana ya pili ya mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwenzake wala haijui maana ya kwanza ya neno hili. Ili kuthibitisha madai yetu, hii hapa ni mojawapo ya kauli ya msemaji;

(41) Aaa hatulitumii sana. Kwa sababu wale watu wanachukuliwa si watu wazuri (Mshiriki 11).

Kauli hii inaonesha kwamba, neno *shoga* halitumiwi sana kwa sababu wasemaji wanalihusisha neno hili na *mwanaume anayeshiriki mapenzi na mwanamume mwenzake*. Manaa ya kwanza ya neno *shoga* ambayo ni *rafiki wa kike wa mwanamke* ama haitumiwi sana au kamwe haitumiwi. Katika maeneo yetu ya utafiti, si rahisi upate mwanamke akimwita rafiki yake wa kike *shoga*. Hii ni kwa sababu ya kulihusisha neno hili na maana moja tu ambayo ni hasi. Kwingineko, neno *shoga* linatumiwa kwa maana zote mbili. Kwa mfano katika maeneo ya Unguja na maeneo mengine ya pwani ya Kenya na Tanzania neno hili linatumiwa sana na wanawake marafiki kuitania. Matokeo ya *shoga* kutumiwa kama neno la mwiko katika maeneo hasa ya bara ya Kenya ni kubanika kwa maana ya neno hili.

---

<sup>18</sup> Tazama maelezo ya Philip (1977) katika uk. 52

### **3.6 Lugha Kupokezanwa Kutoka Kizazi Kimoja Hadi Kingine**

Ullmann (1970) akimnukuu Meillet (1948) anasema kuwa lugha hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kukoma. Kwa sababu hii, kila mtoto anapaswa kujifunza lugha upya. Baadaye watoto wataelewa maana za maneno vinginevyo. Hata hivyo, wao hurekebishwa lakini kwa namna nyingine wakikosa kurekebishwa kunaweza kutokea mabadiliko ya kisemantiki katika kizazi kipy. Tunaongezea kuwa, wasemaji wanayatumia maneno ama kwa kupanua maana zake au kwa kubana maana zake asilia. Hatimaye, matumizi ya maana mpya zinazozuka huweza kusambaa katika jamii lugha nzima na kusababisha kusahaulika au kutoweka kwa maana asilia za maneno yale. Mabadiliko ya kisemantiki huweza kutokea kwa sababu wasemaji hawazijui maana zote halisi za leksimu fulani tangu utotoni mwao na/au wanazijua maana za pembeni pekee.

Mfano;

- (42) a. Mtu A: Nilisikia ati dawa ya *kirusi* ilipatikana.  
b. Mtu B: Wapi? Jibebebebe ukisema ati kuna dawa... hiyo ni ya watu  
hawana...
- (43) a. Mtu A: Tena nilisikia Mafunya alikuwa na *ugonjwa*  
b. Mtu B: Eee huyo alikuwa kwa ARVs

Kirusi ni neno lenye maana wazi ya kiini kinachosababisha ugonjwa. *Kirusi* ni leksimu ambayo inaweza kueleweka vinginevyo na watoto wa kizazi kipy. Watoto wanaweza kuhusisha leksimu hii na maana ya ukingoni pekee wakakosa kujua maana yake wazi kwamba, panapotajwa neno *kirusi*, kulingana na mtoto, itakuwa ni ugonjwa wa UKIMWI. Mtoto asiporekebishwa hataelewa kwamba, *kirusi* ni haiponimia inayojuimuisha aina nyingi za virusi. Hali ya ubanaji vilevile inatokea kwenye neno *ugonjwa* katika mfano wa (43).

Mifano;

- (44) a. Mtu A: *Kijana* yangu tangu aanze muhula hajaitisha hata pesa lakini msichana  
ameitisha mara nne sasa.  
b. Mtu B: Wasichana ni hivyo si kama *vijana*. *Vijana* wanakaa ngumu.

c. Mtu A: Mtu alisema wasichana ni mayai.

(45) a. Mtu G: Kageha alizaa *kijana* ama msichana?

b. Mtu H: Nikidhani ni *kijana*

Neno *kijana* katika Kiswahili lina maana za: 1. Mwana mdogo; mtoto wa kiume au wa kike hadi umri wa kubaleghe TUKI (2013) 2. Mtu mwenye umri kati ya miaka kumi na minane hadi miaka thelathini na mitano 3. Mtu ambaye si mzee wala si mtoto Mdee n.w. (2011). Kutokana na kauli zilizoko kwenye diskosi (44) na (45), ni dhahiri kuwa, neno *kijana* linaleweka na wasemaji wengi kwa maana ya juu ya kuashiria mwanamume tu. Katika Kiswahili sanifu, neno *kijana* linaashiria msichana au mvulana ambaye amebaleghe. Watu walioko kwenye diskosi hizi ni watu wazima. Wasemaji hawa huenda wamekua tangu utotoni wakielewa kuwa kijana ni mtoto wa kiume wala si wa kike. Inaonekana kuwa wasemaji hawakurekebishwa tangu utotoni. Wasemaji wanapunguza viashiriwa vya neno hili bila kukusudia na matokeo ni kubanika kwa maana yake halisi.

Kwingineko, Habwe n.w. (2010) wanaeleza kuwa, mahusiano ya kinasaba huonyeshwa kuitia kwa lugha na huathiri lugha pia. Wanaendelea kueleza kuwa, kila utamaduni huwa na dhana tofauti kuhusu, kwa mfano, nani baba, ndugu, ami, mume, na kadhalika. Katika maeneo yetu ya utafiti, wasemaji wanayo majina ya kinasaba ya kutofautisha kati ya mtoto wa jinsia ya kike na yule wa jinsia ya kiume katika lugha zao za kwanza. Kutokana na mazoea yao ya kutofautisha majina ya jinsia zote katika lugha zao za kwanza, wasemaji wanaona ni vigumu sana kutumia jina moja *kijana* kuashiria watoto wa jinsia zote. Hii ndiyo sababu ya wao kutumia jina kijana kwa jinsia ya kiume wala si ya kike. Aidha, huenda mazoea haya yanatokana na lugha za kwanza za wasemaji ambapo, wanapolitafsiri neno *kijana* kutoka Kiswahili na kulitumia kama /ikija:na/ katika Lulogooli au Lunyore, maana inayojitokeza inaashiria *mtoto wa kiume* pekee awe amebaleghe au hajabaleghe. Jinsi tulivyotangulia kutaja, huenda wasemaji katika diskosi (44), (45) walipata jina kijana likitumiwa kwa kuashiria mtoto mwanamume tu na maishani mwao wamelitumia kwa maana hiyo. Matokeo ni kubanika kwa maana wazi ya neno *kijana* kwa kulitumia kuashiria mvulana tu.

### **3.7 Uvulivuli wa Maana/Uwazi Katika Maana**

Maana za maneno huweza kubadilika kutokana na hali ya kiasili ya maneno, uwingi wa hali za maneno yenye, ukosefu wa uzoefu katika maneno na ukosefu wa mipaka wazi, haya yote huchangia katika matumizi yake kubadilika. Kwa kuwa neno huwa halina mipaka ya kimaana, maana yake huweza kuwa si dhabiti, hivyo kubadilikabadi.

Mifano;

(46) a. Mtu A: Hebu tuone, *Mombasa* iko na kaunti ngapi?

b. MtuB: Ni taaatu ama ni tanooo?

(47) a. Mtu D: Kijana yangu vile alirudi, alisema walifika *Mombasa* wakaona

sanamu ya Vasco ta kama (Vasco da Gama)<sup>19</sup>. Pesa yangu

haikuenda bure hivyo...

b. Mtu Q: ...eeh

Leksimu *Mombasa* inavyotumiwa katika tamko la Mtu A na Mtu D inatumwa kivingine. Maana ya kawaida ya leksimu *Mombasa* ni mji wa kale unaoaminika kuwa ndiyo chanzo cha historia ya Kiswahili. Katika maana hii, neno *Mombasa* linaashiria sehemu moja tu. Mtu A anaitumia leksimu hii kuashiria sehemu zote za pwani ya Kenya. Kulingana na kauli ya Mtu A, tunatathmini kwamba, *Mombasa* ni pwani nzima ya Kenya. Katika ulimwengu halisia, *Mombasa* ni kaunti moja mionganini mwa kaunti nyingine zilizoko pwani ya Kenya. Kaunti nyingine katika eneo hili ni Lamu, Kwale, Kilifi, Tana River na Taita Taveta kijiografia. Kutokana na asili kwamba *Mombasa* ni mji unaojulikana zaidi kuliko miji mingine katika pwani ya Kenya, na hali kwamba, ndio mji mojawapo unaojulikana katika asili ya Kiswahili, na ni mji uliokuwa wa kibiashara na kuendelea zaidi kuliko miji mingine pwani, ndipo unatambulika zaidi. Hali hii ndiyo inafanya wasemaji hasa wa bara kujumuisha miji mingine yote inayopatikana pwani ya Kenya katika maana ya leksimu *Mombasa*. Hali hii ya kutumia neno *Mombasa* katika kutajia miji yote ya pwani ndiyo

---

<sup>19</sup> Vasco da Gama –neno hili limewekwa kwenye mabano ili kuonesha maendelezo na matamshi yake sahihi.

inayosababisha maana ya leksimu *Mombasa* kupanuka. Aidha, kwa sababu watu wengine hawajazoea kutumia majina ya miji mingine ya pwani kama vile Malindi, inawalazimu kutumia neno *Mombasa* kwa kujumuisha miji mingine yote iliyoko pwani ya Kenya. Huenda hii ndiyo sababu ya Mtu D kudhania kwamba sanamu ya Vasco da Gama inapatikana Mombasa wakati ambapo tunafahamu kwamba, sanamu hii inapatikana Malindi. Ili kutoa ithibati zaidi, huu hapa ni mfano wa kauli ya mshiriki:

(48) *Mombasa* ni kama mtu ameenda mahali kama Malindi, ameenda mahali kama Kilifi, Kwale... huko ni Mombasa... (Mshiriki 10)

Msemaji katika kauli hii huenda hajawahi kufika pwani ya Kenya. Kauli hii inaonesha kwamba, wasemaji hawawezi kuweka mipaka wazi kati ya mji wa Mombasa na miji mingine inayopatikana pwani ya Kenya. Aidha, kutokana na kukosa uzoefu katika matumizi ya neno *Mombasa*, wasemaji wanaishia kutanua maana ya neno hili. Sababu hizi zote zinasababisha neno *Mombasa* kupata fahiwa mpya ambazo zinasababisha neno hili kupanuka maana.

Tuchunguze mfano mwingine;

(49) Tony niuzie *mchele*, leo nimeamua kula *mchele*. Na unga ya chapati unauzaje...

Zipo leksimu ambazo zimeleksishwa katika Kiswahili hivi kwamba, maana yazo zinajumuishwa ndani ya maana ya neno jumuishi. Neno *mchele* ni mfano mzuri wa neno jumuishi. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa, katika lugha ya Kiswahili kuna maneno sita ya kutajia mchele:

- i)      Mchele –mchele mbichi
- ii)     Mpunga –mchele ukiwa shambani
- iii)    Mashendeya –mchele mbovu
- iv)    Pilau –mchele uliopikwa kwa viungo
- v)     Biriani –mchele uliopikwa kwa birinzi
- vi)    Wali –mchele uliopikwa

Maana ya leksimu *mchele* kamusini ni chembechembe za mpunga uliotwangwa na kuondolewa makobo Mdee n.w (2011). Maana hii imejumuisha maana nyingine sita za kila aina ya mchele tulizozitaja hapo juu. Tukichunguza vizuri aina za michele zilizoorodheshwa hapo juu ni kwamba,

ingawa *wali* ambao ni mchele uliopikwa, maana hii imeleysishwa ndani ya neno jumuishi *mchele*. *Wali* linatumwa pia kama neno jumuishi na linaleksisha aina nyingine za wali kama vile pilau, biriani, wali wa samli na wali wa nazi.

Tukirejelea tamko la msemaji (49) ni kwamba, *ameamua kula mchele*. Maana inayojitokeza ni tata kutokana na utata wa kileksika wa neno *mchele*. Huenda ikawa msemaji anaashiria kula mchele mbichi ambao tayari umeshatolewa makobo au ameamua kula mashendeya. Hata hivyo, pana uwezekano kuwa, msemaji huenda alikusudia kuitisha ujumbe kwamba *ameamua kula wali*.

Tukielezea sababu zinazomfanya msemaji kutoa tamko hili ni kwamba, huenda msemaji hajui hali ya kiasili ya kitajwa cha neno hili. Kwa mfano, labda msemaji hajawahi kushuhudia mchele ukiwa shambani. Graddol n.w. (1987) wanaeleza kwamba, maneno jumuishi mengi ambayo tunatumia katika uainishaji wa haiponimu ni itikadi zetu kuu: yamekuwa sehemu ya mtazamo wa kiulimwengu wa utamaduni wetu kwa karne nyingi, na kwa sababu hiyo yamechukuliwa kwa hali ya kawaida kama ukweli, na yana ukinzani sana na mabadiliko. Tunajenga maelezo yetu kutokana na nukuu hii kwa kudai kwamba, msemaji hajawahi kupata kuona aina tofauti za michele tukianza na mpunga—*mchele ukiwa shambani* hadi kwa aina za wali kama vile wali wa nazi na wali wa samli. Hali hii inamsababisha msemaji kujumuisha maana za aina zote za michele kwenye leksimu *mchele* na kulingana na yeye (msemaji) inakuwa ni *itikadi* na jambo la kawaida na lililozoleka kiasi kwamba, neno hili haliwezi kubadilisha maana yake katika matumizi. Aidha, kutokana na wingi wa hali zilizozalishwa za aina za michele, inaonekana kwamba, ama msemaji hazijui aina hizi zote au anajua aina chache tu za michele. Hali hii ya haiponimu nyingi za kuashiria aina za michele zinazoleksishwa katika haiponimia *mchele* inasababisha usawazishaji wa leksimu *mchele* kufanyiwa ujumuishaji. Aidha, katika matumizi ya lugha ya kila siku, wasemaji hawajajizoeza kutumia majina mengine ya kutajia aina za michele au hawayajui kabisa, hivi kwamba, wana mazoea ya kufanya ujumuishaji. Matokeo ni kupanuka kwa maana ya neno *mchele* katika matumizi.

Mwisho ni kwamba, ukosefu wa mpaka wazi katika maana za haiponimu za *mchele* huweza kumfanya msemaji kukanganyikiwa kiasi cha kumfanya yeye kuchagua neno moja tu lililozoleka la kuitia aina moja ya mchele na kulitumia katika kuashiria aina nyingine zote za michele. Kwa mfano, hakuna mpaka wazi kati ya maana ya leksimu *mchele* na maana za haiponimu zake. Wala hakuna mpaka wazi kati ya maana za haiponimunyenza zinazopatikana chini ya haiponimia

*mchele*. Mfano, maana ya neno *mchele* ni mchele mbichi. Kianalojia, inafuatia kwamba, kwa kuwa *mpunga* huwa mbichi, tunadai kwamba, *mpunga* ni mchele, na tunafikia hitimisho kwamba, *mpunga* basi ni aina ya mchele mbichi ulio shambani na maana ya neno *mchele* hivyo basi si wazi. Uvulivuli huu wa maana ndiyo unafanya wasemaji wengi kujumuisha kila aina ya *mchele* katika maana ya leksimu *mchele*. Jambo hili linasababisha maana ya neno *mchele* kupanuliwa katika matumizi yake.

### 3.8 Kupotea kwa Motisha

Hali ya maneno kuendelea kuegemezwa katika mizizi yao, na katika maneno mengine ya jamii moja huweza kudhibiti maana ya neno kwa kiasi fulani. Zaidi ni kwamba, miungano mingine ya maneno kama vile mizizi ya maneno katika lugha iko hatarini, hivi kwamba, fahiwa inayoibuka inaweza kuwa mbali zaidi kutoka kwenye maana asilia.

(50) Siku ile *ulinigonga*, leo unipimie vizuri...

Katika Kiswahili, leksimu *gonga* ina maana ya kukutanisha kitu kimoja na kingine kwa kuvipiganisha Mdee n.w. (2011). Leksimu *gonga* ilivyotumiwa katika tamko la (50) inaonekana ama imeongezewa maana au maana yake asilia imedondoshwa kisha ikapewa maana mpya. Hii ni kwa sababu, maana halisi ya leksimu iko mbali zaidi na fahiwa mpya inayoibuliwa. Fahiwa inayoibuliwa na leksimu hii katika tamko la (50) ni kwamba, *anayerejelewa alimpunja msemaji bidhaa kisiri na kwa njia ya ujanja fulani bila ya yeye msemaji kugundua*. Anayerejelewa kwenye diskosi hii anaweza kuwa amefanya hivi labda kwa kumpimia msemaji bidhaa ambayo haifikii thamani ya pesa alizotoa kununua bidhaa ile. Kwa sababu ya umbali wa fahiwa mpya kujitenga na maana halisi ya neno *gonga*, maana halisi ya neno *gonga* inaweza kukosa motisha katika matumizi ya lugha na kuifanya maana ya pembedi ya neno hili kutumiwa kama maana kuu. Hali hii ikitokea, mzizi wa kisemantiki wa neno *gonga* hivyo basi utakuwa hatarini mwa kufa. Matokeo yake yatakuwa ni kuhamisha maana kikamilifu, jambo ambalo litafanya maana asilia kupotea.

Mfano;

(51) a. Mtu A: Kuwa *shoga* ni kitu cha ujinga sana

b. Mtu B: *Shoga* ni wewe..... na hizo mapikipiki zako

c. Mtu C: Na mmeanzaje hii mada ya kuwa *shoga*?...si mtafute mambo

mengine ya kuongea...

Neno *shoga* kwenye diskosi hii, linatumwa kama matusi kwa maana ya wanaume wanaofanya mapenzi au wanaooana. Radford n.w. (1999) wanaeleza kwamba, mabadiliko ya kisemantiki kama kawaida hutanguliwa na tofauti za kisemantiki–kwa maneno mengine katika hatua fulani ya uhawilishaji maana kutoka maana A hadi maana B, maana hizi zote zitakuwepo wakati huo katika jamii. Wanatoa mifano kutoka lugha ya Kiingereza kwa kusema kwamba, wakati mmoja, hivyo basi, maana hizi mbili ‘*joyful*’ na ‘*homosexual*’ zilikuwa maana za neno ‘*gay*.’ Wanaendelea kudai kwamba, kwa utaratibu, katika kipindi cha wakati, maana moja imeanza kutumiwa zaidi kuliko ile nyine kiasi kwamba, maana ile nyine inakufa. Hali hii pia imetokea kwenye neno *shoga* katika matumizi ya kila siku ya Kiswahili.

Kwa sababu ya wasemaji katika maeneo yetu ya utafiti na maeneo mengine kutumia neno *shoga* kwa maana moja pekee, maana ya kwanza ya neno hili inakosa motisha katika matumizi. Hii ni kumaanisha kwamba, maana ya kwanza ya neno *shoga* ya *jina linalotumiwa na wanawake marafiki kuitania* iko hatarini mwa kufa katika baadhi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hali hii inatokea kwa sababu ya wasemaji kuegemeza maana ya neno hili kwenye mzizi mmoja wa shoga kuwa mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwenzake. Hali hii inalidhibiti neno hili kwa kulifanya kutumiwa katika muktadha mmoja mahususi. Isitoshe, maana hii moja wanayoitambua wasemaji ya *mwanamume anayeshiriki mapenzi na mwanamume mwenzake*, haitumiwi sana kwa sababu kitendo chenyewe ni mwiko. Hii inatokana na hali kwamba, katika utamaduni wa kiafrika hali ya ushoga haikubaliwi. Hali ya kulihusisha neno hili na kitendo cha mwiko, inafanya neno hili kupoteza motisha ya maana zake mbili. Ilivyo kawaida na maneno ya mwiko, huwa yanatafutiwa neno mbadala la tasifida. *Shoga* likitafutiwa neno mbadala basi mizizi yake yote itakuwa hatarini na matumizi yake ama hayatakuwepo kabisa au yatazidi kuwa finyu zaidi.

### **3.9 Upolisemia**

Neno linaweza kupata mabadiliko ya maana au fahiwa mpya bila ya kupoteza maana yake asilia. Maneno hubadilika maana kulingana na jinsi yanavyotumiwa kimahususi au jinsi yanavyobadilika kimatumizi. Tunaongezea kwamba, ni tabia ya kila siku ya watumiaji lugha kunururisha maneno na sifa mojawapo ya mawasiliano ya binadamu ni upolisemia.

Mifano;

(52) a. Mtu A: Unajua hata Musumba *anakunywa*....

b. Mtu B: mmm! *Anakunywa* 'paka chang'aa...

(53) *Imagine* siku yote *sijakunywa* sigara. Si unipee mbili... nitakulipa...

Leksimu *-nywa* katika Kiswahili ina maana wazi ya kutia kitu kiowevu kinywani kisha kukimeza. Leksimu hii inaweza kutumiwa kimahususi pia kutumiwa kwa kubadilisha matumizi yake. Kimahususi kwa sababu, vipo vinywaji vingi ambavyo hunywewa kama vile maji, kahawa, chai, uji na soda. Hata hivyo, msikilizaji anaposikia kwamba fulani *anakunywa*, kinachomjia akilini ni *kunywa pombe* hata kama siyo katika muktadha wa baa au mahali panapouzwa pombe. Mfano wa (52) ni ithibati nzuri. Hali hii inafanya maana ya neno *kunywa* kutumiwa kimahususi kwa kuvitenga vitu vingine vyote viowevu na vinavyoweza kunywewa na kuhusisha kitendo cha *kunywa* na pombe tu. Hali hii ya neno kutumiwa kimahususi inafanya neno *kunywa* kupata maana zaidi. Aidha, neno *kunywa* linabadilika matumizi kwa kuwa, maana yake ya kawaida inahawilishwa hadi kwenye kitendo cha kuvuta sigara. Msemaji wa tamko la (53) anavyolitumia neno *kunywa*, inaonekana kwamba, anabadilisha matumizi ya neno hili kutoka kwa hali ya *kunywa vitu viowevu* na kulihawilisha hadi kwenye hali ya *kuvuta sigara*. Neno hili basi linapata maana zaidi na kubakisha maana yake asilia. Aitchison (2003) anaeleza kwamba, maneno mengi katika lugha yana maana zaidi ya moja lakini namna ambazo kwazo, maneno hubeba maana nyingi huweza kutofautiana; hali hii imetetewa. Namna ya kitenzi *kunywa* kinavyobeba maana kwa kutumiwa kwa hali mahususi ya *kunywa pombe* na pia kubadilisha matumizi yake na kuhusishwa na *hali ya kuvuta sigara* ndiyo inayosababisha neno hili kuwa na maana zaidi ya moja katika miktadha ya matumizi yake.

Mfano;

(54) a. Mtu A: Najua Dady anaongea tu na hajakata kura.

b. Mtu B (Dady): Bwana wacha zako, kura niko nayo na niko *ndani*, *ndani*  
kabisu.

c. Mtu A: Sema NASA imekunasa 'paka umeingizwa *ndani*.

Leksimu *ndani* imetumiwa kwa maana mahususi katika diskosi (54). Kikawaida, neno *ndani* linatumiwa kuashiria mahali ambapo si nje. Hivyo basi, neno *ndani* linaweza kuashiria ndani ya nyumba, ndani ya kitabu au ndani ya shimo. Katika muktadha wa Kenya, leksimu hii imepata fahiwa mpya ya *kuwa ndani ya chama*. Katika msimu wa kampeni mwaka wa 2017, neno *ndani* linapotajwa, msikilizaji hujua kuwa ujumbe unaopitishwa ni kwamba, *mtu fulani ni mfuasi sugu wa chama fulani cha kisiasa na ni vigumu kumbandua kutoka chamani*. Maana hii inatumiwa kimahususi na inafanya neno *ndani* kuashiria kuwa *ndani ya chama* kama ilivyo katika mfano wa (54)b. Ikumbukwe kwamba, maana hii ya ukingoni inashika sana katika msimu wa kampeni za uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka 2017 kiasi kwamba, zipo nyimbo za kisiasa zilizobuniwa na zinatumia hili neno kwa fahiwa hii mpya. Zinapoimbwa, wasemaji wanaelewa ujumbe unaopitishwa kuwa *ndani ni kuwa ndani ya chama*. Kwingineko, leksimu *ndani* inabadilisha matumizi yake hivi kwamba, inatumiwa kuashiria rumande au jela kama ilivyo katika tamko hili;

(55) Aendelee tu kunywa, atawekwa *ndani*!

Katika tamko hili, neno *ndani* linachukua nafasi ya neno *jela* ila kiashiriwa kinabakia kuwa kilekile. Aidha, maana asilia ya neno *ndani* inabakia vilevile. Hali ya neno *ndani* kubadilisha matumizi na kutumiwa kuashiria mahali fulani mahususi—*Jelani au rumande* inayapanua mawanda ya kisemantiki ya neno hili. Fahiwa hii ya kuhusisha ndani na rumande au jela inatokana na hali kwamba, mtu anapokamatwa na polisi au askari, mtu huyo hufungiwa katika chumba cha wafungwa na hawezo tena kuonana au kutangamana na watu aliokuwa akitangamana nao kwa urahisi. Mafarakano haya yanamfanya mse maji kusema kuwa fulani yuko *ndani* au *fulani atawekwa ndani*.

### **3.10 Mabadiliko Kutokea Katika Miktadha Tata**

Hapa ni pale ambapo neno fulani huweza kuchukuliwa kwa fasiri mbili tofauti huku maana ya neno hilo katika ujumbe ikisalia vilevile. Tunaongezea kwamba, neno fulani linapotumiwa kwa maana mbili au zaidi huweza kutokea utata wa kimawasiliano ila dhana inayowasilishwa na mse maji inabakia kwenye tamko hilo bila kuvurugwa.

Kwa mfano, neno *tengeneza* linatumiwa kwa fahiwa zaidi ya tatu za pembeni mbali na maana zake za kileksika. Maana za kileksika za neno *tengeneza* ni: 1. Fanya kitu kwa kutumia madini, mbao

n.k. 2. Fanya kitu kilichoharibika kiwe sawa tena Mdee n.w. (2011). Tukizingatia maana hizi za neno *tengeneza*, hebu tutazame mifano ifuatayo;

(56) a. Mtu G: Huyo mtu *atatengenezwa* vizuri nakwambia.

b. Mtu F: Itakuwa kama yule jamaa wa pikipiki, aliundwa damu ikatoka kwa kichwa.

(57) a. Mtu A: Siku ile tulienda kwa matanga ya Samweri *walitujenga* vizuri...

b. Mtu B: Hao watu *walitutengeneza*. Nilikula nikajua hivi ndio watu wanaishi.

(58) Mtu D: Huyo mtu wa *kutengeneza* kelele anakuja?

Miktadha ambamo neno *tengeneza* linatokea inatofautiana kwa kiasi kikubwa. Katika kila muktadha, neno *tengeneza* limeongezewa maana nyininge wala maana yake asilia haijatumiwa. Kwa sababu ya matumizi ya neno hili katika kila muktadha wa aina yake, linaishia kupata maana mpya ambazo tunazieleza hivi; Mtu G analitumia neno *tengeneza* kwa maana ya *kumpiga mtu hasa mwizi kiasi cha kumfanya anayetoa kipigo kile aridhike kwamba ametoa kipigo cha kuweza kumwumiza anayepigwa*. Mtu B naye anaweza kuwa analitumia neno *tengeneza* kwa maana nne, ya kwanza ikiwa ni *kulishwa*, ya pili *kupewa msaada wa chakula*, ya tatu *kulishwa kwa vinono ambavyo kawaida mtu fulani huenda hajawahi vila au amechukua muda mrefu kabla ya kuvila au dhana kuwa *alilishwa kiasi cha kwamba alishiba zaidi tukilinganisha na jinsi alivyowahi kushiba kabla**. Naye Mtu D analitumia neno hili kwa maana ya *kupiga kelele ovyoovyo*. Maana za Mtu B ndizo zinakaribiana sana na maana ya kawaida ya 2 hapo juu ya kufanya kitu kilichokuwa kimeharibika ili kifae tena. Maana za Mtu G na Mtu D katika matamko yao mtawalia zinatokea kuwa kinyume cha maana hii ya 2. Kwa mfano, *kutengeneza mtu* kwa maana ya *kumpiga* ni kinyume cha kufanya kitu kilichokuwa kimeharibika ili kifae tena. Tunachukulia kwamba anayepigwa atakuwa *anaharibiwa* wala hatakuwa anafanywa kuwa sawa tena. Tukichunguza kauli ya Mtu D, tunadai kwamba, *anayepiga kelele ovyoovyo* atakuwa *anayaharibu* mazingira bali si kuyaboresha mazingira au kuyafanya yafae tena. Kutokana na hii miktadha mipyä ya neno *tengeneza*, kila msikilizaji anaposikia kauli hizi (56, 57, 58) za matumizi ya neno hili, huzua ufasiri

wake ambao ni tofauti na wa mwenzake. Matokeo ni kupatikana kwa fasiri nyingi za neno tengeneza ambazo zinafanya hili neno kupanuka maana. Tukizingatia fahiwa hizi mpya za neno *tengeneza*, hebu tudondoe tamko la Mtu G;

(56) a. Mtu G: Huyo mtu *atatengenezwa* vizuri nakwambia

Msikilizaji ambaye haelewi au anayeelewa maana zote za neno *tengeneza*, zikiwemo zile fahiwa mpya, anaposikia tamko hili huweza kutatizika kuelewa ujumbe unaopitishwa. Kwa mfano atajiuliza; Iweje mtu *atengenezwe*? Iweje mtu aharibike kisha afanywe kuwa sawa tena? Aidha, anayeelewa maana za ukingoni za neno hili atashindwa kuelewa iwapo *kutengenezwa* ni *kulishwa kwa vinono* au ni *kupewa msaada wa chakula* au ni *kupigwa ipasavyo*. Hapa patakuwa pametokea utata wa kimuktadha kwa sababu neno hili linatumwa katika miktadha ainati ukiwemo ule muktadha ambamo linaweza kutumiwa kwa maana yake halisi. Tunadai kwamba, ni kutokana na utata wa kimuktadha wa matumizi ya neno *tengeneza*, ndipo neno hili linapata fahiwa mpya mbali na maana yake halisi. Hii ni kwa kuwa, msikilizaji anaweza kufasiri kauli za Mtu G na Mtu B na kupata dhana nyingi. Mfano, kauli ya Mtu G inaweza kuzua fasiri za *kulishwa kwa vinono* au ya *kupigwa ipasavyo* ila ujumbe uliobebwa katika tamko hili na msemaji utasalia vilevile. Kuzuka kwa fasiri mbili au zaidi ndiko kunasababisha neno *tengeneza* kupata fahiwa zingine mpya. Hali hii vilevile inasababisha kudhoofika kwa mawasiliano.

Ni vizuri kuelewa kwamba, maana mpya za leksimu *tengeneza za kulishwa* au *kulishwa kwa vinono* au *kupewa msaada wa chakula* zimechimbuka kutokana na muktadha kwamba, jinsi kifaa fulani kama vile baiskeli kinavyoharibika na kuhitaji *kutengenezwa*, ndivyo mtu aliye na njaa huchukuliwa kama kifaa kilichoharibika na anahitaji *kutengenezwa*. Manaa hizi zinakaribiana na maana wazi kwa sababu mtu anapokuwa na njaa huwa ni kama ameharibika au amepata kasoro hivyo basi anahitaji *kutengenezwa* ili afae tena katika matumizi namna kifaa kama vile baiskeli au redio kinaweza *kutengenezwa* ili kitumiwe tena. Kule *kumlisha vizuri* mtu ndiko *kumfanya awe sawa tena*. Wasemaji wamebuni maana hii kutokana na mazingira yao ya kutumia vifaa kama vile baiskeli na redio kwa wingi. Vifaa ambavyo mara nyingi huharibika na kuhitaji *kutengenezwa* katika mazingira yao. Leksimu *jenga* vilevile inatumwa kwa maana hii mpya katika mfano wa (57) a. Maana wazi za leksimu *jenga* na *tengeneza* zinaoana.

### **3.11 Muundo wa Msamiati**

Ullmann (1970) anasema kuwa hiki huenda kikawa ni kigezo muhimu kinachotawala mabadiliko ya kisemantiki, anaeleza kuwa msamiati huwa na vipashio vingi ambavyo kwavyo, vingine havionekani. Hivyo basi, vipashio vipyta, maneno na hata maana huweza kuongezwa (kwenye msamiati) kwa urahisi huku yale ya awali yakidondoshwa kwa urahisi katika matumizi yake. Aidha anaeleza kwamba, mfumo wa kifonolojia na wa kisarufi wa lugha umeundwa kwa idadi finyu ya elementi zilizopangiliwa kwa pamoja.

Mfano;

- (59) a. Mtu A: We ni mtu wa *kidagaa*.
- b. Mtu B: Mimi si wa *kidagaa*, 'mi ni mzee. *By the way* kuna msichana aliniomba *kidagaa* changu 'paka saa hii hakuwahi 'rudisha.
- c. Mtu A: Unauzaje *kidagaa*?

Katika matamko haya, vipashio vya lugha vimepangwa kwa utaratibu kwa mujibu wa sarufi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika tamko la Mtu A, kuna kiima, kiarifu na kirai nomino kwa usanjari huo. Tatizo hapa ni kwamba, matamko haya hayapitishi ujumbe kwa urahisi kwa kuwa kunatokea utata wa kimawasiliano. Msikilizaji ambaye yuko nje ya diskosi hii atajiuliza; Iweje mtu awe ni mtu wa *kidagaa*? Iweje mtu aombe *kidagaa* tu? Ilivyozoleka ni kwamba, *kidagaa* ni udogo wa *dagaa* ambayo ni aina ya samaki. Katika diskosi hii, maana halisi ya msamiati *dagaa* inadondoshwa na neno hili linachukua maana nydingine ambayo ni aina ya kitabu chenye kichwa *Kidagaa Kimemwozea*. Kitabu hiki ni riwaya ya Kiswahili na ndicho kinachorejelewa katika diskosi hii. Watu walioko kwenye diskosi hii ni wanunuzi kwenye duka la vitabu na wanafanya kukaguakagua vitabu vya kununua. Mtu A anajaribu kumwambia Mtu B kwamba iwapo yeye (mtu B) alisoma riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* akiwa shulenii basi yeye anao umri mdogo. Mtu B anakataa madai ya Mtu A kwa kujitetea. Hapohapo, anakumbuka msichana aliywombwa riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea* akakosa kuirejesha. Msamiati huu ni wa muktadha wa masomoni na unaeleweka vizuri na watu walioko kwenye diskosi hii. Haja ya kutaka kufupisha maneno katika kichwa cha riwaya hii katika mawasiliano, kunafanya maana halisi ya neno *kidagaa*

kudondoshwa na neno hili linachukua maana ya aina ya kitabu katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

Mfano;

- (60) a. Mtu B: *Nilioshwa*. Timu ya Asenali *iliniosha*. Hiyo siku ningekuwa na pesa.
- b. Mtu C: Utaendelea *kuoga* mtu wangu. Wachia sisi haya mambo.
- c. Mtu D: Eeih na wewe (akimwashiria mtu C) *umeiva* sana *betting*. Wikendi pia ulishinda...

Leksimu *osha, oga* na *iva* zinatumwi kwa fahiwa mpya katika muktadha huu. Ingawa vipashio vya kiisimu vimepangwa kiutaratibu katika kauli hizi kwa mujibu wa sarufi ya lugha ya Kiswahili, panaweza kutokea utata katika mawasiliano. Msikilizaji ambaye yuko nje ya diskosi hii atashindwa kuelewa maana za ukingoni za leksimu hizi. Kwa mfano; maana ya neno *osha* katika Kiswahili ni kuondoa uchafu mwilini kwa kutumia maji ila katika tamko la Mtu B, fahiwa ya neno *osha* ni kwamba, *msemaji aliweza kufeliwa katika mchezo wa kamari na timu ya Asenali ambayo ndiyo aliyotarajia imfaulische*, hali ambayo ilimfanya apoteze hela zake. Maana halisi ya neno *iva* ni kupikika kwa chakula hadi kiwango cha kuweza kuliwa. Fahiwa inayoibuka na neno hili katika muktadha wa hapo juu ni *kuwa na ujuzi wa kiwango cha juu zaidi kiasi cha kuweza kuaminika na wengine*. Muundo wa maneno *osha, oga* na *iva* kutumiwa kama misamiati ya lugha ya michezo na lugha ya mitaani unafanya leksimu hizi kupata miktadha mipyä. Ongezeko la miktadha linafanya leksimu *osha, oga*, na *iva* kupata fahiwa mpya mbali na maana zake asilia.

### **3.12 Hitimisho**

Katika sura hii, tulikuwa na lengo la kuelezea sababu za usawazishaji wa maana katika Kiswahili. Tulitumia mitazamo ya Ullmann (1970, 1972) na Palmer (1981) ambayo tuliona ni faafu katika kuainisha sababu za usawazishaji leksimu kwa mujibu wa data yetu. Ilidhihirika kuwa, sababu za usawazishaji maana katika Kiswahili zilikuwa za kiisimu kwa kiasi kikubwa kuliko zilivyo za kijamii. Sababu tulizozielezea ni pamoja na kutokea kisadfa, mahitaji ya maana mpya, maneno ya kisayansi, mwiko, lugha kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, uwazi katika maana, kupotea kwa motisha, upolisemia, mabadiliko kutokea katika miktadha tata na muundo wa msamiati.

Ilionekana kwamba, hakuna mipaka wazi katika kuelezea baadhi ya sababu za mabadiliko ya kisemantiki kwa sababu neno moja lilitokea kuwa limebadilika maana kutokana na sababu moja au zaidi ya moja. Tunakubaliana na mwingiliano huu kwa sababu si rahisi kupata etimolojia au sababu faafu na ya ukweli ya kila neno. Hata hivyo, maelezo yetu yameegemea mifano na aina za maneno na sababu zimeelezwa kwa mujibu wa miitikio ya washiriki katika utafiti huu.

## SURA YA NNE

### ATHARI ZA USAWAZISHAJI WA LEKSIMU

#### **4.1 Utangulizi**

Lengo la sura hii ni kutaka kuchunguza athari zinazotokana na usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili. Maneno yanapotanuliwa maana au yanapobanwa maana athari fulani huweza kutokea katika neno hilo. Neno hupata athari fulani kwa utaratibu katika kipindi fulani cha wakati linapoendelea kutumiwa kwa fahiwa mpya. Tutashughulikia mifano ya maneno ambapo tutachunguza maana ya kawaida ya neno na kuilinganisha na maana mpya ambayo neno hilo limepata kwa sababu ya usawazishaji. Kisha, tutatathmini athari inayotokea kwenye neno hilo baada ya kupata maana mpya. Maneno mengi katika sura hii ni yale yaliyoko kwenye diskosi tulizozichanganua katika sura ya pili na ya tatu. Huenda tusizoneshe diskosi hizo katika sehemu hii. Hata hivyo, muktadha wa matumizi utakuwa muhimu katika kuelezea athari hizi. Tutatumia uainishaji wa Ullmann (1970, 1972) katika kuainisha athari hizi. Ullmann (keshatajwa) anaainisha athari mbili kuu za mabadiliko ya maana katika lugha. Athari hizi ni pamoja na;

1. Badiliko katika mawanda: kupanuka na kubanika kwa maana.
2. Badiliko katika tathmini: msawajikomaana na uemeshajimaana.

#### **4.2 Kupanuka kwa Maana**

Hapa maana ya neno inakuwa ya kijumla zaidi au inayojumuisha vitu vingi zaidi kuliko maana yake awali ya kihistoria kwa sababu ya uhawilishaji wa kisemantiki. Wizani wa neno hivyo basi unaongezeka panapotokea upanuzi wa maana. Mifano,

Neno *Al-shabab* linaonekana kupanuka maana kutoke na hali kwamba, linatumiwa kuzungumzia vitu vingi. Neno hili lina maana wazi ya vijana hasa walio na nguvu katika lugha ya Kiaribu. Kutoke na hali kwamba, kuna kundi haramu linaloitwa *Al-shabab* linalofanya mashambulizi, imetokea kwamba, neno hili linatumiwa kuashiria watu wote wanaoogopewa kwa mashambulizi. Matokeo ya badiliko hili ni kwamba, neno hili linaongezeka wizani kwa sababu vitajwa vyake vinakuwa vingi. Hata hivyo, makusudio ya kupitisha ujumbe ulioimarika zaidi kwa kutumia neno hili yanapungua kwa kuwa halihusishwi tena na kitajwa kimoja. Aidha, maana mpya

ya neno hili haitoi maelezo ya kina ya vitajwa lilivyoongezewa (yaani watu wote wanaosababisha mashambulizi) tukilinganisha na maana yake asilia.

Neno *Shaaban Robert* linatumiwa kumwitia Shaaban Robert aliywahi kuishi pamoja na watu wengine ambao wanakienzi Kiswahili. Kwa kuwa Shaaban Robert alikuwa anajulikana kama baba wa fasihi ya Kiswahili, jina lake linatumiwa katika kuwaitia watu wengine ambao wana sifa kama yake au inayokaribiana na yake. Matokeo ni kwamba, neno hili limeongezewa maana. Matokeo mengine ya upanukaji wa maana ni maana halisi ya neno kuwa legevu hivi kwamba, linaweza kuchukua vitajwa zaidi mbali na kitajwa chake halisi. Athari ya neno kuongezewa vitajwa inakuwa kwamba neno linaongezeka kwa wizani ila makusudio yake yanapungua. Kwa sababu watu wengi wataitwa kwa jina *Shaaban*, almradi wanakienzi Kiswahili, inatokea kwamba, hatuwezi kujuia iwapo msemaji ana kusudi la kumwashiria mtu yupi mahususi ila likitumiwa kwa maana yake ya kihistoria ya Shaaban aliywahi kuishi, makusudio ya msemaji yanakuwa finyu na mahususi na kuelewa ujumbe ulioko kwenye tamko inakuwa pia rahisi.

Neno *mguu* lina maana wazi ya kiungo kinachomwezesha mtu, mnyama au mdudu kusonga. Neno hili limepata fahiwa mbili mpya. Fahiwa ya kwanza ni ile ya kulihuisha neno hili na mwanamke anayetumiwa kimapenzi kisha kuachwa. Fahiwa ya pili ni kuwa neno hili linatumiwa kwa maana ya sehemu ya siri ya mwanamke. Fahiwa hizi zinasababisha neno hili kuongeza wizani kwani linapata vitajwa zaidi –*mwanamke na sehemu ya siri ya mwanamke*. Hata hivyo, maana yake halisi inakuwa legevu kwa kuwa inaashiria vitu vingi.

#### **4.3 Kubanika kwa Maana**

Hali hii hutokea wakati ambapo kuna kupungua kwa wizani wa neno. Maana ya neno huja kupungua kutoka hali jumuishi au kutoka hali ya kujumuisha vitu vingine kuliko ilivyokuwa katika maana yake ya awali ya kihistoria. Mifano;

Neno *kunywa* linaashiria kutia kitu chochote kiowevu mdomoni kisha kukimeza. Neno hili limekuja kuhuishwa na unywaji wa pombe. Kwa mfano, mtu anaposikia kuwa *fulani anakunywa*, jambo la kwanza linalomjia akilini ni *pombe*. Carston (2002) anaeleza kwamba aina nyingine ya ufidiaji ni kwamba, kuliko kuongezea kiambajengo cha kimuktadha, mchakato wa kipragmatiki unalenga faridi fulani ya kileksika na kufanya dhana ambayo faridi hiyo ya kileksika inasimba iwe dhabiti. Ufidiaji unaozungumziwa hapa ndio ubanaji wa maana ya neno kulingana na muktadha.

Kutokana na hali kwamba, vileo vingi huwa viowevu na hunywewa, hivyo basi sifa ya kuhusisha kitendo cha *kunywa* na *ulevi* ikawa ni kawaida. Wasemaji hawakuweza kutafuta neno jingine la kuashiria kitendo hiki bali walilenga leksimu -*nywa* na kubana maana iliyosimbwa na leksimu hii. Matokeo yake ni kupata fahiwa thabiti ya *kunywa pombe tu* tofauti na maana yake iliyosimbwa ya *kunywa kinywaji chochote kile* na ambayo inaonekana kuwa legevu. Vilevile, kutokana na mahitaji ya neno la tasifida la kutajia kitendo cha kulewa, ndipo wasemaji wakabana maana ya neno *kunywa*. Matokeo ya ubanaji huu ni kwamba, neno hili limetoka katika hali ya kuashiria tabia ya kunywa kinywaji chochote kiowevu hadi kwenye mawanda finyu ya kuashiria kunywa kwa pombe pekee. Maana asilia ya neno hili imepungua wizani ila maana hii imetoka kwa hali ya kuwa legevu ya *kunywa kinywaji chochote* hadi hali ya kuwa na nguvu ya kuashiria unywaji wa pombe. Kuongezewa kwa kitajwa *pombe* kwenye maana asilia ya neno hili kunalifanya neno hili liimarike maana yake.

Neno *kijana* lina maana ya kawaida ya mtoto wa kiume au wa kike hadi umri wa kubaleghe. Maana hii ina vitajwa viwili (mtoto wa *kiume* na wa *kike*). Linapitia ubanaji kwa kulihusisha na kitajwa kimoja katika matumizi yake. Athari ni kwamba, neno hili linapungua kwa wizani. *Hata hivyo, maana yake asilia inaimarika* kwani inakuwa mahususi zaidi linapotumiwa kumwitia mtoto wa kiume na kumtenga yule wa kike. Kuimarika huku kunaongezea kusudio la matumizi ya neno *kijana* katika mazungumzo ya kila siku. Msemaji anaelewa kwamba, mtu fulani anapomhitaji *kijana* fulani, anakuwa na kusudio mahususi la kuashiria mtoto wa jinsia ya kiume wala si wa jinsia ya kike. Athari ya kulihusisha neno *kijana* na jinsia ya kiume pekee huenda inatokana na baadhi ya lugha za kwanza za wasemaji ambapo, wanapolitafsiri neno *kijana* kutoka Kiswahili na kulitumia kama /kija:na/ au /ikija:na/ katika Lulogooli au Lunyore, linaashiria mtoto wa kiume pekee awe aliyebaleghe au asiyebaleghe. Kuna uwezekano kuwa msemaji alipoanza kutumia lugha yake ya kwanza tayari alipata wasemaji wengine wakibana maana ya neno hili naye akaendelea kulibana hivyo katika Kiswahili.

#### **4.4 Msawajikomaana**

Massamba (2004) anaeleza msawajikomaana kuwa ni hali ya maana ya neno kubadilika kutoka maana nzuri na kuelekea kuwa na maana mbaya. Tunaongezea kwamba, kutokana na uhawilishaji wa maana katika neno, maana ya neno inaweza kubadilika na kuwa hasi zaidi katika matumizi yake. Hii inatokana na kupotea/kupungua kwa thamani ya maana ya neno hilo. Mifano;

Maneno mengi yanapata maana hasi kutokana na hali kwamba yanatumiwa katika nafasi ya maneno ya mwiko. Mifano ya maneno haya ni *sugua*, *mguu*, *kengele* na *shoga*. Maneno haya ni yale yanayochukua nafasi ya neno la mwiko katika jamii. Yanapochukua nafasi ya neno la mwiko yanatumiwa kama maneno ya tasifida. Kutokana na hali hii, maneno haya basi yanabadilika hatua kwa hatua na kupata maana hasi.

Maana wazi ya *sugua* ni kupidisha kitu juu ya kitu kingine kwa kurudiarudia kwa nguvu kwa madhumuni ya kuondoa alama au uchafu ulioko TUKI (2013). Maana hii ni chanya na ya kijumla hivi kwamba, inaashiria *kupidisha kitu chochote kile juu ya kingine*. Kutokana na hali ya kutafuta neno la tasifida la kutajia tendo la ndoa, wasemaji wanatumia kitenzi *sugua* kuashiria kitendo hiki. Inatokea kwamba, tabia ya kushiriki tendo la ndoa ni *kusuguana*. Maana ya kawaida ya neno hili inabadilika kutoka kwa maana chanya ya kusugua kitu chochote kile hadi kwenye maana hasi ya kuashiria hali ya kushiriki tendo la ndoa. Athari yake ni kushuka kwa hadhi ya neno hili.

Leksimu *Mombasa* inapotumiwa kama kirai: *Mombasa raha*, inapata maana hasi. Maana wazi ya *Mombasa* kuwa ni mji unaojulikana kwa historia ya Kiswahili inabadilika na kuchukuliwa kuwa mji wa raha. Wala si raha tu bali raha inayorejelewa ni hali fulani isiyoelezeka ya mtu kujihisi vizuri wakati wa tendo la ndoa ndipo wasemaji wakabuni kirai *Mombasa raha*. Muktadha kwamba, mji wa Mombasa ni kisiwa kilichozungukwa na maji matamu ya bahari ya kuogelea, unawafanya wasemaji kulihusisha neno hili na maana hii mpya. Ikawa sasa kushiriki tendo la ndoa ni kama kufurahia mawimbi ya maji mtu anapoogelea baharini Mombasa. Aidha, kutokana na kasumba kwamba, mji huu unachukuliwa kuwa wa watalii au wa watu kubarizi wala hakuna kufanya kazi, ndipo wasemaji wakahuishsa neno hili na maana ya *Mombasa raha*. Matokeo ni neno hili kupata maana hasi ambayo ni dhahania hivyo basi linashuka hadhi.

Neno *chomelea* linatokana na kitendo *choma*. Kuchoma ni kuteketeza kitu kwa moto. Kitendo cha kuchoma kinaonekana kuwa chanya kwa kiasi kikubwa. Neno hili linapohusishwa na maana mpya ya *chomelea* kuwa ni mtu anayevikarabati vyombo vya plastiki kwa kuzurura na moto wa makaa mkebeni huku akiradidi neno *chomelea* kwa sauti, maana yake inashuka hadhi. Tena maana yake asilia inashuka kutoka maana dhahania ya kuashiria kitendo cha kuchoma hadi maana ya mguso ya kuashiria mtu anayetekeleza kitendo hicho. Maana mpya ya neno *choma* ni hasi kwa sababu watu wanaofanya kazi hii wanahuishwa na tabaka la masikini katika jamii.

Neno *shoga* lina maana mbili za kileksika 1. Rafiki wa kike wa mwanamke, 2. Mwanamume anayefirwa TUKI (2013). Wasemaji wengi wanaifahamu maana ya pili ya neno hili. Hali hii imefanya maana ya kwanza ya neno hili kutotumiwa sana. Hata hivyo kwa ujumla, neno hili halitumiwi sana kwa maana zote mbili kwa sababu ya mazoea ya kulihusisha neno hili na maana ya pili. Hali hii inafanya maana ya kwanza ya neno hili ambayo ni chanya kusahaulika au kufa katika matumizi yake huku maana ya pili ambayo ni hasi ikikosa motisha katika matumizi kwa sababu ni mwiko kuzungumzia au kutenda kitendo cha ushoga. Kutokana na utata wa kileksika uliopo kwenye neno hili, msikilizaji anaposikia neno *shoga*, kinachomjia akilini ni mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwenzake wala si ile maana ya rafike wa kike wa mwanamke. Neno hili limepata athari hasi kikamilifu katika matumizi yake kwani halitumiwi tena na wanawake marafiki kuitania katika maeneo yetu ya utafiti.

Neno *kijana* lina maana wazi ya mtu ambaye si mzee wala si mtoto. Neno *kijana* limepata maana hasi linapotumiwa kumwitia mtoto wa kike aliyebaleghe. Hii ni kutokana na mazoea ya kulihusisha neno hili na watoto wa kiume pekee. Mara nyingine wasichana wanapoashiriwa kwa kutumia neno hili, wao huchukulia kama kwamba wanadhalilishwa kwa kuwekwa katika kategoria ya wanaume. Kutumia hili neno kumwitia msichana ni kama kwamba, unampa sifa ya kuwa mwanamume ambayo kulingana na yeche ni sifa hasi.

#### **4.5 Uemeshajimaana**

TUKI (1990) wanaeleza kwamba, uemeshajimaana ni ubadilikaji taratibu wa maana ya neno na kupata maana nzuri zaidi. Tukipanua maelezo haya tunaongezea kwamba, hadhi ya maana ya neno katika badiliko hili inapanda, hivi kwamba, maana ya neno inakuwa chanya zaidi kuliko ilivyokuwa awali. Fauka ya hayo, kuna ule uemeshajimaana uliokamilifu ambapo maana ya neno inabadilika kikamilifu kutoka maana hasi hadi maana chanya na ule uemeshajimaana usiokamilifu ambapo maana ya neno inabadilika na kuwa chanya kwa kiasi kidogo tu. Mifano;

Neno *gonga* limepata maana mpya ambayo ni chanya kwa kiasi fulani. Maana wazi ya neno *gonga* ni kukutanisha kitu kimoja na kingine kwa kuvipiganisha. Maana hii inaonekana kuwa hasi neno hili linapotumiwa katika muktadha wa kumgonga mtu kwani anapogongwa huhisi uchungu. Hata hivyo, maana mpya inayoongezewa neno hili ya kumpunja mtu bidhaa au pesa kwa njia ya ujanja asiyoweza kugundua kwa urahisi inakuwa chanya zaidi kuliko ile hali ya kumgonga mtu kiuhalisia. Neno hili halibadiliki maana yake asilia kikamilifu ikawa chanya ila kwa kiasi fulani

inapata maana chanya tukilinganisha na maana yake asilia. Aidha, neno hili linapobadilika kutoka maana hasi hadi maana chanya, maana chanya inayoibuka inakuwa ya kidhahania kuliko maana yake halisi (kukutanisha vitu kwa kuvipiganisha) ilivyokuwa.

Neno *iva* hutumiwa kuashiria kupikika kwa kitu, kukomaa kwa kitu au kuiva kwa tunda. Maana ya iva inaonekana kuwa hasi kwa kiasi fulani kwa kuwa inahusishwa na mapishi. Neno hili limepata fahiwa mpya ya kurejelea ile hali ambayo mtu fulani amefikia upeo wa juu wa kuaminika katika kutekeleza jambo fulani. Maana hii ya ukingoni ya neno *iva* imejitenga zaidi kutoka kwa maana halisi ya kukomaa kwa kitu au kupikika kwa kitu. Matokeo ni maana ya mtu *kuaminika katika ujuzi fulani* ambayo ni chanya kikamilifu. Hivyo basi pametokea maana kubadilika kikamilifu kutoka maana hasi hadi maana chanya.

Neno *rusha* lina maana wazi ya kutuma kitu upande wa pili hasa kwa kutumia nguvu. Kitu kinaporushwa huenda kwa nguvu hivi kwamba kinaweza kusababisha madhara. Neno *rusha* linapotumiwa kwa maana ya kutuma pesa kupidia huduma ya simu linapata maana chanya. Maana chanya ambayo neno hili linapata inakuwa nzuri kikamilifu hivi kwamba, inahusishwa na kutuma pesa wala si kurushwa kwa kitu kinachoweza kuleta madhara kama vile jiwe. Tunadai kuwa neno hili limepitia uemeshajimaana uliokamilifu kwani limepanda hadhi kutoka kwa hali ya kurusha kitu chochote kile kinachoweza kuleta madhara, hadi kwenye hali ya kuhawilisha pesa kutoka kwa mhudumu mmoja hadi mwingine kupidia njia ya simu. Hata hivyo, maana inayoibuka (ya kutuma pesa kupidia huduma ya simu) ni ya kidhahania.

Vitenzi *-pa* na *-leta* mionganoni mwa vitenzi vingine vingi vinaonekana kuwa vya kuamrisha katika Kiswahili. Kutohana na mazoea ya kuongezea kiambishi tamati {-ko} cha uemeshajimaana katika vitenzi hivi, vitenzi hivi vinapata fahiwa mpya ambayo inaonekana kuwa chanya. Maana mpya inayojitokeza inakuwa ya kuamrisha kwa njia ya upole kuliko ilivyokuwa ya kuamrisha hapo awali. Maneno haya yanapoongezewa hiki kiambishi yanajitokeza na muundo huu; *nipatie-{ko}*, *leta-{ko}*. Muundo huu unaonekana kuwa wa kuamrisha ila kwa njia ya upole. Kiambishi tamati {-ko} kinapoongezwa kwenye vitenzi, kinapunguza makali ya maana halisi ya neno kutoka hali ya kuonekana kuamrisha na kuifanya maana yake kupidisha fahiwa ya upole ambayo ni chanya. Habwe n.w. (2010) wanaeleza kwamba, lugha za kiafrika huwa na mfumo mpana wa kuonyesha unyenyekevu/adabu. Hii ni kwa sababu utamaduni wa kiafrika unasisitiza hayo. Mofimu tamati {-ko} inayoongezewa kwenye vitenzi hivi inatokana na mofimu {-ku} na {-kho} za lugha za kwanza

kama vile Lulogooli na Lunyore ila mofimu hizi zinafanyiwa mageuzi na kujitokeza kama {-ko} katika Kiswahili. Hali hii inatokana na hali kwamba, katika jamii za maeneo yetu ya utafiti, wasemaji wamezoea kuonesha adabu wanapajaribu kuomba kitu kutoka kwa mtu mwingine.

#### **4.6 Kupanuka Maana na Kubanika Maana Mtawalia**

Tukizingatia athari za mabadiliko ya maana za Ullmann (keshatajwa) tunaweza kuongezea kuwa, yapo maneno mengine ambayo yamepitia mabadiliko ya maana kuwili. Maneno mengine yamepanuka maana na yakabanika maana kulingana na muktadha wa matumizi.

Neno *chai* limepanuka na kubanika maana kulingana na miktadha ya matumizi. Chai ni *ni kinywaji kinachoandaliwa kwa maziwa au maji yaliyochemshwa na majani ya mchai*. Neno hili limeongeza maana na kushirikisha vinywaji vingine. Pyles na Algeo (1964) wanaeleza kwamba, wakati tunapoongeza mawanda ya neno, tunapunguza idadi ya sifa katika maelezo ya maana ya neno hilo ambazo hudhibiti matumizi ya neno hilo. Ni wazi kwamba, dhana ya kisemantiki iliyosimbwa na neno chai ni finyu kwani inaashiria kitu kimoja kwamba *chai ni kinywaji kinachoandaliwa kwa maziwa au maji yaliyochemshwa na majani ya mchai*. Sifa kuu inayoitambulisha kinywaji chai ni *kuandaliwa kwa majani ya mchai*. Sifa hii ndiyo inayodhibiti au kufanya maana ya *chai* kuashiria aina ya kinywaji kimoja. Wasemaji wanavuruga maana ya kisemantiki ya neno *chai* bila kutarajia kwa kudondosha sifa ya *kuandaliwa kwa majani ya mchai*. Sifa hii inapodondoshwa, tunapata maana ya neno *chai* kuwa: *ni kinywaji kinachoandaliwa kwa maziwa au maji yaliyochemshwa*. Maana hii inaonekana kuwa legevu ndipo wasemaji wanaongezea vitajwa vingine kama vile kahawa na chokoleti kwenye maana hii legevu kwa urahisi. Msemaji anaposema kuwa *amekunywa chai*, anaweza kuwa anamaanisha kinywaji cha kahawa au chokoleti. Athari inayotokea ni kwamba, neno *chai* linaongezeka kwa wizani na mawanda yake ya kisemantiki yanapanuka. Yaani, neno hili linapata vitajwa zaidi (kahawa, chokoleti) ambavyo vinaongeza wizani wake na kulifanya litumike katika muktadha zaidi ya mmoja. Hata hivyo, kusudio la kutumia neno hili linapungua kwa kuwa linatumia kuashiria vitu vingi kuliko lilivyokuwa likiashiria kitu kimoja mahususi.

Kwingineko, leksimu *chai* imebanika maana. Kinywaji *chai* huweza kutengenezwa kwa majani ya mchai kwa kutumia maziwa au maji. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu, chai ni lazima itiwe maziwa na majani ndipo ipate *kibali* cha kuitwa *chai*. Kwa kuihusisha maana ya neno *chai* na sifa ya kuwa ni lazima iwe na maziwa, sifa hii inaidhibiti maana wazi ya neno *chai* hivi kwamba,

neno hili linaashiria kinywaji cha aina moja –*kilichotiwa maziwa na majani*. Kinywaji kilichoandaliwa kwa maji na majani bila kutiwa maziwa kinafungiwa nje ya maana hii. Maana ya neno hili inaimarika hivi kwamba inatoa maelezo ya kina kuhusu kitajwa kinachorejelewa kuliko ilivyokuwa katika upanuzi ambapo maelezo ya kitajwa cha neno hili yalipungua kwa kuvishirikisha vitajwa vingine. Neno hili linapunguka wizani kwa sababu, ile sifa ya kuwa chai huweza kupikwa kwa maji inadondoshwa na kuhusisha chai na *maziwa pekee*.

Neno *ndugu* limepanuka maana halkadhalika limebanika maana. Maana ya kawaida ya neno *ndugu* ni mtu aliyezaliwa nawe kwa baba, kwa mama au kwa wazazi wote wawili. Katika kupanuka maana, sifa za kuwa *ndugu huzaliwa nawe kwa baba, kwa mama au kwa wazazi wote zinadondoshwa* na kubakia na maana legevu ya *ndugu ni mtu*. Athari za kudondosha sifa hizi ni mbili na changamani. Baada ya kudondosha sifa hizi, maana ya neno *ndugu* inaonekana kuwa pana kisemantiki hivi kwamba, wasemaji wanaongezea vitajwa vingine kwenye maana ya neno hili bila kutarajia. Wanapofanya hivi, *ndugu* linatumwiwa kuashiria mtu yelete mbali na yule mliyezaliwa naye. Kutokana na hali hii, hatuna budi kukubaliana na maoni ya Habwe n.w. (2010) wanaposema kwamba, katika jamii za kiafrika ndugu ni mtu wa nasaba yako. Kwa hivyo hii maana legevu ya *ndugu ni mtu* inapanuka kwa kuwa kuna kudondosha sifa nyininge za maana iliyosimbwa na neno *ndugu* kisha kuongezea viashiriwa vingine kwenye maana hiyo ambavyo vinajumuisha watu wa nasaba moja. Hali hii inafanya wizani wa neno *ndugu* kuongezeka na kusudio lake katika mawasiliano kupungua.

Aidha, neno *ndugu* limebanika maana kwa kutumiwa kuashiria wanaume na kuwatenga wale wa kike. Tunapotengwa wale wa jinsia ya kike, neno *ndugu* linapata maana hii iliyobanika: *ndugu ni mwanamume mliyezaliwa naye kwa baba au kwa mama au kwa wazazi wote wawili*. Maana hii inaongezea sifa ya *ndugu* kuwa mtu wa jinsia ya kiume na kuwafungia nje wale wa jinsia ya kike. Uchangamani unatokea pia kwa kuipanua hii maana mpya inayoibuka na kupata maana hii hapa: *ndugu ni mwanamume yelete* katika matumizi yake. Hii maana inayoibuka inakuwa pana na pia finyu hivi kwamba, ingawa maana hii inaongezewa vitajwa vingine ambapo ndugu anakuwa si yule wa *kiume mliyezaliwa naye* tu bali pia *wanaume wengine wote*, inamfungia nje yule *ndugu wa kike*. Hali ya kulihusisha neno hili na jinsia ya kiume inatokana na neno *indugu* ambalo ni neno mkopo la Lulogooli kutoka kwa neno hili la Kiswahili *ndugu*. *Indugu* hivyo basi linapotumiwa katika Lulogooli linatumwiwa tu katika kuashiria watu wa jinsia ya kiume. Athari hii inahamishwa

hadi Kiswahili na kulifanya neno *ndugu* kuashiria mwanamume katika matumizi ya Kiswahili. Matokeo ni kuwili na yanaelezwa hivi, kwa kuwafungia wale *ndugu wa kike* nje, leksimu hii inapungua wizani wake na kusudio lake linaimarika. Kwa kuitumia katika kuashiria *wanaume wote*, wizani wake unaongezeka kwa sababu ya ongezeko la vitajwa katika maana yake iliyosimbwa ila kusudio lake linapungua.

Katika miktadha mingine, neno *ndugu* linatumwa kwa hali tofauti. Katika muktadha wa kanisani, neno *ndugu* linapanuka maana kwa kutumiwa na waumini wote kuitania. Hii inatokana na Biblia ambacho ni kitabu kitakatifu kwa wakristo kutumia neno la Kiingereza *brethren* kwa kuashiria wana wa Mungu. Tafsiri ya *brethren* hadi Kiswahili ni *ndugu* na linatumwa kwa maana hiyo iliyotajwa. Katika hali hii, neno hili limepanuka maana. Tukichunguza katika muktadha wa kisiasa, neno *ndugu* vilevile limepanuka maana linapotafsiriwa kihafifu kutoka neno *comrade* la Kiingereza. Linapotumiwa katika siasa, linaashiria wale watu walio na msimamo mmoja kisiasa.

Katika matumizi mengine ya neno hili, inaonekana kwamba, limebanika maana kuwili. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu ni kwamba, matumizi ya kwanza ni yale ambayo *ndugu* linatumwa na wanaume waliozaliwa na mzazi au wazazi wamoja kuitania. Matumizi ya pili ni kwamba, *ndugu* linatumwa na watoto wa kike waliozaliwa na mzazi au wazazi wamoja kuitania. Maana iliyosimbwa na neno hili imebanika kulingana na miktadha hii miwili hivi kwamba, watu wa jinsia moja tu ndio wanaoweza kuitana *ndugu*. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu ni kwamba, dada hawezi kumwita kakake *ndugu* na kaka hawezi kumwita dadake *ndugu*. Habwe n.w. (2010) wanaeleza kuwa, kila utamaduni huwa na dhana tofauti kuhusu, kwa mfano, nani baba, *ndugu*, ami, mume na kadhalika. Katika maeneo yetu ya utafiti, wasemaji wanayo majina yote kutoka lajaja zao ya kutofautisha kati ya mtu mliyezaliwa naye wa jinsia ya kike na yule wa jinsia ya kiume. Kutokana na mazoea yao ya kufanya utofauti wa kijinsia, inaonekana ni vigumu sana hasa kwa wanaume kutumia jina moja *ndugu* katika kuashiria jinsia zote katika Kiswahili. Tena, kwa sababu huenda wasemaji hawajui au hawajazoea kuyatumia majina kaka na dada ya Kiswahili yanayoweza kutumiwa kutofautisha jinsia, wao wanalitumia neno hili moja *ndugu* kuwili, kila jinsia ikilitumia kivyake. Matokeo ni neno *ndugu* kubanika maana kuwili na pia kunaweza kutokea utata wa kimawasiliano hasa kwa msemajji ambaye haelewi utamaduni wa jamii fulani.

#### **4.7 Msawajikomaana na Uemeshajimaana Mtawalia**

Tunajenga maelezo yetu kutoka kwa maelezo ya Ullmann (1972) kuhusu msawajikomaana na uemeshajimaana kwa kuongezea kwamba, yapo maneno mengine ambayo yanaweza kupata maana mbaya katika muktadha mmoja na yakapata maana chanya katika muktadha mwininge. Mifano;

Neno *tengeneza* limepata maana chanya na hasi vilevile. *Kutengeneza* ni kufanya au kurekebisha kitu kilichokuwa kimeharibika ili kifae tena. Maana hii inabadilika na kuwa chanya wakati ambapo hali ya *kutengeneza* inaashiria *kulishwa kwa vinono* au *kupewa msaada wa chakula* au *kulishwa kwa vinono ambavyo* mtu *hajawahi kuvila kabla* au *amechukua muda mrefu tangu kuvila*. Hali ya kutengeneza kitu chochote kile kinachoweza kuharibika kama vile baisedeli au redio inaonekana kuwa hasi kwa kiasi fulani. Maana ya *kutengenezwa* inapohawilishwa hadi kwa fahiwa mpya ya *kulishwa kwa vinono* inakuwa chanya tukilinganisha na maana wazi ya neno hili kabla ya badiliko. Maana hii imeibuka kutokana na wasemaji kutumia vifaa fulani kama vile baisedeli au redio kwa wingi, na vinapoharibika huhitaji kurekebishwa. Mtu anaposikia njaa huwa ni kama baisedeli au redio iliyoharibika na sasa anahitaji kufanywa upya au *kutengenezwa* ili afae tena katika matumizi. *Kulishwa vizuri* hivyo basi kunahuishwa na kutengenezwa. Thamani ya neno hili inapanda kihadhi kutoka kwa hali ya *kuunda kifaa chochote kile* hadi kwa hali ya *kumlisha mtu vinono*.

Aidha, neno *tengeneza* limepata maana hasi kikamilifu. Fahiwa mpya ya kumpiga mtu kiasi cha kwamba anayetoa kipigo kile aridhike kwamba amemwumiza anayepigwa ni kinyume cha kutengeneza au kurekebisha kitu kilichoharibika. Mtu anapopigwa huwa harekebishiwi mwili wake ili afae tena ila huwa *anaharibiwa*. Maana wazi ya neno *tengeneza* imeshushwa hadhi na kuashiria hali ya *kuharibu* ambayo ni tofauti na hali yake chanya ya *kufanya upya kitu kilichoharibika ili kifae tena*. Athari hizi zinatokana na lugha za kwanza za wasemaji. Wasemaji wanapofanya ubunaji wa leksimu wanafanya tafsiri sisisi ya maneno kutoka lugha zao za kwanza hadi lugha ya Kiswahili. Matokeo ni kuongezeka kwa maana mpya katika maneno ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, maana hizi mpya za neno *tengeneza* zimetokana na tafsiri ya moja kwa moja ya leksimu *romba* na *lomba* kutoka Lulogooli na Lunyore mtawalia na zenye fahiwa mpya za *kufanya kitu kifae tena* au *kulishwa vizuri*.

Neno *kondoo* lina maana wazi ya mnyama mpole. Neno hili linapotumiwa katika muktadha wa kanisani linapata maana chanya ya kuashiria muumini wa dini ya kikristo. Mfano wa mstari;

kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata (Yohana Mtakatifu 10: 27). Hapa neno *kondoo* limetumiwa kuashiria wakristo wanyenyeketu kama kondoo na wanaofuata njia za Mungu. Pia neno hili linatumwiwa kuashiria Yesu Kristo linapotumiwa kama neno ambatani; *mwanakondoo*. Mfano wa nukuu kutoka Biblia; siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, tazama, mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu (Yohana Mtakatifu 1:29). Yesu Kristo anaaminika kwamba, alikufa kikondoo kwa ajili ya dhambi za watu. Yaani alitolewa kafara namna kondoo anavyotolewa kafara. Kutokana na asili hii ya Biblia, neno *kondoo* linatumwiwa katika kanisa na sehemu za ibada kuashiria wakristo. Maana iliyosimbwa na neno *kondoo* inapanda hadhi kutoka kuashiria kondoo mnyama hadi kwa kuashiria kondoo binadamu na si binadamu tu bali muumini wa dini anayefuata njia za Mungu.

Aidha, neno *kondoo* limepata maana hasi linapotumiwa katika muktadha wa kumrejelea mtu mjinga. Kutokana na hali kwamba, mnyama kondoo huchukuliwa kuwa mnyama mjinga, ndipo wasemaji wakahusisha maana ya neno hili na mtu mjinga. Matokeo ni kwamba, neno hili linapata maana hasi kikamilifu ya kuashiria mtu mjinga na hadhi yake inashuka. Hii maana hasi inaonekana kutumiwa sana katika mazingira ya shulen iambapo mwanafunzi anaweza kuitwa *kondoo* kwa maana kwamba yeye (mwanafunzi) ni mjinga.

#### **4.8 Hitimisho**

Katika sura hii tumeelezea athari zinazotokea kwenye maneno kutokana na hali kwamba maneno hutumiwa kwa maana tofauti kulingana na muktadha. Athari tulizozishugulikia ni pamoja na kupanuka kwa maana, kubanika kwa maana, msawajikomaana na uemeshajimaana. Katika kuchunguza athari hizi katika maneno yetu, tuligundua kuwa, yapo maneno ambayo mbali na kupanuka maana, pia yamebanika maana. Aidha, kulikuwako na maneno mengine ambayo mbali na maana yake kubadilika na kuwa hasi, maana yake pia ilibadilika na kuwa chanya. Pia tuligundua kwamba, maneno mengine yanapopitia msawajikomaana au uemeshajimaana, maana inayoibuka ama ni dhahania au ni ya mguso tukilinganisha na maana yake asilia. Muktadha wa matumizi wa maneno haya ulionekana kuwa wa muhimu katika kusababisha athari hizi za mabadiliko ya maana za maneno.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO**

#### **5.1 Utangulizi**

Katika utafiti huu, tulikuwa na lengo la kuthibitisha kuwa usawazishaji wa leksimu unatokea katika Kiswahili. Ilidhihirika kwamba, usawazishaji wa leksimu unatokea katika Kiswahili na michakato miwili (upanuzi na ubanaji wa maana) ndiyo inayohusika. Tumeelezea haya mabadiliko ya maana kwa mifano ya matamko ambayo tulikusanya katika kaunti ya Vihiga, Kenya.

Katika utafiti huu, tuliongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika ambayo ilitufaa sana katika kuchanganua data yetu. Nadharia hii vilevile ilitumiwa katika kuainisha aina za mabadiliko ya maana. Ilidhihirika kwamba, Nadharia ya Pragmatiki Leksika inaweza kutumiwa katika kuainisha aina za mabadiliko ya maana katika Kiswahili. Kwa ujumla, nadharia hii inafaa sana katika kuelezea mabadiliko ya maana yanayotokea katika leksimu za Kiswahili.

#### **5.2 Matokeo ya Utafiti Huu**

Leksimu za Kiswahili zimepitia usawazishaji wa maana na zimepata miktadha mipyä ya matumizi kutokana na michakato ya upanuzi na ubanaji wa maana. Michakato hii ndiyo iliyosababisha leksimu hizi kupata fahiwa mipyä. Kutokana na mabadiliko haya, yafuatayo yalijitokeza katika hali ya mawasiliano kati ya msemaji na msikilizaji:

- i. Maarifa ya kiusuli ni ya muhimu katika kufasiri ujumbe ulioko kwenye tamko. Maarifa haya ya kiusuli yanawakilishwa na dhana ambazo zimehifadhiwa akilini na yanafaa kuwa sawa kati ya msemaji na msikilizaji ili kuwawezesha (msemaji na msikilizaji) kufikia uhusiano.
- ii. Dhana za dharura ziliundwa na msikilizaji katika mkondo wa kuelewa ujumbe unaowasilishwa kwenye kauli. Uundaji huu wa dhana za dharura ulitegemea sana vitomeo vya maarifa ya ufahamu vya msikilizaji pamoja na mazingira ambayo msikilizaji ametangamana au anatangamana nayo.
- iii. Maneno yote tuliyoyashughulikia hayakupoteza maana zake za kileksika bali maana hizi zilisawazishwa au kufanyiwa mageuzi kulingana na muktadha na kupata fahiwa mipyä. Mageuzi ya maana hizi yalisababishwa sana na mahitaji na haja ya kutaka kuitisha ujumbe fulani na wasemaji lugha.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo;

- i. Aina za usawazishaji wa leksimu kama vile ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kileksika, upanuzi wa kisitiari, chuku, kisio la maana, upanuzi wa kategoria na ubunaji wa maana mpya zinatokea katika Kiswahili.
- ii. Sababu zinazopelekea mabadiliko ya maana za leksimu katika Kiswahili ni za kiisimu na zinatokana na mawasiliano katika muktadha.
- iii. Mabadiliko ya maana ya leksimu yanababisha kuvunjika kwa mawasiliano mionganini mwa wazungumzaji.

Kutokana na nadharia tete hizi ilidhihirika kwamba;

- i. Aina zote za mabadiliko ya maana zilizotajwa zinatokea katika Kiswahili na zinaweza kuelezwu kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kama ilivyo katika nadharia hii, aina mbili kuu za mabadiliko ya maana zilijitokeza nazo ni ubanaji wa maana na upanuzi wa maana. Upanuzi wa maana ulijumuisha aina nyingine za mabadiliko ya maana ambazo ni: upanuzi wa kisitiari, chuku, kisio la maana, upanuzi wa kategoria na ubunaji wa maana mpya na uundaji wa kileksimu.
- ii. Iltokea kwamba, sababu za mabadiliko ya maana katika leksimu za Kiswahili ziliwuza za kiisimu. Sababu hizi ziliibuka kutokana na miktadha ya matumizi ya maneno hayo. Sababu ambazo tulizilishughulikia ni pamoja na; kutokea kisadfa, mahitaji ya maana mpya, maneno ya kisayansi, mwiko, lugha kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, uvulivuli wa maana au ukosefu wa uwazi katika maana, kupotea kwa motisha, upolisemia, miktadha tata na muundo wa msamiati.
- iii. Kwa mujibu wa washiriki katika utafiti huu ni kwamba, mara nyingine kulitokea kudhoofika au kupotea kwa mawasiliano mionganini mwao kwa sababu ya mabadiliko ya maana za maneno na kuzuka kwa miktadha mpya ambayo kwa kiasi fulani hawakuwa wameizoea. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa kulitokea kudhoofika kwa mawasiliano jumbe zilipopitishwa kutoka kwa mse maji mmoja hadi mwengine au wengine.

### **5.3 Mapendekezo**

Katika utafiti huu tulishughulikia mabadiliko ya maana za maneno ila maana halisi za maneno haya bado zinadumu katika lugha. Tulishughulikia namna mabadiliko ya maana za maneno

yanatokea katika miktadha ya matumizi. Katika lugha yoyote ile, maana za kileksika zinaweza kubadilika kwa njia tatu; maana inaweza kupitia upanuzi, ubanaji au uhawilishaji. Uhawilishaji unatokea wakati ambapo maana halisi ya neno chanzi inahawilishwa kutoka kwenye neno hilo hadi kwenye neno jingine (neno lengwa). Matokea ni kupotea kwa maana asilia ya neno chanzi. Huenda maneno mengine yapo ambayo maana zake asilia zimepotea kabisa na kamwe hayatumwi katika Kiswahili. Tunapendekeza utafiti mwingine uweze kufanywa ili kuchunguza iwapo kuna mabadiliko mengine ya maana yanayoweza kuwa yametokea katika Kiswahili na yakasababisha kupotea kwa maana za maneno kikamilifu katika matumizi yake.

Aidha, katika utafiti huu, tulijifunga katika usawazishaji wa maana za maneno kulingana na muktadha wa matumizi. Hatukushughulikia etimolojia ya kale ya maneno haya ambayo inaweza kupeana msingi bora wa mabadiliko ya maana kulingana na vipindi mbalimbali vyta wakati. Tunapendekeza utafiti mwingine ufanywe ili kuchunguza mabadiliko ya kidaikronia yanayoweza kuwa yametokea katika leksimu za Kiswahili.

Utafiti huu umefanyika katika eneo moja na katika Kiswahili sanifu. Lugha ya Kiswahili ni lingua franka ya Afrika Mashariki na lugha hii ina lahaja nyingi, tunapendekeza kwamba, utafiti kama huu uweze kurudiwa katika eneo jingine ambamo lugha ya Kiswahili inatumwa ili kuthibitisha iwapo usawazishaji wa leksimu unatokea kwa kiwango cha juu na kwa mawanda mapana katika matumizi ya Kiswahili. Aidha, tunapendekeza utafiti mwingine ufanywe ili kuchunguza mabadiliko ya kisemantiki katika lahaja za Kiswahili kulingana na muktadha.

Katika utafiti huu, imedhihirika kwamba, usawazishaji wa maana za maneno ulisababishwa kwa kiasi fulani na athari za lugha za kwanza kwa Kiswahili. Mifano iliyojitokeza ni ukopaji sisisi wa maana za maneno kutoka lugha za kwanza hadi lugha ya Kiswahili. Pia kulitokea unyambuaji wa maneno ya Kiswahili ambapo unyambuaji huu ultokana na athari za lugha za kwanza. Matokeo yalikuwa ni kubadilika kwa maana asilia ya neno la Kiswahili. Tunapendekeza kwamba, utafiti wa kiulinganishi ukafanywe ili kuchunguza jinsi lugha za kwanza zinavyoathiri maana za maneno ya Kiswahili na jinsi maana za maneno ya Kiswahili zinavyoathiri maana za maneno ya lugha za kwanza. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lingua franka ya Afrika Mashariki na ni lugha jirani na lugha nyingi za kwanza.

Kwa muhtasari, kudhoofika au kupotea kwa mawasiliano katika Kiswahili kuliweza kusababishwa na mabadiliko katika maana za maneno. Miktadha mipyä ambamo maneno haya yalitokea ndiyo iliyosababisha kudhoofika kwa mawasiliano. Pia maana mipyä za maneno ziliathiri miktadha ambayo tayari ilikuwa imezoleka. Fauka ya hayo, ilidhihirika kwamba, maneno mengi tuliyoyashughulikia yaliweza kupata maana mipyä mbali na maana zake halisi. Wasemaji walifanya upanuaji maana chapwa wa maneno mengi na matokeo yalikuwa kwamba, neno lilipata fahiwa moja mipyä au zaidi. Neno linapoongezewa maana, huwa kunatokea utata wa kileksika katika neno hilo na katika sentensi ambamo neno hilo linatokea. Tumetangulia kutaja kwamba, mabadiliko ya maana katika Kiswahili yaliweza kuelezwu ifaavyo kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kutokana na mabadiliko haya, ilimlazimu msikilizaji kufanya mchakato wa ubanaji au upanuzi ili aweze kufikia dhana inayowasilishwa kwenye tamko. Alifanya hivi kwa kusawazisha ujumbe, muktadha na athari za kimawazo, mchakato ambaa ulimwezesha kufikia uhusiano.

Aina kuu za mabadiliko ya maana zinazoibuka katika leksimu za Kiswahili ni upanuzi na ubanaji wa leksimu. Maana halisi ya neno inakuwa pana katika upanuzi na kuongezewa mawanda ya kisemantiki ili ikaweze kujumuisha hali au viashiriwa vingine zaidi. Jambo hili liliababishwa na kupanuka kwa miktadha ya matumizi ya neno hilo. Katika ubanaji, maana ya neno inakuwa finyu ili ikaweza kuashiria hali au vitu vichache zaidi kuliko maana iliyosimbwa na neno hilo. Hata hivyo, mchakato wa kiakili wa ubanaji uliweza kutokea katika ubanaji na upanuzi wakati ambapo msikilizaji anajaribu kutafuta uhusiano kutegemea muktadha wa matumizi.

Sababu za mabadiliko ya maana katika Kiswahili ni za aina nyingi na ni za kiisimu kwa kiasi kikubwa. Maneno yanabadilika maana katika Kiswahili kulingana na muktadha wa matumizi. Maana mipyä zinazoibuka zinaathiri leksimu ile kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, leksimu inaweza kupanuka maana yake ya kileksika au kubanika maana yake au kupanuka na kubanika maana mtawalia kutegemea na aina ya badiliko ambalo leksimu hiyo imepitia. Leksimu inapopanuka maana, wizani wa leksimu hiyo unaongezeka na kusudio lake kupungua na wakati inapobanika maana, wizani wa leksimu hiyo unapungua na kusudio lake katika mawasiliano kuimarika. Aidha, leksimu nyingine ziliweza kuitia uemeshajimaana uliokamilifu au usiokamilifu huku nyingine zikipitia msawajikomaana au zikipitia uemeshajimaana na msawajikomaana mtawalia tukilinganisha na maana yake asilia.

## **MAREJELEO**

- Aitchison, J. (2003) *Words in the Mind: An Introduction to the Mental Lexicon*. Oxford: Blackwell Publishing.
- Bloomfield, L. (1933) *Language*. New York: Holt, Reinhart and Winston.
- Bloomfield, L. (1933) *Language*. London: Compton Printing ltd.
- Blutner, R. (1998) Lexical Pragmatics in *Journal of Semantics* 15: 115-162.
- Carston, R. (2002) *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Oxford: Blackwell Publishing.
- Carston, R. (2004) *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Oxford: Blackwell Publishers Limited.
- Cruse, D.A. (2000) *Meaning in Language: An Introduction to Semantics and Pragmatics*. USA: Oxford University Press.
- Cuddon, J.A. (1979) *A Dictionary of Literary Terms* (2<sup>nd</sup> ed). Great Britain: Andre Deutch Limited.
- Graddol, D. J. Cheshire & J. Swann, (1987) *Describing Language*. Michigan: Open University Press.
- Fromkin, V. & R. Rodman, (1974) *An Introduction to Language* (4<sup>th</sup> ed). New York: Rinehart and Winston, Inc.
- Fromkin, V. & R. Rodman, (1993) *An Introduction to Language* (5<sup>th</sup> ed.). New York: Harcourt Brace College Publishers.
- Habwe, J. H. (1999) *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya PhD. (Haijachapishwa).
- Habwe, J. & P. Karanja, (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Habwe, J. M. Assumpta, & J. Nyonje, (2010) *Darubini ya Isimujamii: Kwa Shule na Vyuo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Hock, H. H. & D. B. Joseph, (1996) *Trends in Linguistics Studies and Monographs 93: Language History, Language Change and Language Relationship; An Introduction to Historical and Comparative Linguistic*. New York: Mouton De Gruyter.

Hollmann, W.B. (2009) *Semantic Change*, Chapter 35, [www.lancaster.ac.uk>staff>hollmann](http://www.lancaster.ac.uk/staff/hollmann).  
13.6.2017, saa 2: 30 usiku saa za Afrika Mashariki.

Horn, L.R. & G.Ward, (2004) *The Handbook of Pragmatics*. Oxford: Blackwell.

Jeffers, J. R. & I. Lehiste, (1979) *Principles and Methods for Historical Linguistics*. London: The MIT press-Cambridge, Massachusetts.

Kolaiti, P. & D. Wilson, (2012) *Corpus Analysis and Lexical Pragmatics: An Overview*. <http://www.phon.ucl.ac.uk/home/deirdre>, 27/5/2017, 1.36 za usiku na sekunde 45 saa za Afrika Mashariki.

Leech, G. (1983) *Principles of Pragmatics*. London: Longman.

Levinson, S. (1983) *Pragmatics*. Cambridge University Press.

Marmaridou, S.A. (2000) *Pragmatic Meaning and Cognition*. Amsterdam: John Benjamins.

Massamba, D.P. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

McMahon, A.M.S. (1994) *Understanding Language Change*. New York: Cambridge University Press.

Mdee, J.S. K. Njogu, and A. Shafi, (2011) *Kamusi ya Karne ya 21*, Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Mmbwanga, K.F. (2010) *New words and Meanings on Facebook: A Lexical Pragmatics Analysis*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Murphy, L. (2003) *Semantic Relations and the Lexicon*, Cambridge: C.U.P.

Muyuku, J.A. (2009) *Language Mixing in the Language of Advertising: A Case Study of Commercial Banks and Mobile Telecommunications in Kenya*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Njimu, P.N. (2010) *Lexical adjustments of sports language in three Kenyan Newspapers*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Ochichi, A.K. (2013) *Uwazi na Umaanisho: Usimbaji maana kimazungumzo katika Ekegusii na Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Ochoki, B.M. (2010) *Pragmatics interpretation constraints in Kenyan Hip Hop Lyrics*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Ohly, R. (1977) Patterns of New-coined Abstract Terms (Nominal forms) in Modern Swahili katika Swahili Studies in *Journal of the Institute of Kiswahili Research* (vol.47/1). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pp 1-14.

Palmer, F.K. (1981) *Semantics*. Cambridge: C.U.P.

Philip, H. (1977) *New Words for Old*. London: Hamish Hamilton.

Pyles, T. and J. Algeo, (1964) *The Origins and Development of the English Language* (3rd ed.). New York: Jovanovich, Inc.

Radford, A. M. Atkinson, D. Britain, H. Clahsen and A. Spenser, (1999) *Linguistics: An Introduction*. New York: Cambridge University Press.

Schiffrin, D. (1994) *Approaches to Discourse*. Oxford: Blackwell publishers.

Schroder, H. (2012) A Relevance-Theoretical Analysis of Intercultural Misunderstanding in Global Communication in *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*. Vol. 2. pp.44.

Searle, J. R. (1975) Indirect Speech Acts in P. Cole and J. Morgan (eds). *Syntax and Semantics 3*. New York: Academic Press, pp. 59-52

Simiyu, C. N. (2016) *The Portrayal of men and women in selected Bukusu Circumsition Songs: A Lexical Pragmatic Approach*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Sperber, D. & D. Wilson, (2007-2008) *Relevance: Communication and Cognition*. Wiley: Blackwell.

The Bible Society of Kenya & The Bible Society of Tanzania (1997) *Biblia: Maandiko Matakatifu*. Dodoma & Nairobi: Published jointly by The Bible Society of Tanzania & The Bible Society of Kenya.

TUKI, (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughu*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors ltd.

TUKI, (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la tatu). Dar es Salaam: University Press. East Africa Ltd.

Ullmann, S. (1957) *The Principles of Semantics*. Oxford: Basil Blackwell.

\_\_\_\_\_, S. (1970) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell & Mott ltd.

\_\_\_\_\_, S. (1972) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell Paperblack.

Wambugu, W.M. (2010) *Semantic Shifts In Gikuyu Lexemes: A Lexical Pragmatic Approach*. University of Nairobi. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Wilson, D. (2003) Relevance and lexical pragmatics in *Italian Journal of Linguistics* 15.2:273-291

Wilson, D. (2006-07) Lecture notes on *Issues in Pragmatics* (PLNI 3001).

Wilson, D. & R. Carston, (2007) *A unitary approach to lexical pragmatics: Relevance, inference and ad hoc concepts* from <http://www.phon.ucl.ac.uk/home/deirdre/index3.html> 17.4.2017, 1:20 na sekunde tisa, usiku, saa za Afrika Mashariki.

Wilson, D. (2007-08) Lecture Notes on *Pragmatic Theory* (2001).

## **KIAMBATISHO**

### **SAMPULI YA MASWALI**

Mimi ni mwanafunzi wa Uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu jinsi maneno ya Kiswahili yanabadilika maana kulingana na muktadha wa matumizi. Karibuni katika utafiti huu na ujumbe mtakaopeana utakuwa wa siri. Hustahili kupeana jina lako katika mahojiano haya.

1. Unaweza kukadiriaje kiwango chako cha ujuzi wa Kiswahili?
  - a. Kiko Juu zaidi
  - b. Kiko juu
  - c. Wastani
  - d. Kibaya
2. Umri wako?
3. Ulizaliwa katika kaunti gani?
4. Je, unadhani maneno ya Kiswahili yamepata maana mpya?
5. Je, unaweza kutupa mfano wa neno ambalo unadhani limebadilika maana?
6. Je, ukipewa mifano ya maneno, unaweza kutupa maana zake?
7. Kati ya maana za maneno ulizotupa, zipyi unapendelea kutumia? Zile za Kiswahili sanifu au zile mpya?
8. Tupe sababu za kutumia maana mpya za maneno uliyotupa.
9. Je, unawasiliana na wenzako kwa urahisi unapoyatumia maneno haya kwa maana mpya ulizotupa?